13 Ahoaho Seuta akawamba wandima, 'Mzengetezeni sigi za mwe miundi na mwe mikono mkamwase chongoi kwe kiza, uko endaaiye na kuuma meno.' "
14 Yesu akabindiizia kwa kugombeka, "Wantu wekwetangwao ni wangi, iya wekusagulwao niwacheche."

*Yesu auzwa mbui kuiha ushuu*
*Maliko 12:13-17; Luka 20:26*

15 Nee Mafalisayo wakahauka na kuita sia ya kuteganya wendavyo wamgwiye Yesu kwa ntamwiizi zakwe.
16 Aho wakawaagiiya wahina wao hamwe na wahina wa kizumwezumwe cha Mahelode. Wakamuuza, "Mhinyi, tamanya wee ni mntu yedi na wahinya sia ya Muungu ya wantu kugosoa yekuwayo yedi, khumwogoha mntu yoyose kwamana ya ukuu wakwe na ukuu wakwe kwako khio kintu.
17 Haya tambie wee waona viivihi? Ni vyedi kumuiha ushuu kwa seuta mkuu wa Lumi hambu tisekumuiha?"
18 Yesu akamanya nteganyi zao za ufyaimi akawagombeka, "Nywie ni wahokho, kwambwai mwanigeeza kwa kunihega?
19 Nionyeshani iyo sensi iihayo ushuu." Nawo wakamwekha sensi mwenga.
20 Ahoaho, Yesu akamuuza, "Cheni na magondo aya ni ya ndai?"
21 Wakatambaisa, "Ni seuta mkuu wa lumi." Aho Yesu akawamba, "Ya seuta mkuu wa lumi mwekheni seuta mkuu wa lumi na ya Muungu mwekheni Muungu."
22 Wekusikiavyo ivyo nee wahondomaa, wakambada wakaita.

*Yesu auzwa mbui ya uyuyuko*
*Maliko 12:18-27; Luka 20:27-40*

23 Msi uwouwo wamwe wa Masadukayo wagombekao wekufao khawayuyuka vituhu wakamtimia Yesu.
24 Na kumwamba, "Mhinyi, Musa kagombeka mntu inga akategua na akauya na nyuma na khekubada mwana, yakundigwa nduguye amtegue uyo mvyee mwekufiiwa ni mgosi, ili ampatie wana.
25 Hanu hetu nee kuwa na wandugu mfungate. Wabosi kategua nee auya na nyuma na khekujaiwa mwana, akadoigwa ni nduguye uyo mvyee mwekufiiwa ni mgosi.
26 Vikagosoka ivyoivyo kwa ndugu wakaidi na wantatu, adi wose mfungate.
27 Bada ya ndugu ao wose kuuya na nyuma na yuda mvyee nae akauya na nyuma.

28 Wendaho ubue uwo msi wa uyuyuko wendaho wayuyuke mvyee uyo endaawe ni mkaza ndai wamwe wa wada wandugu mfungate? Kwaviya wose mfungate nee wamtegua."
29 Yesu akawatambaisa, "Nywie mwaga kwaajii khammanya Maandiko ya Muungu wala udaho wa Muungu.
30 Kisingi wantu wendaho wayuyuke khawana wategulwe wala kutegua, iya wendawawe inga wandima wa uwanga kwa Muungu.
31 Iya kwa ida mbui ya wantu kuyuyuka tambe khamzati kusoma yada ekuwagombekayo Muungu?
32 'Miye ni Muungu wa Iblahimu na Muungu wa Isaka na Muungu wa Yakobo!' Yee khie Muungu wa wekuuyao na nyuma, iya ni Muungu waugima."
33 Yada mazumwezumwe ya wantu yekutegeezaho mahinyo yakwe wakahondomazwa muno.

*Amli kuu*
*Maliko 12:28-34; Luka 10:25-28*

34 Mafalisayo wekusikiaho kuwa Yesu kawatwiiza Masadukayo, na wakakintana hamwe.
35 Yumwe wa Mafalisayo ambae amanya miko, akamuuza Yesu kwa kumgeeza.
36 "Mhinyi mwe miko ni amli ihi yekuwayo khuu?"
37 Yesu akamtambaisa, " 'Mkundise Zumbe Muungu yako kwa moyo wako wose na muye wako wose na kwa akii zako zose.'
38 Inu nee amli khuu na ya bosi.
39 Yakaidi yaigana na inu, 'Mkundise mntu yoyose inga wekundisavyo wee mwenye.'
40 Miko yose ya Musa na mahinyizo ya Waoni zizengwa na amli izi mbii."

*Mbui ya Klistu mwohozi*
*Maliko 12:35-37; Luka 20:41-44*

41 Kisingi Mafalisayo wekukintanaho hamwe, Yesu akawauza.
42 "Nywie mwaona viivihi kuusu klistu mwohozi? Yee ni mwana wa ndai?"
Wakamtambaisa, "Yee ni mwana ya Daudi."
43 Yesu akawauza, "Yadahika viivihi Daudi akaongweewa na Muye wa Muungu amwetange Klistu ni 'Zumbe?' Kwaviya kagombeka,
44 'Zumbe kamwamba Zumbe yangu,
Ekaa he mkono wangu wa kuume
Adi nendaho niwavote wamasa wako.'
45 Akawa Daudi amwetanga Klistu 'Zumbe', yadahika viivihi Daudi kuwa mwanawe?"
46 Khahana mntu yoyose mwekudaha kumtambaisa Yesu mbui iyo, na kuvokea msi uwo khahana mwekudaha kugeeza kumuuza vituhu dodose.

# 23

*Yesu awaakia wahinyi wa Miko na Mafalisayo*
*Maliko 12:38-39; Luka 11:43,46; 20:45-46*

1 Naho Yesu akawamba wada wantu wangi na wangi wekuwao aho, hamwe na wahina,
2 "Wahinyi wa Miko na Mafalisayo nee wekwekhigwao udaho wakusosoa miko ya Musa.
3 Ivyo tozani na mtongee dodose wendado wawagombekee. Iya mwesekutongea yada wayagosoayo, kwaviya wowo khawayatongea yada wayahinyayo.
4 Wadoa maafuushi yazamayo na kuwabadika wantu mwe mawega, akini wowo wenye khawakunda kuidon'ta hata kwa chaa wadahe kuyenua.
5 Wao wagosoacho mbui zao zose ili kwakweonyesha he meso ya wantu. Kwaviya wavaa kwenye vyeni vyao na mwe mikono yao ntii khuu za babu ambavyo viandikwa miko ya Musa, na kuomeea mafundo mwe magwanda yao.
6 Wakunda kwekaa phasi za kutunywa mwe ntafuno na vigoda vya kutunywa mwe Nyumba za kukintania Wayahudi.
7 Wakunda kuuguswa kwa kutunywa gwiiyo na nakwetangwa na wantu. 'Mhinyi.'
8 Iya nywie wantu wasekuwetanga 'Mhinyi.' Kwaviya mhinyi yenu ni yumwedu, na nywie wose ni ndugu.
9 Nahodu mwesekumwetanga mntu yoyose 'Tate' hanu mwe inusi kwaviya Tate yenu ni yumwedu, mweuko uwanga kwa Muungu.
10 Naho mwesekwetangwa 'Wagookezi,' Kwaviya mgookezi yenu ni yumwedu nee Klistu.
11 Na mntu yoyose ambae akunda kuwa mgookezi, akundigwa awe awagosoeya ndima wenziwe.
12 Na mntu yoyose egosoaye kuwa mkuu Muungu enda amtende mdodo na yoyose etendae mdodo Muungu enda amtende mkuu.

*Yesu awawakia wahokho*
*Maliko 12:40; Luka 11:39-42,44,52; 20:47*

13 "Mmbwii yenu, wahinyi wa miko na Mafalisayo mwekuwao wahokho! Uvi muuvugaa wa Useuta wa Muungu hemeso ya wantu. Nywie wenye khamwengia umo, naho khamuwabada watuhu wakundao kwengia wengie.

14 Mmbwii yenu wahinyi wa miko na
Mafalisayo nywie wahokho! Mwada
khande mwe nyumba za wavyee wekufi-
wao ni wagosi, nywie mwetenda kuwa ni
wedi mwavika kisingi kileacho. Kwaajii
iyo mwenda mwekhigwe sugusa khai.
15 "Mmbwii yenu, wahinyi wa miko
na Mafalisayo, wahokho! Mwatamba
mwe mazimshindo na mwesanga khavu
ili mmuohoe mntu esae kuwa Myahudi
awe Myahudi mkabinda awatongea nywie,
iya mkabinda kumpata mwamgosoa awe
mntu akundigwae kuita mwe si ya moto
wesao kukomeka inga nywie wenye.
16 "Mmbwii yenu, wagookezi matuntu!
Nywie mwahinya, 'mntu akaaha kwa
Nyumba ya Muungu khio kintu, iya akaaha
kwa zahabu yekuwayo mwe Nyumba ya
Muungu kuaha kwakwe kwenda kumtoze.'
17 Nywie matuntu wahezi! Kihi ambacho
ni cha mana muno, ni zahabu hambu
Nyumba ya Muungu yekugosoayo iyo za-
habu iwe ya Muungu!
18 Naho mwahinya mntu akaaha kwa
ingo da kulaviya malavyo khio kintu, iya
akaaha kwa funge ikuikwayo uwanga ya
ingo, kuaha kwakwe uko kwamtoza.
19 Nywie matuntu kweikwei! Ni kihi
chekuwacho kikuu muno. Ni funge hambu
ingo ambado dagosoa iyo funge iwe ya
Muungu.
20 Kwaiyo mntu aahae kwa ingo da
kulaviya malavyo, kuaha kwa ido ingo na
vintu vyose vyekuwavyo uwanga yakwe.
21 Na aahae kwa Nyumba ya Muungu,
kaaha kwa iyo Nyumba ya Muungu na
yuda ekaae ndani yakwe.
22 Na aahae kwa uwanga kwa uwanga
kwa Muungu, aaha kwa kigoda cha kiseuta
cha Muungu na kwa uyo ekaae uwanga
yakwe.
23 "Mmbwii yao, wahinyi wa miko na
Mafalisayo, wahokho! Mwawatoza wantu
zaka ya mani ya halufu ntana, na binzali,
na bwache, na uku mwabada mbui za mi-
agiiyo inga viya haki na mbazi na uzumizi.
Aya nee asa mkundigwayo kuyagosoa na
mwesekujaa yada matuhu.
24 Wagookezi matuntu! Mwalavya
nisi mwe vyakudomeea, akini mwakhia
ngamia!
25 "Mmbwii yenu Wahinyi wa Miko na
Mafalisayo wahokho! Mwasunta kikombe
na kalai kwa chongoi, iya ndani mwabada
kumema vintu mwe kupatavyo kwa kuwa-
hoka wantu na uchoyo.
26 Nywie Mafalisayo matuntu! Vokani
kusunta kikombe ndani, na chongoi chen-
dakiwe kisuntika.
27 "Mmbwii yao wahinyi wa miko na
Mafalisayo nyie wahokho! Mwaigana
na mambia yekusiswayo nchokaa ambayo
kwa chongoi yakaulwa kuwa ni matana,
akini umo ndani yamema mavuha ya
vimba na kia namna ya usama.
28 Viyaviya kwa chongoi nywie
mwaonekana kuwa ni wantu wedi, akini
kwa ndani mmema uhokho na kia namna
ya ufyaimi.

*Yesu awamba mafalisayo sugusa yao yezayo*

*Luka 11:47-51*

29 "Mmbwii yenu wahinyi wa miko
na Mafalisayo, wahokho. Mwayazengea
mambia ya waoni na mwayazengea na
kuhamba mbia za wantu wedi,
30 nywie mwagombeka, inga nee tiwaaho
kisingi cha wadaa wetu nee khatoku-
tongeana nao mwe ukomaji wa waoni!"
31 Ivyo mwesemea wenye kuwa nywie ni
uvyaigwa wa wantu wekukomao waoni
32 Aya iiganizeni ndima ida wadaa wenu
wekuivokayo.
33 Enywi uvyazi wa mdudu mwenye
sumu! Mwendamdahe viivihi kuhepa su-
gusa ya si ya moto wesao kukomeka misi
yose kwesiho kiisikizi?
34 Nee mana miye nawegaiiya nyie
waoni, wantu wenye akii na wahinyi,
mwenda muwakome na kuwagong'ondea
he mhamba na wamwe wao, na watuhu
mwendamuwatoe ngoda mwe nyumba za
kukintania Wayahudi na kuwaguusa kwa
kia mzi.
35 Ivyo lawama yose inda iwapate kwaa-
jii ya phome yose ya wantu wedi wa
Muungu yekwetiwayo uwanga ya inusi,
kuvokea phome ya Abeli ambae khekuwa
na hatia hadi ida ya Zakalia, mwana wa
Balakia ambae mumkoma he Nyumba ya
Muungu gatigati ya hantu hang'azi ha ingo.
36 Nawamba kwei, wantu wa kivyazi iki
chendachekhigwe sugusa kwaajii ya mbui
izi.

*Yesu ekuwakundisavyo wantu wa Yelusalemu*

*Luka 13:34-35*

37 "Nywie wantu wa Yelusalemu! Nywie
wantu wa Yelusalemu! Uwakomae waoni
wa Muungu na kuwatambikia maiwe
wada wose wekuagiiwao aha hako. Maa
nyingahi khigeeza kuwaika hamwe wana
wako kwangu, inga via nguku awatami-
iavyo wanawe asi ya mawawa yakwe,
akini khamwekukunda.
38 Kauwa Muungu endaaibade Nyumba
yenu yenda ibomolwe na kubadwa ukiwa.
39 Nakwamba, khuna unikauwe vituhu
hadi kisingi wendaho ugombeke, 'Ajaiwe
uyo ezae kwa zina da Zumbe.' "

# 24

*Yesu atamwiiya kubanangwa kwa Nyumba ya Muungu*
*Maliko 13:1-2; Luka 21:5-6*

1 Yesu akalawa he Nyumba ya Muungu,
wahina wakwe wakamtimia na kum-
wonyesha mazengo ya Nyumba ya
Muungu.
2 Yesu akawamba, "Ni sawa, mwadaha
kuyakauwa aya yose! Kwei nawamba,
khahana hata iwe dimwe dendado disigae
uwanga ya iwe tuhu, kia iwe dendadibo-
molwe."

*Suuba na usuumizi*
*Maliko 13:3-13; Luka 21:7-19*

3 Yesu ekuwaho kekaa he muima wa
Mizaituni, wahina wakwe wakamtimia
Yesu ili wawe ikedu, wakamuuza, "Tambie,
mbui izi zendazilawiiye ini, na ni ntangio
ihi ya kweza kwako na ntangio ya kisikiizi
cha inusi ni mbwai."
4 Yesu akawatambaisa, "Kuwani meso
mntu asekuwatiiya.
5 Kwaviya wangi wendaweze na wen-
dawatumiye zina dangu na kugombeka,
'Miye nee Klistu, nao wenda wawatiiye
wangi.' "
6 Mwenda mtegeeze mbui za khondo
na ufukufuku wa khondo kauweni
mwesekuogoha, kwaviya aya yakundigwa
yalawiiye, iya kia kisikiizi chenye khak-
izati.
7 Wantu wa si mwenga wenda watoane
khondo na wantu wa si ntuhu, wantu wa
useuta umwe wenda watoane khondo na
wantu wa useuta mtuhu. Kwendakuwe
na saa na mizingizo mwe hantu mbaimbai
mwe inusi.
8 Yose ayo ni inga usungu wa bosi wa
kwefungua mwana.
9 "Naho mwenda muemewe na wantu na
kuwasuumiza na kukomwa. Wantu wa Si
zose wenda wawakime kwaajii kunizumiia
miye.
10 Naho wangi wenda wabade kuzumiia
kwao na wendawahitukane na khawana
wakundisane katu.
11 Wendawalawiiye waoni wangi wa
uhokho, nao wenda wawatiiye wantu
wangi.
12 Naho ukundiso wa wantu wangi
wenda uhungue, kwaajii mavigaviga
yenda yawe yamema.
13 Na yoyose endaeagooke mwe untinti-
mavu adi kisikiizi, uyo nee endaeaoholwe.
14 Mbui Yedi ya useuta wa Muungu inda
ibiikiwe mwe inusi yose, ili wantu wose
waimanye nee kisikiizi chendahocheze.

*Suuba khuu*
*Maliko 13:14-23; Luka 21:20-24*

15 "Ivyo mwendaho muone mbui ya
kutisa na dietado ubanasi, digooka he
Nyumba ya Muungu inga ekugombekavyo
muoni Danieli, ivyo kia asomaye na
amanye mbui iyo."
16 Aho, wada wekaao Uyahudi waguukie
he miima.
17 Yoyose mwe uwanga ya taa da nyumba
yakwe asekuseeya kudoa chochose kulawa
mwe nyumba yakwe.
18 Ekuwae tanga asekuuya kaya kudoa
gwanda dakwe.
19 Mmbwii yao wakina mmaa wekwen-
uao maifu na waokhesao misi iyo!
20 Ombezani Muungu kuguuka kwenu
kusekuwa kisingi cha khusi hambu Msi wa
Kuhumuiza.
21 Kwaviya kisingi icho chendakiwe na
suuba khuu ambayo khaizati kulawiia ku-
vokea aho bosi wa inusi adi ivyeo, wala
khakina kilawiiye vituhu.
22 Iya Muungu kahunguza misi izo, inga
khekugosoa ivyo khahana mntu ambae
nee kaoholwa, na Muungu kazihunguza
kwaajii ya wantu wakwe ekuwasaguwao.
23 "Kisingi icho mntu yoyose akawamba,
'Klistu, yuhanu!' Hambu 'Yuhada,'
msekuzumiiya."
24 Kwaviya wendawalawiiye wantu
wetangao Klistu akini khio, naho
wendawalawiiye waoni wa uhokho.
Wendawagosoe ntangio na vihii vikuu
vya kudaha kuwaza, vikadahika hata
wekusagulwao ni Muungu.
25 Kauwani! Khibindiiza kuwahaza kae
kabla mbui izo khazizati kulawiia.
26 "Kwaiyo, mntu yoyose akawamba,
'Klistu yuuko he nyika, msekuita.'
Hambu wakagombeka, 'Klistu yuuko gati,
msekuzumiiya.'
27 Kwaviya inga umbauwa umuikavyo
kulawa awiyo da zua adi engiiyo da zua,
nee ivyo vyendavyoviwe kweza kwakwe
Mwana wa Mntu.
28 "Hada weiho mzoga, neaho wakin-
tanaho tai.

*Kweza kwakwe Mwana wa Mntu*
*Maliko 13:24-27; Luka 21:25-28*

29 "Maa misi iyo za suuba zendaho zem-
boke, Muungu endaadihitue zuwa kuwa
kiza na mweenge nayo khaina ilavye
mng'ao na ntoondo zendazigwe kulawa
uwanga, viyaviya endaazisingise nguvu za
uwanga.
30 Aho wenda uoneke ntangio ya Mwana
wa Mntu uwanga kwa Muungu na wantu
wose mwe inusi wenda watoe bwaimbo,
wenda wamwone Mwana wa Mntu akeza
uwanga ya maangwi ya uwanga kwa
Muungu kwa udaho na ukuu mwingi.

31 Nae endaawaagiiye wandima wa uwanga kwa Muungu uku watoa gunda divumado muno, nao wendawawaike hamwe wekusagulwao ni Muungu kulawa phande zose nne za inusi, kulawa kisikizi iki cha inusi adi kisikizi kituhu cha inusu.

*Kwehinya kulawa kwa mti wetangwao mtini*

*Maliko 13:28-31; Luka 21:29-33*

32 “Mwehinye kulawa kwa mti wa mkuyu, muonaho matambi yakwe yamema mani, mwamanya kisingi cha fua kibua.

33 Ivyoivyo, mwonaho mbui izo zikagosoka mmanye kuwa Seuta yuhehi muno.

34 Nawamba kwei, wantu wa kivyazi iki khauna wemboke kabla ya mbui izo khazizati kulawiiya.

35 Uwanga kwa Muungu na inusi zendazemboke, iya mbui zangu khazina zemboke katu.

*Khahana amanyae msi wala saa*

*Maliko 13:32-37; Luka 17:32-37; Luka 17:26-30,34-36*

36 “Kwa mbui ya msi uda na saa ida khahana amanyae, ata wandima wa uwanga kwa Muungu wala Mwana, iya Tate ikedu nee amanyae msi uwo.

37 Inga yekuwavyo kisingi cha Nuhu, nee vyendavyoviwe kweza kwakwe Mwana wa Mntu.

38 Kwaviya kisingi icho, kabla ya mazi mangi kuigubika inusi, wantu neewawa wakada na kudomea, wakategua na kutegulwa, hadi Nuhu ekwengiaho mwe ida Safina.

39 Khawokumanya kuna mbwai hadi yada mazi mangi yekulawiiyaho, kuwakumba wose. Nee vendavyoviwe kisingi Mwana wa Mntu endahoeze.

40 Kisingi icho wantu waidi wendawawe tanga yumwe endaadoigwe na mtuhu endaabadwe.

41 Wavyee waidi wendawawe wakabunduga khande, yumwe endaadoigwe na mtuhu endaabadwe.

42 Ekauweni, kwaviya khammanya msi endahoeze Zumbe yenu.

43 Iya mmanye mbui inu, inga mwenye nyumba ati nee kamanya msi mbavi endahoabue, nee akacheeza, wala khekuwa aibadie nyumba yakwe itulwe.

44 Viyaviya nanywi mwekae meso, kwaviya Mwana wa Mntu endaeze saa mwesayokuikauwiya.

*Mndima mkwei na mwesekuwa mkwei*

*Luka 12:41-48*

45 “Nindai mndima mkwei na mwenye akii, ambae zumbe yakwe endaamwiike agookee weziwe na awekhe khande kwa kisingi chakwe?

46 Yendaiwe vyedi mndima uyo ambae zumbe yakwe endahoeze endaambwiiye agosoa ivyo.

47 Nawamba kwei, endaamwiike mndima uyo agookee vintu vyakwe vyose.

48 Inga mndima ni mfyaimi akegombekea mwe moyo, ‘Zumbe yangu endaacheewe kuuya,’

49 nae akavoka kuwatoa wandima weziwe, na kuvoka kuda na kudomea hamwe na wakozi,

50 zumbe yakwe mndima uyo endaeze msi ambao mndima khamkauwiiya na saa ida ambayo khaimanya.

51 Endaamsuumize vifyaimi na kumwiika hamwe na wahokho. Uko kwendakuwe na ndio na kuuma meno kwa usungu.

# 25

*Msimo wa wandee kumi dimwe*

1 “Useuta wa Muungu wendauigane na wandee kumi dimwe wekudoao taa zao, na wakaita kumhokea zumbe wa ndoza.”

2 Washano nee niwahezi na washano wawa wenye akii.

3 Wada wahezi wadoa taa zao, iya khawekudoa mavuta ya kuomeea,

4 Iya wada wenye akii wadoa taa zao na mavuta ya kuomeea mwe nchupa zao.

5 Kwaviya mteguzi kacheewa kweza, wada wandee wose wakasikha na wakagona.

6 “Kio kikuu kukawa na vuzo, ‘Homgwiiyo, homgwiiyo! Mteguzi eza, hitani mkamhokee.’

7 Aho wada wandee wose wakenuka wakaziika vitana taa zao.

8 Wada wahezi wakawamba wada wenye akii, ‘Tipangieni mavuta kwaviya taa zetu zafa.’

9 Akini wada wenye akii wakawamba, ‘Khayanayatitoshe nywie na swiswi! Ni ebae mwiite kwa watagao mavuta mkague wenye!’

10 Aho wada wandee wahezi, wakaita kugua mavuta. Uku nyuma mteguzi akabua, na wada wekuwao watayali wakengia hamwe nae mwe nyumba ya wiya, na uvi ukavugalwa.

11 “Yekwembokaho ayo wada wandee watuhu wakeza, na kwetanga. ‘Zumbe, Zumbe, tivuguiye uvi!’

12 Akini yee akawatambaisa, ‘Nawamba kwei,’ khiwamanya nywie.”

13 Ahoaho Yesu akawamba, “Ekauweni, kwaviya khammanya msi wala saa.

*Msimo wa wandima watatu*

*Luka 19:11-27*

14 “Naho Useuta wa Muungu inga mntu yumwe mwe kukunda kutamba, akawetanga wandima wakwe, akawekha vintu vyakwe.

15 Akamwekha kadii ya udaho wa kia yumwe, yumwe vifuko vya hea vishano na mtuhu vifuko vya hea viidi na mtuhu kifuko cha hea kimwe, na ahoaho akatamba.

16 Yuda mwe kwekhigwa vifuko vya hea vishano akazigosoeya biashaa zikavyaa vifuko vya hea vishano ntuhu.

17 Viavia yuda mwe kwekhigwa vifuko vya hea viidi nazo zikavyaa vifuko vya hea vituhu.

18 Iya yuda mwe kwekhigwa kifuko cha hea kimwe, yee akaita akafuka tubwi na kuifukia kia kifuko cha hea ya zumbe yakwe.

19 “Yekwembokaho kisingi kilehacho, yuda zumbe wa wada wandima akauya, na kugosoa ntaazia nao.

20 Yuda mndima mwe kwekhigwa vifuko vishano vya hea akeza uku kaeta vifuko vishano vya hea zekuongezekazo. Akagombeka. ‘Zumbe kunekha vifuko vishano vya hea, kauwa kiongeza mituhu mishano.’

21 Zumbe wakwe akamwamba, ‘Vyedi mndima yedi, nee kuwa yedi kwa vintu vicheche, ninda nikuike uwe mgookezi kwa vintu vingi. Soo ushiiki nyemi ya zumbe yako!’

22 Yuda mwekwekhigwa vifuko viidi vya hea mbii nae akeza. Akagombeka, ‘Zumbe kunekha vifuko viidi vya heya mbii. Kauwa kieta vifuko vituhu viidi.’

23 Zumbe yakwe akamtambaisa, ‘Kutenda vyedi muno mndima yedi na kuwa mzumiiwa mwe mbui ndodo, nendanikuike kuwa yedi kwa vintu vingi. Soo ushiiki mwe nyemi ya zumbe yako!’

24 Naho yuda mndima mwekwekhigwa kifuko kimwe cha heya akeza na kugombeka, ‘Zumbe, namanya kuwa wee ni mntu utogae, wabonda kwesiho kuhanda na kukisanya kwesiho kwetiya mbeyu.

25 Khikuogoha kwaza kifiko chako cha hea, na khiifisa kifuko kimwe cha heya yako mwe sanga. Doa kifuko kimwe cha heya yako.’

26 Zumbe yakwe akamwamba, ‘Wee ni mndima mfyaimi na mbwa! Kumanya kuwa, miye nabonda hantu ambaho nchekuhanda, nadoa hantu ambaho nchekwetiya mbeyu.

27 Kukundingwa kuika kifuko cha hea kwa walavyao nyongeza, na miye mwe kifuko changu nee khipata nyongeza.

28 Haya mhokeni icho kifuko cha hea mkamwekhe yuda mwenye vifuko kumi.

29 Kwaviya mwena endaekhigwe na ngeeko. Na yuda mwesena hata kia enacho endaahokwe.

30 Mtambikeni uyu mndima mfyaimi chongoi mwe kiza! Uko kundakuwe na ndio na kuuma meno kwa usungu.’

*Kuamwiiwa kwa kisikiizi*

31 “Mwana wa Mntu endahoeze na ukuu wakwe na wandima wa Muungu wakawa hamwe nae, aho endaekae mwe kigoda chakwe cha Useuta na ukuu.

32 Wantu wa si zose wendawakintane hemeso yakwe, nae enda awaike wantu inga via mwiisi awaikavyo ngoto hantu hakwe na mbuzi hantu hakwe.

33 Aho endaawaiike ngoto phande ya kuume na mbuzi phande ya kumoso.

34 Naho Seuta endaawambe wada wa phande ya kuume, ‘Sooni nywie mwekujaiwao na Tate yangu, hokeani Useuta mwekuikiwao kae kuvokea kugosolwa kwa inusi.

35 Kwaviya nekhiwa na saa, mkanekha khande, na nekhiwa na khiu mkanidomeza na nekhiwa mgeni mkanihokea,

36 nekhiwa mwazi mkanivika magwanda na nekhiwa mtamu mkeza kunikauwa na nekhiwa mwe kifungoni mkeza kunivuiiya.’

37 Aho awo wantu wedi wenda wamtambaise na kumwamba, ‘Zumbe ni ini, tekukuonaho una saa tikakwekha khande hambu ukawa na khiu tikakudomeza mazi?

38 Ni ini tekukuonaho umgeni na swie tikakuhokea na tekukuonaho umwazi tikakuvika magwanda?

39 Na ni ini tikuona ukawa mtamu tikeza kukukauwa hambu wekuwaho mwe kifungo tikeza kukuvuiiya.’

40 Nae Seuta endaawatambaise, ‘Kwei nawamba, chochose mwekuwagosweado wamwe wa awa wandugu zangu mnigosweeya miye!’

41 “Ahoaho endaawambe wada wekuwao phande yakwe ya kumoso, haukeni aha hangu, nywie mwe kubadiwao lazi, hitani mwe moto wa misi zose kwesaho kukomeka na wekuikwao kae kwaajii ya ibiisi na wandima wakwe!

42 Kwaviya nekhiwa na saa khamwekunekha khande na nekhiwa na khiu khamwekunidomeza mazi;

43 Nekhiwa mgeni nywie khamwekunihokea, na nekhiwa mwazi khamwekunivika magwanda na nekhiwa mtamu khamwekweza kunikauwa, na nekhiwa mwe khiwa mwe kifungo khamwekweza kunivuiiya.”

44 Wowo wenda wamtambaise, “Zumbe, ni ini, tekukuonaho una saa na khiu,

hambu ukawa mgeni na umwazi, na ukawa mtamu, na ukawa mwe kifungo, khatikweza kukuambiza?"
45 Nae endaawatambaise, "Nawamba kwei kiya mwekuemeavyo kumwambiiza yumwe wa wadodo awa mwemea kuniambiiza miye."
46 "Awa wendawaite kwe usuumizi wa misi zose zesazo kuwa na kisiikizi, na wada wantu wedi wenda waite kwe ugima wa misi zose zesazo kuwa na kisiikizi."

# 26

*Nteganyi za kumkoma Yesu*
*Maliko 14:1-2; Luka 22:1-2; Yohana 11:45-53*

1 Yesu ekubindaho kuwahinya ayo yose, akawamba wahina wakwe,
2 "Mwamanya kuwa bada ya misi miidi indaiwe ni sikukhuu ya Pasaka, na Mwana wa Mntu endaalavigwe ili agong'ondewe mwe mhamba."
3 Naho wagookezi wa waviki wakakintana hamwe kwe ukumbi wa Mviki Mkuu zina dake Kayafa.
4 Wakagosoa nteganyi wendavyo wamgwiiye kwa sii kwa unyanyi na kumkoma.
5 Iya wakamba, "Isekuwa kisingi cha sikukhuu ama khivyo kunda kulawiiye khumbizi kwa wantu."

*Yesu etiiwa mavuta uko Besania*
*Maliko 14:3-9; Yohana 12:1-8*

6 Yesu ekuwaho Besania kaya kwa Simoni, mwekuwa na utamu wa nyoka.
7 Mvyee yumwe mwekuwa na nchupa ya iwe yetangwayo alibasta yenye mavuta yanukhiayo vitana ya yombe khuu, akamtimia hada Yesu ekwekaaho ada khande, na akamwetiiya ayo mavuta mwe mtwi.
8 Wahina wakwe wekuonaho ayo wakakimwa na kugombeka, "Kwambwai taza hea ivi!
9 Mavuta aya nee yatagwa kwa yombe khuu, na hea izo wekhigwe wakiwa."
10 Yesu akamanya mamakhanyi zao, akawamba, "Kwambwai mwampisha uyu mvyee? Yee kanigosoeya mbui yedi.
11 Wakiwa mnao misi yose, iya miye khamna muwe nami misi yose.
12 Mvyee uyu kanitiiya mavuta ili niwe tayali kwa maziko yangu.
13 Nawambeni kwei, hohose mweinusi ambaho Mbui Yedi yendaibiikiwe, kintu iki ekugosoacho mvyee uyu chendakitamwiiwe kwa khumbuso yakwe."

*Yuda Isikaliote amhituka Yesu*
*Maliko 14:10-11; Luka 22:3-6*

14 Naho Yuda Isikaliote, yumwe wa wada wahina kumi dimwe na waidi, akaita kwa wagookezi wa waviki,
15 akawamba, "Mwendamnekhe mbwahi nendahonimhituke Yesu kwenu?" Wakamtaazia ntii makumi matatu ya madini ya feza.
16 Kuvokea kisingi icho Yuda Isikaliote akaondeza phasi ya kumhituka Yesu.

*Yesu ada khande ya Pasaka hamwe na wahina wakwe*
*Maliko 14:12-21; Luka 22:7-23; Yohana 13:21-30*

17 Msi wa bosi ya sikukhuu ya mabumunda yesayo kugewa hamila, wahina wakaita kwa Yesu na kumuuza, "Wakunda tikuikie kuhi khande ya Pasaka?"
18 Yee akawatambaisa, "Hitani mwe mzi kwa mntu yumwe, na mmwambe, 'Mhinyi amba kisingi changu kibua, mwe nyumba yako nakunda niide khande ya Pasaka hamwe na wahina wangu.' "
19 Wahina wakatenda inga Yesu ekuwaagiiavyo, wakaandaa khande ya Pasaka.
20 Yekubuaho guoni, akekaa asi hamwe na wahina wakwe kumi dimwe na waidi.
21 Wekuwaho wakada, Yesu akawamba, "Nawambeni kwei, yumwe yenu endaanihituke."
22 Wahina wakaungumia muno, wakavoka kuuza yumweyumwe, "Ni miye Zumbe?"
23 Yesu akawatambaisa, "Agintae bumunda hamwe na miye mwe wiga nee endae anihituke.
24 Mwana wa Mntu aita zakwe inga Maandiko yagombekavyo, iya mmbwii yakwe mntu yuda amhitukae Mwana wa Mntu! Neeiwa ebae kwa mntu uyo inga khekuvyaigwa."
25 Yuda Isikaliote ambae nee mwe kumhituka akamuuza, "Mhinyi! Ivi ni miye?" Yesu akamtambaisa, "Eehe weye mwenye kugombeka".

*Khande ya Zumbe*
*Maliko 14:22-26; Luka 22:14-20; 1 Wakolinto 11:23-25*

26 Wekuwaho wakada, Yesu akadoa bumunda akamtogoa Muungu, akadibendua akawekha wahina wakwe akamba, "Doani mde unu nee mwii wangu."
27 Akakidoa kikombe cha divai akamtogoa Muungu akawekha akamba, domeani wose,
28 "Inu nee phome yangu iyonyeshayo Agane dangu ni dakwei, phome yetiwayo kwaajii ya wantu wangi kwa kuwausia mavigaviga.
29 Nawamba, khina nidomee vituhu divai ya mzabibu adi msi uda nendaho nidomee mphya hamwe na nywinywi mwe Useuta wa Tate yangu."

30 Wekubindaho kutoa wiya, wakahauka wakaita mwe muima wa mizeituni.

*Yesu amba pwii Petulo endavyoamuemee*

*Maliko 14:27-31; Luka 22:31-34; Yohana 13:36-38*

31 Aho Yesu akagombeka, "Kio cha ivyeo nywie wose mwendamniguuke kwaviya Maandiko yagombeka, 'Muungu endaamtoe mwiisi na tintimo da ngoto dendadiangadike.'

32 Iya bada ya miye kuyuyuka nendaniwaongwee uko Galilaya."

33 Petulo akamwamba Yesu, "Wose wakakubada miye katu khinanikubade."

34 Yesu akamwamba Petulo, "Kwei nakwamba, kio iki zogoo khadizati kukema wendauniemee maa ntatu."

35 Petulo akamwamba, "Hata nikakudigwa niuye na nyuma hamwe nawe khinanikubade katu." Wada wahina watuhu wose wakatamwiiya viyaviya.

*Yesu avika uko Getisemane*

*Maliko 14:32-42; Luka 22:39-46*

36 Yesu akaita hamwe na wahina wakwe adi hantu ekwetangwaho Getisemani akawamba, "Ekaeni hanu, miye naita kuvika."

37 Akamdoa Petulo hamwe na wada wana waidi wa Zebedayo, akavoka kuwa na usungu na uku aona kiyangayanga,

38 aho akawamba, "Nina usungu muno mwe moyo ata nihehi na kuuya na nyuma, ekaeni hanu na msekugona na muwe hamwe na miye."

39 Aho akaita mbee kidogo akagonea ifu, akavika akamba, "Tate yangu, usekutenda nengie mwe masuumizo yezayo isasa, khio inga nikundavyo miye iya inga ukundavyo wee."

40 Akawatimia wada wahina akawabwiia wagona, neamuuza Petulo, "Yaani khamwekudaha kucheeza hamwe na miye hata saa dimwe?

41 Msekugona iya vikani msekweza kwengia mwe mageezo. Kwaviya muye wakunda akini mwii unyong'onyea."

42 Akaita vituhu maa ya kaidi akavika, "Eee Tate yangu, ikawa khaidahika kuyembokea maasumizo haya makuu, naho ugosoe ukundavyo wee."

43 Akawatimia vituhu akawabwiiya wagona, kwaviya nee watozwa muno na usisiza.

44 Aho akawabada, akaita vituhu kuvika maa ya ntatu kwa mbui idaida.

45 Naho akawaitiya wada wahina, akawamba, "Mke mgonie na kuhumwiza? Kauwani, saa ibua na Mwana wa Mntu endaalavigwe kwa wantu wenye mavigaviga.

46 Enukani, titeni! Kauwani, eza yuda endaeanihituke."

*Yesu agwiwa*

*Maliko 14:43-50; Luka 22:47-53; Yohana 18:3-12*

47 Ekuwaho ake kugombeka, Yuda Isikaliote yumwe wa wada wahina kumi dimwe na waidi akabua, uku katongeana na zumwezumwe kuu da wantu wenye malungu na mapaange wekuwao waagiiwa na wagookezi wa waviki na wagookezi wa Wayahudi.

48 Yuda Isikaliote mwe kukunda kumhituka Yesu akawekha awo wantu ntangio, "Mntu uyo nendae nimuuguse kwa kumuumbatia uyo mgwiyeni."

49 Yuda Isikaliote akamtimia Yesu hehi akamuugusa, "Mhinyi nakuugusa!" Nee amuumbatia.

50 Yesu akamwamba, "Mbuyangu gosoa wekwezeado." Aho wada wantu wakamtimia nee wamfuntia na kumgwiiya Yesu.

51 Yumwe wa wada wekuwao hamwe na Yesu akasomoa tuni dakwe khuu, akamsenga gutwi mtumwa wa mviki mkuu.

52 Yesu akamwamba, "Vuza tuni dako mwe kisafuo, kwaviya yoyose atumiae tuni kwa kukoma wantu, endaauye na nyuma kwa tuni.

53 Ivi tambe khammanya kuwa nadaha kumwombeza uwambiizi Tate yangu akanietea mazumwezumwe kumi dimwe na mbii ya wandima wakwe wa Muungu?

54 Iya nikagosoa ivyo Maandiko ya Muungu yendayaiganie viivihi?"

55 Kisingi ichoicho Yesu akadigombeka ido zumwezumwe da wantu, "Ivi mweza kunigwiiya kwa mapaange na malungu inga miye nibagaa? Kia msi nekhiwa he Nyumba ya Muungu nikahinya, na khamwekunigwiiya!

56 Iya aya yose yagosoka ili Maandiko wekuandikayo waoni yaiganie." Nee wahina wose wakambada na kumguuka.

*Yesu hemeso ya Mkonga*

*Maliko 14:53-65; Luka 22:54-55,63-71; Yohana 18:13-14,19-24*

57 Wada wantu wekumgwiiyao Yesu wakamwegaa he nyumba ya mviki mkuu ekwetangwae Kayafa, wekukintanikaho wahinyi wa miko na wagookezi wa Wayahudi.

58 Petulo akamtongea kwa hae adi kwe ukumbi da mviki mkuu, akengia mwe buha da ida nyumba hamwe na wagoji adahe kukauwa mbui zendavyozilawiiye.

59 Wagookezi wa mkonga na waviki wakuu wakaondeza uvuhuzi wa uhokho wadahe kumkoea masa Yesu ili wamkome.

60 Iya khawekupata uvuhuzi wowose, etiho nee weza wavuhuzi wangi wa uhokho. Kisikiizi wakeza wavuhuzi waidi,
61 wakamba, "Mntu uyu kagombeka, 'Nadaha kuituwa Nyumba ya Muungu na kuizenga kwa misi mitatu.' "

62 Mviki mkuu akagooka na kumuuza Yesu, "Wee khuna chakutambaisa kwa aya wagombekayo wantu awa?"
63 Iya Yesu yee khekuandua dodose. Mviki mkuu akamwamba, "Nakuahiza kwa Muungu wa ugima, tambe ati wee nee Klistu, Mwana wa Muungu!"

64 Yesu akamtambaisa, "Inga wekugombekavyo miye nee uyo. Iya nawamba, kuvokea isasa mwendammuone Mwana wa Mntu kekaa phande ya kuume ya yuda mwenye udaho, akeza uwanga ya mazunde ya uwanga kwa Muungu."

65 Aho mviki mkuu akatatua gwanda dakwe akamba, "Kambea Muungu takunda wavuhuzi wani vituhu? Nywie wenye mtegeeza ekumbeavyo Muungu.
66 Nywie mwaona viivihi?"

Wowo wakamtambaisa, "Akundigwa auye na nyuma!"

67 Ahoaho wakamswiiya ovu mwe cheni na watuhu wakamtoa ngumi na watuhu vibao,
68 wakamwamba, ati wee nee klistu "Otea! Ni ndai mwekukutoa!"

*Petulo amuemea Yesu*
*Maliko 14:66-72; Luka 22:56-62; Yohana 18:15-18,25-27*

69 Kisingi Petulo nekekaa chongoi he buha. Mndima yumwe wa kivyee wa Mviki Mkuu akamwezea na kumwamba, "Wee namba ne uhamwe na Yesu wa Galilaya."

70 Petulo akaemea hemeso ya wose akamba, "Khimanya wagombeka mbwai."
71 Ekuwaho akalawa he uvi, mndima mtuhu wa kivyee ekumwonaho, akawamba wada wekuwao hada, "Mntu uyu nekawa na Yesu wa Nazaleti."

72 Petulo akaemea vituhu kwa kuaha, "Khimmanya mntu uyo."

73 Kisingi kidogo, wantu wekuwao hada wakambasa Petulo na kumwamba, "Ata wee, ni yumwe yao, kwaviya ata viya ugombekavyo kwakumanyisa."

74 Aho Petulo akavoka kweswiiya ute na kweahiza na kugombeka, "Khimmanya mntu uyo!" Ahoaho zogoo akakema,
75 aho Petulo akaikumbuka ida mbui ekwembigwayo ni Yesu, "Zogoo khadizati kukema wenda uniemee maa ntatu." Aho akalawa chongoi na akavoka kuiya kwa usungu.

# 27

*Yesu egalwa kwa Pilato*
*Maliko 15:1; Luka 23:1-2; Yohana 18:28-32*

1 Kwekuchaho wagookezi wa Waviki wose na waongoezi wa Wayahudi wakakintana vituhu ili wagosoe nteganyi wadahe kumkoma Yesu.
2 Wakamzengeteza phingu na kumwegaa kwa Pilato, mwekuwa mgookezi wa Kilumi.

*Kuuya na nyuma kwa Yuda Isikaliote*
*Ntendwa 1:18-19*

3 Yuda Isikaliote mwekumhituka Yesu, ekuonaho Yesu kabindakae kuamuiwa, akamema usungu na akawavuzia wagookezi wa waviki wakuu zia ntii za makumi matatu ya madini ya feza.
4 Akawamba, "Khikoa masa kwa kumlavya mntu mwesekuwa na masa yoyose akomwe."
Iya wowo wakamtambaisa, "Yatiambiiza mbwai swie? Ivyo umanye wee mwenye!"
5 Nee atambika zia ntii za madini ya feza he nyumba ya Muungu na kulawa chongoi na kuita kwetungika.
6 Waviki wakuu wakadoa zia ntii za madini za feza wakamba, "Khaifaa kuika hamwe madini aya ya feza na madini yalavigwayo mwe Nyumba ya Muungu kwaviya ntii izi za madini ya feza zilavigwa kwaajii ya kumkoma mntu."
7 Wekubindaho kumamakhanya wakevana kugua mnda wa kiongo hawe hantu hauzisi ha wanyika.
8 Nee mana adi ivyeo mnda uwo wetangwa mnda wa phome.
9 Nee yaigania ida mbui yekwegombekwayo na Muoni Yelemia, kuwa, "Wakadoa ziya ntii za makumi matatu ya madini ya feza, yombe yekupangwayo na wantu wa Isilaeli,
10 wakaziguiya mnda wa kiongo, inga Zumbe ekuniagiiavyo."

*Yesu hemeso ya Pilato*
*Maliko 15:2-5; Luka 23:3-5; Yohana 18:33-38*

11 Yesu ekuwaho kagooka hemeso ya Pilato ekuwaye mgookezi wa Kilumi, akamuuza, "Wee nee Seuta wa Wayahudi?" Yesu akagombeka, "Inga wekugombekavyo miye nee uyo."
12 Iya wagookezi wa waviki na wadaa wekumwahiavyo masa khekutambaisa mbui.
13 Ivyo Pilato akamuuza, "Ivi khutegeeza mbui ambazo wazigombeka?"
14 Iya Yesu khekuandua ata mbui mwenga, ata uyo mgookezi wa Kilumi akahondomaa muno.

### *Yesu aamuiwa kukomwa*

*Maliko 15:6-15; Luka 23:13-25; Yohana 18:39; 19:16*

15 Neiwa kawaida kisingi cha sikukhuu ya Pasaka mgookezi wa Kilumi awavugwiiya zumwezumwe da wantu mfungwa yumwe wamkundae.

16 Kisingi icho nekuwa na mfungwa yumwe ekuwaye mntu mfyaimi, zina dakwe Balaba.

17 Ivyo wantu wekukintanikaho hamwe, Pilato akawauza, “Mwakunda ni wavugwiiye yuhi gatigati ya awa waidi, Balaba hambu Yesu etangwae Klistu?”

18 Kagombeka ivyo, kwaviya kamanya wamueta kwakwe kwaajii ya kinyuu.

19 Pilato ekuwaho kekaa mwe kigoda chakwe cha kuamuiya, mkaziwe akamwetea bauwa inu. “Usekumgosoa kintu chochose mntu uyu yedi, na kwaviya ivyeo khisuumizwa muno mwe sozi kwaajii yakwe.”

20 Iya waviki wakuu na wadaa wakawanchochea dia zumwezumwe da wantu wamwombeze Balaba aekewe na Yesu akomwe.

21 Pilato akawauza, “Gatigati ya awa waidi ni yuhi mumkundae niwavugwiiye?” Wakatambaisa, “Balaba!”

22 Pilato akawauza, “Isasa mwaonda nimtende viivihi na Yesu mwetangwae Klistu?”

Wose wakagombeka, “Agong'ondewe he mhamba!”

23 Pilato akawauza, “Kwa mbwai? Ni ufyaimi wani ekugosoao?”

Wowo wakaendeea kutoa mgutio, “Agong'ondewe he mhamba!”

24 Pilato ekuonaho kuwa khadaha kugosoa dodose na kwaviya khumbizi zavoka kulawiiya, akadoa mazi na akasunta mikono hemeso ya dia zumwezumwe da wantu, akamba, “Mie khimo mwe mbui ya kumkoma mntu uyu, mbwii yenu wenye.”

25 Wantu wose wakamba, “Kwa mbui inu tiigosoayo, Muungu na atekhe sugusa swie hamwe na wana wetu!”

26 Aho Pilato akawavuguiya Balaba kulawa he kifungo, na akagombeka Yesu atoigwe na ngoda yekwegosolwayo na babu da kiboko, na akamlavya agong'ondewe he mhamba.

### *Asikai wamhega Yesu*

*Maliko 15:16-20; Yohana 19:1-3*

27 Wakamwegaa gati mwe nyumba ya ugookezi, na maasikai wose wakamzunguka.

28 Wakamhambua gwanda dakwe, wakamhasika joho dekhundu.

29 Wakagosoa kintu inga khofia seuta yekugosolwayo na miwa wakamhasika mwe mtwi, wakamwiikia ngoda mwe mkono wakwe kuume. Wakakinta mavindi hemeso yakwe, wakambea kwa kumwamba, “Takuugusa Seuta wa Wayahudi!”

30 Wakamswiiya ovu, wakadoa ida ngoda wekumwekhayo mwe mkono wakwe na kumtoa nayo mwe mtwi

31 Wekubindaho kumgosoeya ayo, wakamhambua dia gwanda na kumhasika nguo zakwe, na wakamwegaa kumgong'ondea mwe mhamba.

### *Yesu agong'ondewa he mhamba*

*Maliko 15:21-32; Luka 23:26-43; Yohana 19:17-27*

32 Wekuwaho wakaita kumng'ondea he mhamba wakamuona mntu yumwe zina dakwe Simoni, mwenyezi wa Kilene. Aho asikai wa Wakilumi wakamshuutiza kuudoa mhamba wakwe Yesu.

33 Wekubuaho hantu hetangwaho Goligota mana yakwe, hantu hafufu da mtwi,

34 wakamwekha divai yekuhanganywayo na nyongo. Iya Yesu ekuionjaho akaemea kuidomea.

35 Wakamgong'ondea he mhamba, naho nguo zakwe wakapangana kwa kuzitoea kula

36 Wakekaa, wakawa wamuinda.

37 Uwanga ya mtwi wakwe kwe mhamba nee kuikwa kibao chekuandikwacho, “Uyu ni Yesu, Zumbe wa Wayahudi.”

38 Viyaviya mabagaa waidi nee wagong'ondewa kia yumwe na mhamba wakwe, yumwe phande ya kuume na mtuhu phande ya kumoso.

39 Wantu wekuwao wakemboka hehi na aho wakamdumua na kusingisa mitwi yao kwa kumseka na kugombeka,

40 “Wee kwevuna, wadaha kuitua Nyumba ya Muungu na kuizenga kwa misi mitatu! Inga wee ni Mwana wa Muungu, eohoe mwenye na usee mwenye kulawa aho he mhamba!”

41 Viyaviya, wagookezi wa waviki na wahinyi wa miko na waongoezi wa Wayahudi wakamhega na kugombeka.

42 “Kawaohoa watuhu, akini kweohoa mwenye khadaha! Ati yee ni Seuta wa wantu wa Isilaeli! Na asee mwe mhamba, na swie tenda timzumiiye!

43 Kamkauwiya Muungu, na isasa Muungu amwoohoe inga amkunda, kwaviya kagombeka, ‘Mie ni Mwana wa Muungu.’ ”

44 Ata wada wahokaji wekugong'ondewao hamwe nae wakamdumua viyaviya.

### *Yesu auya na nyuma*

*Maliko 15:33-41; Luka 23:44-49; Yohana 19:28-30*

45 Kuvokea saa mtandatu, musi adi saa
kenda, si yose nenikiza du.
46 Yekubuaho saa kenda Yesu akaiya kwa
mgutio mkuu, “Eloi, Eloi, Lama sabaki-
tani?” Yaani, “Muungu yangu, Muungu
yangu, mbona kunibada?”
47 Iya wantu wada wekugookao hada
wekutegeezaho ivyo wakagombeka,
“Amwetanga Elia.”
48 Yumwe awo akaguuka na akadoa
dodoki akadiginta mwe divai yekusasayo,
akaiika uwanga ya lasi, na akamwekha
adomee.
49 Watuhu wakagombeka, “Eka tikauwe
ati Elia endaeze kumwoohoa.”
50 Naho Yesu akaiya vituhu kwa mgutio
mkuu na akauya na nyuma.
51 Ahoaho pazia da Nyumba ya Muungu
dikatatuka ntii mbii, kulawa uwanga hadi
asi, na inusi ikazingiza na maiwe makuu
yakabondekabondeka,
52 mambiya yakavuguka na wantu wa
Muungu wakayuyuswa.
53 Bada ya kuyuyuka kwakwe Yesu,
wakalawa mwe mambiya na wakengia mzi
wa Muungu na wantu wangi wakawaona.
54 Yuda mkuu wa maasikai hamwe
na weziwe wekuwao wakamuinda Yesu
wekuonaho zingizo da inusi na zia
mbui zekulawiiazo wakaogoha muno na
wakagombeka kwei, “Mntu uyu neekawa
Mwana wa Muungu.”
55 Hantu aho newaaho wavyee wangi
wakamkauwa kwa hae. Awo nee wada
wekumtongeao Yesu kulawa Galilaya
wakamwambiiza.
56 Gatigati yao nee ni Maliamu mntu wa
Magidala na Maliamu mami yao da Yakobo
na Yusufu, hamwe na mami yao wana wa
Zebedayo.

*Uzisi wa Yesu*

*Maliko 15:42-47; Luka 23:50-56; Yohana 19:38-42*

57 Yekubuaho guoni, akeza mntu yumwe
mwenye vintu vingi zina dakwe Yusufu
mwenyezi wa mzi wa Alimataya. Yee naye
nekawa mhina wa Yesu,
58 akambasa Pilato akauombeza mwii wa
Yesu. Aho Pilato akamba ekhigwe.
59 Yusufu akaudoa uda mwii
akauzengeteza sanda yekung'aayo muno,
60 akauiika mwe mbia dihya ekudis-
ongoado mwe iwe kuu, akadoa iwe kuu na
kudiika he uvi, na akahauka zakwe.
61 Maliamu mntu wa Magidala na
Maliamu yuda mtuhu, newekaa kukauwa
mbia da Yesu.

*Mbiya daindwa*

62 Kioi yakwe, yaani Msi wa Kuhumwi-
iza, Waviki wakuu na Mafalisayo wakam-
basa Pilato,
63 wakamwamba, “Mkuu tikumbuka
kuwa, ‘Yuda mtiizi katigombeka, kisingi
khazati kuuya na nyuma, bada misi mitatu
nendaniyuyuke.’
64 Kwaiyo agiiya ido mbiya diindwe adi
misi mitatu ili wahina wakwe wasekweza
kumbawa, na kuwamba wantu kayuyuka.
Uhokho hunu wa kisikiizi wendauwe wa
ufyaimi muno kusima uda wa bosi.”
65 Pilato akawamba. “Haya, mnao wain-
daji na waite mkadiinde mmanyavyo.”
66 Ivyo wakaita na wagoji ili kudiinda dia
mbia vitana, na wakaika alama mwe dia
mbia na aho waika asikali wainde.

# 28

*Kuyuyuka kwa Yesu*

*Maliko 16:1-10; Luka 24:1-12; Yohana 20:1-10*

1 Wekwembokaho Msi wa Kuhumwi-
iza na yekubuwaho keo muno msi wa
Jumapili. Maliamu mntu wa Magidala na
yuda Maliamu mtuhu wakaita kudikauwa
dia mbia.
2 Vuu puu, kukalawiiya zingizo kuu da
inusi mndima wa Zumbe akaseeya kulawa
uwanga kwa Muungu akaditongoosa dia
iwe na akadekaiya.
3 Akoonekana inga umweko na nguo za-
kwe nezing'aa chwee.
4 Wagoji wa dia mbiya wakakama kwa
ukeng'enta mkuu wakawa inga wekuuyao
na nyuma.
5 Iya yuda mndima wa uwanga kwa
Muungu akawamba wada wavyee,
“Nyie mwesekuogoha! Namanya mwa
mwondeza Yesu mwekugong'ondewa he
mhamba.
6 Hanu khayuho kwaviya kayuyuka inga
ekugombekavyo. Sooni mhakauwe hantu
hekuwaho mwii wakwe ugonezwa.
7 Naho hitani kinyionyio mkawambe
wahina wakwe kuwa kayuyuka na isasa
awaongoeya kuita Galilaya, uko mwenda-
mumwone. Aya miye khigombeka kae.”
8 Awo wavyee wakahauka hada he
mbiya uku wamema ukeng'enta na nyemi
muno, wakaita uku waguuka wakawambe
wahina wakwe mbui iyo.
9 Vuu puu, Yesu akakintana nawo ak-
agombeka, “Mwaona vihi.” Awo wavyee
wakamtimia na kukinta mavindi hemeso
yakwe wakatoza miundi yakwe wakavika.
10 Nee Yesu awamba, “Mwesekuogoha!
Hitani mkawambe wandugu zangu waite
Galilaya na uko wenda wanione.”

*Wagoji waita kugombeka yada wekuyaonayo*

11 Kisingi wada wavyee wekuwaho
wakaita zao siai, wamwe na wamwe wa
asikai wekuwao wainda mbiya wakaita

mwe mzi na kuwatamwiiziya wagookezi wa waviki kia kintu chekulawiiacho.
12 Awo wagookezi wa waviki kukintana hamwe na waongoezi wa Wayahudi na kugosoa nteganyi yao, na wakawekha wada asikai hea nyingi muno,
13 wakawamba, “Nywie mwenda mgombeke ivi, ‘Wahina wakwe nee weza na kio, wakaudoa mwii wakwe kisingi swie nee tigona.’
14 Inga mbui izi zikambwiiya mgookezi Pilato swie tendatigombeke nae na nywie khamnampate tatizo dodose.”
15 Wada wagoji wakazidoa zia hea inga wekuhinywavyo. Mbui iyo ikaambazika gatigati ya Wayahudi hadi ivyeo.

*Yesu awalawiiya wahina wakwe*

*Maliko 16:14-18; Luka 24:36-49; Yohana 20:19-23; Ntendwa 1:6-8*

16 Wada wahina kumi dimwe na mwenga wakaita Galilaya kwe uda muima inga ekuwaagiiavyo Yesu.
17 Akini watuhu newawa khawazumiiya kuwa kwei nee ni Yesu.
18 Yesu akeza hehi na kuwamba, “Nchekhigwa udaho wose wa uko uwanga kwa Muungu na mwe inusi.
19 Hitani mkawagosoe wantu wa si zose wawe wahina wangu, mkawabatiiza kwa zina da Tate na da Mwana na Muye wa Muungu.
20 Wahinyeni kutoza miagiiyo yangu nikuwekhayo. Na miye ni hamwe na nywie misi yose, adi kisingi cha kisikiizi.”

# Mbui Yedi inga yekuandikwavyo ni Maliko Uwongoezi

Mbui Yedi kulawana na Maliko ni mwenga aho ya vitabu vine mwe agane dihya, vigombekavyo ugima wa Yesu Klistu. Kiya yumwe aho etangwa mbui ntana ionyeshayo Mbui Zedi na zekuandikwazo bada ya ufe wa Yesu na Matayo, Maiko, Luka na Yohana.

Mbui Yedi kulawana na Maliko ni njihi muno kusima zose nne. Yagombekwa kuwa iyandikwa bada ya kuvyaigwa Yesu, wekusomao wangi wamba iyandikwa uko Lumi kwa kusudi da kukunda waklistu wa Kilumi uko. Maliko amanyika inga Yohana Maliko nekawa hamwe na muagiiwa Paolo na Balinaba, akini ntunyo yakwe iumizwa kisingi kabada ntambo yao ya kuambaza Mbui ya Muungu Ntendwa 13:13 badae Maliko akamanyika inga mmbuya wahehi wa Petulo 1 Petulo 5:13. Inga Maliko khekumwona Yesu akini wekusomao wazumiiya na nee wamba Maliko kaandika mbui nyingi mno za Petulo na ido ne vokeo da Mbui Yedi, kuigana na Maliko mwe Mbui ya Maliko amanya uhina wakwe kwa Yesu kisingi cha kisikizi.

**Yeumondani**

- Maliko ivokea mwe kitabu cha Maliko 1:1-13.
- Naho Maliko atiambiza mbui za Yesu kisingi ekuwaho Galilaya, Maliko 1:14 - 8:21.
- Naho ahadisia uwanga ya ntambo ya Yesu kuita Yelusalemu mwe Maliko 8:22 - 10:52.
- Maliko abindiza kwa kuandika kisingi Yesu uko Yelusalemu hamwe na ufe wakwe na kuyuyuka, Maliko 11:1 - 16:8.

*Yohana Mbatiiza abiikia wantu*
*Matayo 3:1-12; Luka 3:1-18; Yohana 1:19-28*

1 Inu ni Mbui Yedi ya Yesu Klistu, Mwana wa Muungu.
2 Ivoka inga yekuandikwavyo he kitabu cha muoni wa Muungu etangwaye Isaya,
"Muungu akagombeka, 'Namuagiiya mndima yangu
Akuongwee, endaye akugoswee sia yako.'
3 Mgutio wa mntu wetanga mwenyika
'Mgosoeyani Zumbe sia yakwe Nyooshani myemboko yakwe.' "
4 Yohana mbatiiza kalawiiya mwe nyika, akawabiikia wantu na kuwabatiiza na kuwamba, "Waeke mavigaviga na Muungu endaawaekee mavigaviga yao."
5 Wantu wose kulawa si ya Uyahudi na wada wa mzi wa Yelusalemu, wakambasa kumtegeeza Yohana na kubada mavigaviga yao, nee wabatizwa mwe zigizigi da mazi Yolodani.
6 Yohana kavaa gwanda dekugosolwado na mazoya ya mnyama mwetangwa ngamia, na mshipi wa babu mwe kigudi chakwe, naho khande yakwe ne nsige na woki.
7 Akawamba wantu, "Eza mntu kwe mgongo wangu mwenye udaho kusima miye. Naho miye khikundigwa ata kwenama na kuchopoa sigi za sabana zakwe.
8 Miye nabatiiza kwa mazi, akini yee endaawabatiize kwa Muye wa Muungu."

*Kubatiizwa na kugeezwa kwa Yesu*
*Matayo 3:13; 4:11; Luka 3:21-22; 4:1-13*

9 Misi ida Yesu akatimia kulawa Nazaleti mzi wa Galilaya, akabatizwa ni Yohana mwe zigizigi da mazi Yolodani.
10 Ahoaho ekulawaho mwe mazi, Yesu akaona uwanga kwa Muungu kuvuguka na Muye wa Muungu ukaseeya inga suwa uwanga yakwe.
11 Mgutio ukategeezeka kulawa uwanga kwa Muungu, "Uyu ne mwanangu nimkundaye, nitamiwaye naye."
12 Ahoaho Muye wa Muungu ukamuongoeeya kuita he kiwawe.
13 Akekaa uko kwa misi makumi mane, akageezwa ni Ibiisi. Kekaa uko hamwe na wanyama wa mzituni, naho wandima wa uwanga wa Muungu wamuambiza.

*Yesu awetanga walowa wane*
*Matayo 4:12-22; Luka 4:14-15; 5:1-11*

14 Yohana ekuikwaho mwe kifungo, Yesu akaita mwe si ya Galilaya, akabiikia Mbui Yedi ya Muungu.
15 Akagombeka, "Kisingi kibua, Useuta wa Muungu uhehi! Hitukani mzumiiye Mbui Yedi!"
16 Naho Yesu ekuwaho akemboka khandakhanda ya tondoo da mazi ya Galilaya, nee awaona wavuvi waidi, Simoni na nduguye Anduleya, walowa
samaki. 17 Yesu akawamba, "Nitongeani miye, nendaniwatende muwaete wantu kwangu inga walowa waetavyo samaki."
18 Aho wakazibada nyavu zao wakamtongea.
19 Ekuitaho mbee kidodo nee awaona Yakobo na nduguye Yohana wana wa Zebedayo. Wowo pia newawa mwe ngaawa yao, naho ne wakagosoa nyavu zao.
20 Ahoaho Yesu akawetanga, wakambada tati yao Zebedayo mwe ngaawa hamwe na wandima wakwe na kumtongea Yesu.

*Yesu amhonya mntu mwenye mazaiko*
*Luka 4:31-37*

21 Yesu na wahina wakwe nee waita
mzi wa Kapelinaumu. Msi wekwezao wa
Kuhumwiiza, Yesu akengia mwe Nyumba
ya kukintania Wayahudi, nee avoka
kuhinya wantu.
22 Wantu wose wekumtegeezaho nee wa-
hondomaa kwa mahinyo yakwe, kwaviya
khekuwa akahinya inga wahinyi wa miko,
iya inga mntu mwenye udaho.
23 Mwe Nyumba ya kukintania
Wayahudi akaawiiya mntu yumwe
mwekuwa na mazaiko, nee agutia,
24 "Una mbwai na swie, Yesu wa Nazaleti?
Kweza kutidagamiza? Namanya wee u
ndai? Wee ni Mntu Mtana wa Muungu!"
25 Yesu akadiwakia ido zaiko, "Nyamaa
muawe mntu uyu!"
26 Dia zaiko dikamgea ugwa mtwi, akaiya
kwa mgutio mkuu akamlawa.
27 Wantu wose wakahondomaa
wakauzana, "Inu ivivihi? Uwo ni mahinyo
mahya? Kwaviya kwa udaho mntu uyu
alavya mazaiko, naho yamtegeeza!"
28 Nee mbui za Yesu zikaambazwa mwe
si yose ya Galilaya.

*Yesu awahonya wantu wangi*
*Matayo 8:14-17; Luka 4:38-41*

29 Wakalawa he Nyumba ya kukintania
Wayahudi, wakaita mwenga kwa mwenga
kaya kwa Simoni na Anduleya na Yakobo
na Yohana wakaita hamwe nawo.
30 Naho mkwewe da Simoni ya kivyee
nee yumwe usazi ni mtamu ana bombom
kai, Yesu ekubuaho wakamwamba mbui
zakwe.
31 Yesu akamtimia hehi yakwe, akamtoza
mkono uyo mvyee, akamwenua na ahoaho
homa ikamwekea. Akavoka kuwagosoeya
ndima.
32 Guoni zua dekuswaho, wakamwe-
gaiya Yesu watamu wose na wekukwewao
mazaiko.
33 Wantu wose wa mzi uda wakakintana
chongoi ya uvi.
34 Yesu akawahonya wantu wangi
wekuwao na tamu mbaimbai na akaguusa
mazaiko mangi. Naho khekuwaekea
watamwiiye kintu chochose kwaviya
wammanya yee ni ndai.

*Yesu abiikia mwe mzi wa Galilaya*
*Luka 4:42-44*

35 Keokeo da mtungaihu, Yesu akalawa
akaita hantu kwesaho wantu kuvika.
36 Simoni na weziwe wakaita kumoon-
deza,
37 wekumwonaho wakamwamba, "Kiya
mntu akoondeza."
38 Yesu akawatambaisa, "Titeni he mizi
mituhu yahehi nikabiikie uko, miye ncheza
kwaajii iyo."
39 Naho akaita si yose ya Galilaya,
akabiikia mwe Nyumba ya kukintania
Wayahudi na kuwaakia mazaiko.

*Yesu amhonya mntu mwenye utamu wa nyoka*
*Matayo 8:1-4; Luka 5:12-16*

40 Mntu yumwe mwekuwa na utamu
wa nyoka akambasa Yesu, akamheembeza
na kumkintia mavindi na kumwamba,
"Ukakunda, wadaha kuning'aza."
41 Yesu akamwonea mbazi, akenua
mkono wakwe na kumdonta. Nee
amwamba, "Nakunda, ng'azika!
42 Ahoaho utamu wa nyoka ukamuekea
yuda mntu, akang'azika."
43 Naho Yesu akamwamba aite
kinyionyio na kumwamba,
44 "Tegeeza, usekumwamba mntu yoyose
mbui inu. Akini hita ukeonyeshe kwa
mviki, na kwaajii ya kung'aa kwako
ukalavye mviko inga ekugombekavyo
Musa koonyesha kuhona."
45 Akini yuda mntu akaita na akavoka
kuambaza mbui izo kiya hantu, hata Yesu
khekudaha kwengia mwe mzi wowose
kwa kweonyesha. Nee ekaa chongoi kwe-
saho wantu, nee ivyo wantu wakambasa
kulawa kiya phande.

# 2

*Yesu amhonya mntu mwekuohoa*
*Matayo 9:1-8; Luka 5:17-26*

1 Yekwembokaho misi micheche, Yesu
akauya mwe mzi wa Kapelinaumu wantu
wakategeeza yukaya.
2 Aho wakeza wantu wangi na kumema
hewazo adi kwe uvi. Yesu nee awabiikia
mbui zakwe,
3 kisingi ichoicho wantu wane nee
wabua wakamwenua mntu yumwe
mwekuhooa, wakamwegaa kwa Yesu.
4 Kwaajii ya zumwezumwe da wantu
dekumemado, khawekudaha kubua
hehi na Yesu. Ivyo wakabovoa hantu
ha chusi yekuwayo uwanga ya hantu
ekuwaho Yesu, nee waseeza javi da yuda
mwekuhooa.
5 Yesu ekuonaho kuzumiiya kwao,
akamwamba yuda mwekuhooa,
"Mwanangu, kuekewa mavigaviga yako."
6 Wahinyi watuhu wa miko newawa
mwe nyumba ida wekaa, wakama-
makhanya mwe mioyo yao,
7 "Haikuka mbwahi ata agombeka ivi?
Kamdumua Muungu! Khahana mdaha
kuekea mntu mavigaviga iya Muungu
ikedu!"

8 Yesu akamanya wamamakhanyavyo mwe mioyo yao nee awauza, “Kwa mbwai mwamamakhanya ivyo mwe mioyo yenu?

9 Vyedi ni vihi, kumwamba mntu mwekuhooa, ‘Kuekewa mavigaviga yako’, hambu kugombeka, ‘Enuka wetwike javi dako wende?’

10 Akini mmanye Mwana wa Mntu ana udaho wa kuekea wantu mavigaviga yao mwe inusi.” Nee Yesu amwamba yuda mntu mwekuhooa,

11 “Nakwamba, gooka, wetwike javi dako uite kaya!”

12 Ahoaho wantu wose nee wamkauwa yuda mntu akenuka, na kudoa kilago chakwe, akahauka. Wantu wose nee wahondomaa na kumtogoa Muungu wakamba, “Khatizati kuona katu mbui inga inu!”

*Yesu amwetanga Lawi*
*Matayo 9:9-13; Luka 5:27-32*

13 Yesu akaita vituhu khandakhanda ya tondoo da mazi ya Galilaya. Zumwezumwe da wantu dikambasa, nee avoka kuwahinya.

14 Ekuwaho akemboka, nee amwona Lawi mwana wa Alifayo, kekaa mwe kazumba ka kuihia kodi. Yesu akamwamba, “Nitongea.” Lawi akagooka akamtongea.

15 Kisingi kwemboka Yesu nee kekaa mwe nyumba ya Lawi, akada khande. Watoza ushuu na wada wagosoao mavigaviga nee wakambasa Yesu, na wangi wao wawa wekaa hamwe na wahina wakwe.

16 Wamwe wa wahinyi wa miko, wekuwao Mafalisayo, wekumuonaho Yesu ada hamwe na wagosoa mavigaviga na watoza ushuu, nee wawauza wahina wakwe, “Kwambwai ada na watoza ushuu na wagosoa mavigaviga?”

17 Yesu ekuwategeezaho, nee agombeka, “Wantu wesao kuhuma khawakunda mganga akini wamkundao ni wada wahumao. Nchekweza kuwetanga wedi, iya wenye mavigaviga.”

*Mbui ya kwehiniza kuda*
*Matayo 9:14-17; Luka 5:33-39*

18 Kisingi kimwe wahina wa Yohana mbatiiza hamwe na wahina wa Mafalisayo nee wehiniza kuda. Naho wantu wakeza wakamuuza Yesu, “Kwambwai wahina wa Yohana na wa Mafalisayo wehiniza kuda, akini wahina wako khawehiniza kuda?”

19 Yesu akatambaisa, “Wantu wekugonekwao kwe wiya wadaha viivihi kwehiniza kuda ikawa zumbe wa wiya yu hamwe nao? Khawadaha kwehiniza kuda wakawa hamwe na zumbe wa wiya.

20 Akini kisingi chendakibue zumbe wa wiya endaho ausigwe gatigati yao, aho wendawehinize kuda.

21 “Khahana mntu msenga kilaka kihya na kukibwikabwika mwe nguo yekusakaayo, inga akatenda ivyo iko kilaka kihya chendakitatue nguo yekusakaayo, naho yendaibanike muno.

22 Naho khahana wantu wageayo divai mhya mwe mikwiji ya babu yekusakaayo, inga wakagosoa ivyo divai yendaitatue mikwiji ya babu, na divai hamwe na mikwiji ya babu yendaibanike. Divai mhya yagewa mwe mikwiji mihya.”

*Yesu ahinya mbui ya Msi wa Kuhumwiiza*
*Matayo 12:1-8; Luka 6:1-5*

23 Msi umwe wa Kuhumwiiza, Yesu na wahina wakwe wekuwaho wemboka mwe minda ya uhemba, wekuwaho wakenda wahina wakwe wakavoka kusenga uhemba.

24 Mafalisayo wakamuuza Yesu, “Kauwa, ni viivihi wagosoa mbui ziemewazo kugosoa Msi wa Kuhumwiiza?”

25 Yesu nee awatambaisa, “Khamzati kusoma ekugosoavyo Daudi hamwe na weziwe kisingi wekuwaho na saa?

26 Yee akengia mwe Nyumba ya Muungu akada yada mabumunda yekuikwayo hemeso ya Muungu. Mbui inu igosoka kisingi cha Abiazali, nekawa Mviki Mkuu. Na ni waviki wowodu wakukundigwao wade mabumunda ayo, akini Daudi kada na kuwekha na weziwe.”

27 Naho Yesu akawamba, “Msi wa Kuhumwiiza uikwa kwaajii ya wantu na khio wantu kwaajii ya Msi wa Kuhumwiiza.

28 Ivyo Mwana wa Mntu ana udaho ata wa Msi wa Kuhumwiiza.”

# 3

*Yesu amhonya mntu mwenye mkono wekuhooao*
*Matayo 12:9-14; Luka 6:6-11*

1 Naho Yesu akengia vituhu mwe Nyumba ya kuvikia Wayahudi, nemuwa na mntu mwekuhooa mkono.

2 Umo wantu watuhu wakamgoja amhonye mntu uyo Msi wa Kuhumwiiza ili wadahe kumuahiya masa.

3 Yesu akamwamba uyo mntu mwekuhooa mkono, “Soo aha gooka hemeso ya kia yumwe.”

4 Naho akawauza, “Kulawana na miko yetu takundigwa kugosoa mbwai Msi wa Kuhumwiiza? Kuohoa ugima au kukoma?” Akini wowo khawekuandua dodose!

5 Aho Yesu akawafuiya meso kwa maya, akaugumia, kwaajii ya mioyo yao itogayo.

Naho amwamba yuda mntu, “Enua mkono wako!” Naye akenua mkono wakwe, ukatenda mgima vituhu.

6 Ahoaho Mafalisayo wakalawa chongoi, wakakintana hamwe na kizumwezumwe cha Helode wakaondeza sia ihi wendayo wamkome Yesu.

*Zumwezumwe da wantu khandakhanda ya tondoo da mazi.*

7 Yesu hamwe na wahina wakwe, wakahauka na kuita khandakhanda ya tondoo da mazi. Na zumwezumwe da wantu kulawa si ya Galilaya dikambasa,

8 wekusikiaho mbui zose ekugosoazo, zumwezumwe da wantu dikamwezea kulawa Uyahudi na Yelusalemu na Idumea na si zose zekuwazo awio da zua da zigizigi da mazi Yolodani hamwe na wada wa hehi wa si ya Tilo na Sidoni.

9 Yesu akawamba wahina wakwe wamuikie ngaawa kwaviya wantu wasekumfintafinta.

10 Kwaviya ne kawahonya watamu wangi, na watamu wose ne wamfintafinta wadahe kumdonta.

11 Na kia mwenye zaiko ekumuonaho Yesu, aketambika ahosi hemeso yakwe na kugombeka, “Wee ni Mwana wa Muungu.”

12 Akini Yesu akayaemeza kwa ukai yada mazaiko yasekuwamba wantu kuwa yee ni ndai.

*Yesu asagua waagiiwa kumi dimwe na waidi*

*Matayo 10:1-4; Luka 6:12-16*

13 Yesu ne akwea kwe kiima akawetanga wada ekuwakundao ne wambasa.

14 Naho ne awasagua wantu kumi dimwe na waidi na akawetanga waagiiwa, wekae naye awaagiiye kubiikia wantu,

15 na wawe na udaho wa kulavya mazaiko.

16 Aho kumi dimwe na waidi wekusagulwao ni awa, Simoni mwekwekhigwa zina da Petulo,

17 Yakobo na kakie Yohana wana wa Zebedayo, Yesu akawekha zina Boanege mana yakwe, “Wantu wa tuntumo.”

18 Andulea na Filipo na Batolomayo na Matayo na Tomasi na Yakobo mwana wa Alifayo na Tadayo na Simoni mtoanaji wa si yakwe.

19 Yuda Isikaliyote mwekumhituka Yesu.

*Yesu na Belizebuli*

*Matayo 12:22-32; Luka 11:14-23; 12:10*

20 Naho Yesu akauya kaya na zumwezumwe da wantu dikakintana vituhu, ata Yesu na wahina wakwe khawekupata phasi ya kuda khande.

21 Nduguze wekusikiaho mbui iyo wakenda kumdoa kwaajii wantu ne wamba, “Ana kiau.”

22 Wamwe wa Wahinyi wa Miko kulawa Yelusalemu wakamba, Kakwewa Belizebuli! Mkuu wa mazaiko awalavya wantu mazaiko kwa udaho wa mkuu wa mazaiko.

23 Yesu akawetanga, akagombeka nao kwa simo, “Ibiisi adaha viivihi kumguusa Ibiisi mweziwe?”

24 Inga wantu wa useuta umwe wakatoana khondo wenye kwa wenye, useuta wendaugwe.

25 Wantu wa kaya mwenga wakesekwevana kaya iyo yendaidagamie.

26 Kwaivyo useuta wa Ibiisi ukepanga vizumwezumwe khaudaha kwekaisa iya wendaudagamie.

27 “Khahana mntu adahae kwengia mwe nyumba ya mntu mwenye mdundugo na kuvidoa vintu vyakwe, avoke kutoana na kumzengeteza yuda mntu mwenye mdundugo nae akamvota endaadahe kuvidoa vintu vyakwe.”

28 “Kwei nawamba, wantu wadaha kuekewa mavigaviga yao hamwe na kumbea Muungu.”

29 Akini mntu agombekaye yesayokutama kwa Muye wa Muungu khana aekewe katu, endaawe na mavigaviga ya kae na kae.

30 Yesu kagombeka ivyo kwaajii wantu watuhu ne wamba, “Ana mazaiko.”

*Mami yakwe da Yesu na wanduguze*

*Matayo 12:46-50; Luka 8:19-21*

31 Mami yakwe da Yesu na wanduguze wakabua aho, wakagooka chongoi wakamwagiiya mntu kumwetanga Yesu.

32 Zumwezumwe da wantu diwa dekaa aho wekaa bunga. Naho wantu wakamwamba, “Kauwa mami yako na wanduguzo wauko chongoi, wakwetanga.”

33 Yesu akawatambaisa, “Mmaa na wandugu zangu ni wakina ndai?”

34 Aho akawakauwa wada wantu wekuwao wekaa bunga akamba, “Awa ne mmaa yangu na wandugu zangu!

35 Mntu yoyose agosoaye akundavyo Muungu, uyo ne kaka yangu na umbu dangu na mmaa yangu.”

# 4

*Msimo wa mntu mhanda mbeyu*

*Matayo 13:1-9; Luka 8:4-8*

1 Yesu ne avoka vituhu kuhinya khandakhanda ya tondoo da mazi ya Galilaya. Zumwezumwe da wantu wangi dikaika bunga naho akengia mwe ngaawa na kwekaa, wantu wose wekaa mwe sanga khandakhanda ya tondoo da mazi.

[2] Akawahinya mbui nyingi kwa simo, na mwe mahinyo yakwe akawamba.
[3] "Tegeezani! Mntu mhanda mbeyu kenda kwetia mbeyu."
[4] Ekuaho aketia mbeyu ntuhu zigwa khandakhanda ya sia ne wadege weza wakazida.
[5] Ntuhu zikagwa mwe iwe kwesiho na sanga, zikahota aho, kwaviya sanga nee ncheche.
[6] Zua dekulawaho mbeyu ziya zikanyaa, kwaviya mazindo yakwe khayokuwa na udaho.
[7] Mbeyu ntuhu nezagwa mwe miwa, ida miwa neyakua na kuzifintafinta ziya mbeyu naho khazokuvyaa.
[8] Na mbeyu ntuhu zikagwa mwe sanga ntana, ne zakua na kuvyaa vitana, mwenga makumi matatu na mwenga makumi mtandatu, na mwenga makumi kumi.
[9] Yesu akagombeka, "Mwenye magutwi na ategeeze."

*Yesu agombeka mana ya simo*
*Matayo 13:10-17; Luka 8:9-10*

[10] Yesu ekuwaho ikedu wamwe wa wada wekumtegeezao hamwe na wahina wakwe kumi dimwe na waidi ne wambasa na kumuuza kia ekutamwiacho kwa simo.
[11] Yesu akawatambaisa, "Nywie mwekhigwa kumanya sii zose za Useuta wa Muungu, akini kwa wada weuko chongoi wenda wembigwe kia kintu kwa simo,
[12] ili,

'Wakaue kwei, akini wasekuona
Wategeeze kwei, akini wasekumanya.
Ama khivyo ne wamhitukia Muungu, wakaekewa.' "

*Yesu asosoa msimo wa mhanda mbeyu*
*Matayo 13:18-23; Luka 8:11-15*

[13] Naho Yesu akawauza, "Nyie khammanya msimo unu? Mwadaha viivihi kumanya simo tuhu?"
[14] Mbeyu ihandwayo na mntu ahandae mbeyu ni mbui ya Muungu.
[15] Wantu watuhu ni inga viya mbeyu zekwetiwazo siai. Ahoaho wategeezaho ida mbui ya Muungu, Ibiisi eza na kuiusa mwe mioyo yao.
[16] Wantu watuhu nao ni inga mbeyu zekwetiwazo mwe maiwe. Ahoaho wategeezaho mbui ida wakaihokea kwa kinyemi.
[17] Akini khaviwengia nakuwa na mazindo mwe mioyo yao. Mbui ida yekaa kwa misi micheche na kisingi cha suuba kikalawiiya, ahoaho mntu uyu hufa maya.
[18] Wantu watuhu inga mbeyu zekugwazo he miwa. Uwo ni msimo wa wada wekutegezao ida mbui,
[19] akini maatu ya mwe inusi na utiizi wa mai, na kukunda muno vintu vingi zikawengia mwe mioyo yao, zafintafinta ida mbui ya Muungu na kuvota kuvyaa matunda.
[20] Akini watuhu inga mbeyu zekwetiwazo he sanga ntana. Aho wategeeza ida mbui ya Muungu, wakaihokea na kuvyaa matunda watuhu makumi matatu, watuhu makumi mtandatu na watuhu makumi kumi.

*Koloboi yekugubikwayo*
*Luka 8:16-18*

[21] Yesu akaendeea kuwamba, "Uwo wantu wadaha kuwasha koloboi na kwengiza nyumbani na kuigubika kwa biga au kuika mzungui? Aah! Waiika uwanga ya kiango.
[22] Naho kintu chochose chekufiswacho chenda kioneke, na chochose chekugubikwacho chenda kigubulwe.
[23] Mwenye magutwi ya kutegeeza na ategeeze!"
[24] Naho akamba, "Tegeezani vitana kwa kia mtegeezacho! Miko idaida mtumiayo kuamuiiya watuhu, Muungu enda azitumie kuamuiiya nywie, nayo ata kai muno.
[25] Kwaviya mwena endaamemezewe, na mwesena endaahokwe kiya kidodo enacho."

*Msimo wa mbeyu ihotayo na kukua*

[26] Yesu akaendeea kugombeka, "Useuta wa Muungu inga yezayo mntu ahanda mbeyu mwe mnda.
[27] Kio agona, musi yu meso na kisingi icho mbeyu yahota na kukua yee mwenye khamanya vyekugosokavyo.
[28] Kwaviya sanga yenye yagosoa mimea kukua na kuvyaa, uvoka kulavya zani teke, naho dakua suke na kulawiiya uhemba wekudahayo.
[29] Uhemba ukabinda kudahaa, mntu uyo adoa nyengo na kuvoka kusenga, kwaajii kisingi cha ubosi kibua."

*Msimo wa mbeyu ya haladani*
*Matayo 13:31-32,34; Luka 13:18-19*

[30] Naho Yesu akagombeka, "Tiuiganye na mbwai Useuta wa Muungu? Tiutamwiize kwa simo zihi?
[31] Waigana na mbeyu ya haladani, ambayo ni ndodo kwesima zose zihandwazo mwe inusi.
[32] Akini ikabinda kuhandwa, yahota na kutenda ziti kuu kwesima yose mwe mnda. Naho matambi yakwe yawa makuu hata wadege wa uwanga wazenga masasa yao mwe matambi yakwe."
[33] Yesu akawabiikia mbui zakwe kwa simo tuhu nyingi inga izo, akatamwiiana nao kadii wekudahavyo kumanya.

34 Khekutamwiiya nao chochose iya kwa simo, akini ekuaho hamwe na wahina wakwe ikedu akawamba kia kintu.

*Yesu atuiza khusi khai*
*Matayo 8:23-27; Luka 8:22-25*

35 Msi udauda, guoni Yesu akagombeka na wahina wakwe, "Titeni phande ntuhu ya tondoo da mazi."
36 Aho wakabada dia zumwezumwe da wantu, wahina wakwe wakengia mwe ngaawa ekuwayo Yesu. Viyaviya ngaawa ntuhu zikambasa.
37 Khusi khai ikaawiya, mkubwaniso wa mazi ikatoa ida ngaawa, nayo ika-
voka kumema mazi. 38 Yesu ne yun-
yuma ya ngaawa, naho kagonea mwe kigonea, wahina wakwe wakamwenua na kumwamba, "Mhinyi kwa mbwai khutipatiiza khuona inga tinda tiuye na nyuma?"
39 Yesu akenuka na kuiwakia ida khusi na kuyamba mawimbi, "Nyamaa! Twiiya!" Ahoaho khusi ikaeka, ne kwatwiiya tui.
40 Yesu akawauza wahina wakwe, "Kwa mbwai mwaogoha? Khamzati kuzumiiya du?"
41 Naho wakaogoha muno, wakauzana wenye, "Uyu nndai? Hadi khusi na mawimbi vyamtegeeza!"

# 5

*Yesu amhonya mntu mwenye mazaiko*
*Matayo 8:28-34; Luka 8:26-39*

1 Yesu na wahina wakwe wakabua phande ya kaidi ya tondoo da mazi ya Galilaya mwe si ya Wagelasi.
2 Ahoaho Yesu ekuseeaho mwe ngaawa akakintana na mntu yumwe mwenye mazaiko kaawiiya he mambia.
3 Mntu yuda ne akekaa kwe mambia na khahana mntu mwekudaha kumtoza na kumzengeteza minyololo.
4 Maa nyingi wamzengeteza kwa phingu mwe mikono na minyololo mwe miundi, akini kia maa akadaha kuidumua iyo minyololo na izo phingu, naho khahana mntu mwekudaha kumuemeza.
5 Msi na kio ne akekaa mwe mambia na kwe miima akagutia na kwesengasenga na maiwe.
6 Ekumuonaho Yesu kwa hae, akamguukia, akamwenamia.
7 Akamba kwa mgutio mkuu, "Una mbwai nami?, Yesu Mwana wa Muungu mwe uko uwanga muno! Nakuhembeza kwa zina da Muungu wesekunisuumiza!"
8 Akagombeka ivyo kwaviya Yesu nekawa kamwamba, "Ee zaiko mlaweni mntu uyu!"
9 Aho, Yesu akamuuza, "Zina dako ni ndai?" Ne amtambaisa, "Zina dangu ni hindoo kwaviya ti wangi."
10 Naho akamhembeeza Yesu asekuwaguusa mwe si ida.
11 Hehi na aho ne kuwa na tintimo kuu da nguuwe uisi he mpoomoko wa muima.
12 Aho mazaiko yada yakamhembeza Yesu na kumwamba, "Tegae tikengie kwa wada nguuwe."
13 Naye akayekha uhusa, aho yada mazaiko yakamlawa mntu yuda, yakawengiia wada nguuwe. Tintimo dose ido da nguuwe ne diwa elufu mbii dikaseeya mwe uda mpoomoko mkai dikengia mwe tondoo da mazi.
14 Waisi wa wada nguuwe, ne waguuka na kuambaza mbui ida mwe mizi na mwe minda. Wantu wakaita wakauwe yekulawiayo.
15 Ne wamtimia Yesu, wakammbuiya mntu yudayuda mwekuwa kakwewa na hindoo da mazaiko kekaa asi, kavaa nguo, na akii zakwe zimuuiya, wantu wose wakaogoha.
16 Na wada wekuonaho mbui ida ne wawamba wantu watuhu, chekulawiacho kwa yuda mntu mwekuwa na mazaiko hamwe na mbui za wada nguuwe.
17 Aho, wantu wakamhembeza Yesu alawe mwe si yao.
18 Yesu ekuwaho akwea mwe ngaawa yuda mntu mwekuwa na mazaiko akamhembeza waite wose.
19 Akini Yesu akamweemeza, naho akamwamba, "Hita kwenu kaya kwa wanduguzo ukagombeke yada yose Zumbe ekukugosoeavyo na kukufiia mbazi."
20 Aho yuda mntu akaita na kuvoka kubiikia Dekapoli mana yakwe ni si ya mizi kumi dimwe, mbui zose Yesu ekumgosoeavyo. Wantu wose wakahondomaa.

*Yesu awahonya mwana Yailo na mvyee yumwe*
*Matayo 9:18-26; Luka 8:40-56*

21 Yesu akaita vituhu phande ya kaidi ya tondoo da mazi kwa ngaawa. Zumwezumwe da wantu dikammemea hemeso yakwe, naye ne kagooka khandakhanda ya tondoo da mazi.
22 Aho akeza mntu yumwe etangwa Yailo yumwe wa wakuu wa Nyumba ya kuvikia Wayahudi, ekumuonaho Yesu akakinta mavindi hemeso yakwe.
23 Akamhembeeza akamba, "Mwanangu wa kivyee mdodo ni mtamu yu hehi na kuuya na nyuma. Nakuhembeza tite ukamuikie mikono yako adahe kuhona na aendeee kwekaa."
24 Aho, Yesu akahauka hamwe naye. Wantu wangi wakamtongea Yesu na kumfintafinta kia phande.

25 Aho ne hawa na mvyee yumwe mwekuwa na utamu wa mtuo kwa kisingi cha myaka kumi dimwe na miidi.

26 Mvyee uyo ne kaangadika muno kuita kwa waganga wangi. Na etiho kaza mai zakwe zose, akini khekuona ebae, iya kaendeea kuwa mtamu muno.

27 Naye uyo mvyee ne kasikia mbui za Yesu ne ahenya gatigati ya dia zumwezumwe da wantu. Akamlawiiya Yesu kwa nyuma na kudonta nguo yakwe.

28 Kwaviya ne kegombekea mwe moyo wakwe, “Nikadonta nguo yakwe, nenda nihone.”

29 Ahoaho utamu wa mtuo ukanyaa, akeona mwe mwii wakwe kahona utamu wakwe.

30 Ahoaho, Yesu akamanya udaho umlawa. Neahitukia dia zumwezumwe da wantu na kuwauza, “Nndai mwekudonta nguo yangu?”

31 Wahina wakwe wakamtambaisa, “Woona wantu wakufintafinta, naho wauza ni ndai mwekukudonta?”

32 Akini Yesu akakauwa phande zose amwone nndai mwekumdonta.

33 Aho yuda mvyee akamanya yekumlawiayo, akeaviiza, akakama kwa kuogoha, aketambika asi hemeso ya Yesu, na kugombeka yose yekumlawiayo.

34 Yesu akamwamba, “Mwanangu kuzumiiya kwako kukuhonya, hita kwa utuivu naho utende mgima.”

35 Yesu ekuwaaho agombeka, ne weza wantu kulawa kwa Yailo mkuu wa Nyumba ya kuvikia Wayahudi, wakamwamba, “Mwanao kauya na nyuma kae, kwambwai wampisha mhinyi?”

36 Akini, Yesu khekuwaanduwa wekugombekacho nee amwamba yuda mkuu wa Nyumba ya kuvikia Wayahudi, “Usekuogoha, wee zumiiya du.”

37 Yesu khekukunda mntu yoyose amtongee, iya Petulo na Yakobo na Yohana nduguye Yakobo.

38 Wekubuaho mwe nyumba ya Yailo, Yesu ne aona wantu waketambikatambika asi wakiiya na kutoa bwaimbo.

39 Yesu ne engia gati, na kugombeka, “Kwa mbwai mwetambikatambika na kuiiya? Mndee khekuuya na nyuma, kagona.”

40 Akini wowo wakamseka. Aho akawalavya wose chongoi, akamdoa tati yakwe na mami yakwe da yuda mwana na wahina wakwe watatu, wakengia mwe chumba wekumwikacho yuda mndee.

41 Naho akamtoza mkono, na kumwamba, “Talita, komu,” Mana yakwe “Mndee mdodo nakwamba enuka!”

42 Ahoaho mndee yuda akagooka, na kuvoka kuita. Mndee yuda ne kawa na myaka kumi dimwe na miidi. Aho wantu wakahondomaa muno kwa dekulawiado.

43 Akini Yesu akawaemeza wasekugombeka kwa mntu yoyose ida mbui. Naho akawamba wamwekhe khande yuda mndee.

# 6

*Yesu aemewa uko Nazaleti*
*Matayo 13:53-58; Luka 4:16-30*

1 Yesu akalawa hada, akaita mwe mzi wakwe na wahina wakwe ne wamtongea.

2 Msi wa Kuhumwiiza wekubuaho, akavoka kuhinya mwe Nyumba ya kuvikia Wayahudi. Wantu wangi wekumtegeezao wakahondomaa wakauza, “Uwo mbui izi kazilavia kuhi? Ni udaho uhi ekwekhigwao? Naho agosoa viivihi tangio izi?

3 Uwo uyu khii yuda seemaa, mwana Maliamu, wanduguze ni Yakobo na Yusufu na Yuda na Simoni? Na maumbuze wekaa ahaaha hetu?” Wantu ne wawa na matumatu nae.

4 Yesu akawamba, “Muoni wa Muungu akundwa kia hantu iya mwe si yakwe na kwa wanduguze na kaya kwakwe khakundwa.”

5 Khekugosoa tangio zozose hada, iya akaika mikono kwa watamu wacheche, ne awahonya.

6 Yesu akahondomaa muno, kwaviya wantu khawokuzumiia.

*Yesu awagiiya wahina kumi dimwe na waidi*
*Matayo 10:5-15; Luka 9:1-6*

Naho Yesu neaita mizi ya hehi, akahinya wantu.

7 Akawetanga wada wahina kumi dimwe na waidi, akavoka kuwaagiia waidiwaidi. Ne awekha udaho wa kuguusa mazaiko.

8 Akagombeka, “Msekudoa kintu chochose mwe ntambo yenu iya ngoda du. Msekudoa khande, mkwiji wala hea.

9 Vaani sabana, akini mwesekudoa gwanda tuhu.”

10 Vituhu akawamba, “Kaya yoyose mwendayo mhokewe ekaani umo na msekusamasama kuita kaya tuhu hadi mwendaho mhauke mwe mzi uwo.

11 Hantu hohose wantu wendawo wawaemee kuwahokea au kuwategeeza, haukeni aho na kung'unteni sanga ya mwe miundi yenu inga hinyo kwao.”

12 Awo wakahauka na kuwabiikia wantu wamhitukie Muungu.

13 Wakaguusa mazaiko mangi na kuwasisa mavuta ya mizaituni watamu wangi na kuwahonya.

*Ufe wa Yohana mbatiiza*
*Matayo 14:1-12; Luka 9:7-9*

14 Naho, Seuta Helode ekutegeezaho mbui izi kwaviya togoo za Yesu ne ziambazwa kia hantu. Wantu watuhu ne wakagombeka, “Yohana mbatiiza kayuyuka kulawa mwe wekufao, ne mana udaho wa kugosoa vihii wagosoa ndima.”

15 Wantu watuhu wakagombeka, “Uyu ni Eliya” Na wantu watuhu ne wagombeka, “Uyu ni Muoni wa Muungu inga yumwe wa Waoni wa Muungu wa kae.”

16 Akini Helode ekusikiaho akagombeka, “Uyu ni Yohana mbatiiza! Nekumsengae mtwi, tambe kayuyuka!”

17 Aho bosi Helode mwenye kakunda Yohana Mbatiiza agwiwe na aikwe mwe kifungo. Helode katenda ivyo kwaajii ya Helodia, mvyee uyo ne nimkaza Filipo, nduguye Helode.

18 Kwaviya Yohana ne kamwamba Helode, “Khio vitana kumdoa mkaza nduguyo.”

19 Aho Helodiya akakimwa muno na Yohana na akakunda kumkoma, akini khekudaha kumkoma.

20 Helode ne akamuogoha Yohana kwaviya kamanya Yohana ni mntu mtana na yedi, ivyo akamkindia asekukomwa. Helode kakundisa kumtegeeza Yohana, akini ekumtegezaho, akahungumia muno mwe moyo wakwe.

21 Msi umwe Helodia akapata phasi kisingi cha sikukhuu ya khumbuso da kuvyaigwa kwakwe Helode. Helode kawagosoeya ntafuno wadaa waongoezi na wakuu wa mahindoo hamwe na wagookezi wose wa Galilaya.

22 Aho mwana kivyee wa Helodiya akengia akavina, akawatamiza muno Helode na wageni wakwe. Seuta Helode akamwamba yuda mndee, “Niombeza dodose ukundado, nami nenda nikwekhe.”

23 Naho akamwahiiya, “Chochose wendacho uniombeze, nenda nikwekhe hata ntii ya useuta wangu.”

24 Aho uyo mndee akalawa kumuuza mami yakwe, “Niombeze mbwai?”

Mmaa yakwe akamtambaisa, “Ombeza mtwi wa Yohana Mbatiiza.”

25 Yuda mndee akamuuiya seuta kinyionyio na kumwombeza, “Nakunda unekhe isasa mtwi wa Yohana Mbatiiza mwe chano.”

26 Seuta akoona usungu, akini kwaviya ya kuaha kwakwe na kwaviya ya wageni wose wekuwao mwe ntafuno, khekudaha kumuemeea.

27 Aho seuta akamwagiiya asikai kueta mtwi wa Yohana Mbatiiza. Asikai akaita akamdumua mtwi Yohana Mbatiiza.

28 Yuda asikali akaueta mtwi mwe chano, akamwekha yuda mndee, na mndee naye akamwekha mami yakwe.

29 Wahina wa Yohana Mbatiiza wekusikiaho mbui ida, ne waita wakaudoa mwii wakwe wakaugea mwe mbia.

*Yesu awekha khande wantu elufu shano*

*Matayo 14:13-21; Luka 9:10-17; Yohana 6:1-14*

30 Wada waagiiwa wakauya wakakintana hemeso ya Yesu na kumwamba yose wekugosoayo na kuhinya.

31 Yesu akawamba, “Titeni swie ikedu kwesiho wantu mkahumwiize” kagombeka ivyo kwaviya ne hana wantu wangi, wekuwao wabua aho na kuhauka hata Yesu na wahina wakwe khawokudaha kuwa na phasi ya kuda khande.

32 Aho wakahauka wowodu kwa ngaawa na kuita kwesiho wantu.

33 Akini wantu wangi wakawaoona wakaita naho wakawamanya. Ne wantu kulawa kia mzi wakaguuka na kuongoa kubua ekuako aita Yesu na wahina wakwe.

34 Yesu ekuseeaho mwe ngaawa, ne aona zumwezumwe da wantu, akawafiia mbazi, kwaviya ne wawa inga ngoto wesao kuwa na muiisi. Akavoka kuwahinya mbui nyingi na nyingi.

35 Wahina wakwe wakambasa Yesu wakamwamba, “Hantu aha nihe kiwawe na zua daswa.

36 Wabade wantu awa waite mwe minda na mwe mizi ya hehi, wakague khande.”

37 Akini Yesu akawatambaisa, “Wekheni nywie khande.” Ne wamuuza, “Khuona inga tendatikundigwe tiwe na mshahaa wa mntu wa miongo minane idahe kugua mabumunda na kuwekha wantu wade?”

38 Yesu akawauza, “Mna mabumunda mangahi? Hitani mkakauwe.” Wekumanyaho, wakamwamba, “Kuna mabumunda mashano na samaki waidi.”

39 Aho Yesu akagombeka na wahina wakwe wawaike wantu vizumwezumwe na kwekaa asi he mani.

40 Ne wekaa mwe vizumwezumwe vya wantu makumi kumi na vizumwezumwe vya makumi mashano.

41 Naho Yesu akadoa yada mabumunda mashano na wada samaki waidi, akakauwa uwanga kwa Muungu, akavijaiya, ne abendua yada mabumunda na kuwekha wahina wakwe wawapangie wantu. Na wada samaki waidi wawapangie wose.

42 Wantu wose ne wada na kweguta.

43 Wahina wakwe wakadodoa phugutio za vyekusigaavyo vya mabumunda na samaki wakamemeeza ngahu kumi dimwe na mbii.

44 Wekudao ida mikate ne wawa wagosi elufu shano.

*Yesu enda uwanga ya mazi*
*Matayo 14:22-33; Yohana 6:15-21*

45 Ahoaho Yesu akawamba wahina wakwe wakwee mwe ngaawa wamuongoee kuita Betisaida, phande ya kaidi ya tondoo da mazi, kisingi yee aaga zumwezumwe da wantu.

46 Ekubindaho kuagana nao, ne aita mwe muima kuvika Muungu.

47 Yekubuaho guoni, ngaawa ne igatigati ya tondoo da mazi, akini Yesu ne awa ikedu mwe sanga khavu.

48 Aho akoona wahina wakwe mwe ngaawa wakepisha kwa kutoa makasia, kwaviya ne wakahigana na khusi. Hehi na kucha, Yesu akawabasa wahina uku enda uwanga ya mazi, akakunda kuwemboka.

49 Akini wekumuonaho akenda uwanga ya mazi, ne wammamakhanya ni mzimu, wakakema.

50 Kwaviya wose wekumuonaho ne waogoha muno. Ahoaho Yesu akagombeka nao, "Twiiyani msekuogoha! Ni mie!"

51 Naho akengia mwe ngaawa wekuwamo na khusi ikatwiiya, wahina wakwe ne wahondomaa muno.

52 Kwaviya ne khawazati kumanya mana ya yada mabumunda wekudao wantu elufu shano.

*Yesu awahonya watamu uko mwe si ya Genesaleti*
*Matayo 14:34-36*

53 Wakemboka phande ya kaidi ya tondoo da mazi wakabua mwe si ya Genezaleti, aho ne wagea kigomogomo.

54 Wekulawaho mwe ngaawa, wantu naho wakammanya Yesu.

55 Naho wakaita kinyionyio mwe si yose, wakawenua watamu mwe vilago vyao ne wamwegaiya Yesu, hohose hada wekutegeezaho yuaho.

56 Kia hantu Yesu ekubuaho, mwe mizi na mwe minda, wantu ne wawaika watamu wao wazoi, Wakamhembeeza wadon'te du msao wa nguo yakwe, na wose wekumdontao nee wahona.

# 7

*Mahinyo ya mababa*
*Matayo 15:1-9*

1 Wamwe wa Mafalisayo na Wahinyi wa Miko wekuwao walawa Yelusalemu ne wakintana hemeso ya Yesu.

2 Wakoona wamwe wa wahina wa Yesu wada khande kwa mikono yao kwesiho kusunta inga ikundingwavyo na Miko ya Wayahudi.

3 Mafalisayo na Wayahudi wose watozeeza mahinyo wekuyahokeayo kwa wadaa wao, khawada khande yoyose hadi wasunte mikono yao vitana kubua mwe kiko.

4 Naho khawada chochose kulawa gwiiyo hadi wasunte mikono. Viyaviya watozeeza mahinyo matuhu wekuhokeayo kuvokea kae, inga viya wasuntavyo vikombe na nyungu na via vya shaba.

5 Aho wada Mafalisayo na Wahinyi wa Miko wakamuuza Yesu, "Kwa mbwai wahina wako khawatongea mahinyo ya wadaa? Iya wada khande kwesiho kusunta mikono?"

6 Yesu akawatambaisa, "Muoni Isaya ne koona kwei kwenu nywie wabakha inga viya ekugondavyo, Muungu kagombeka, 'Wantu awa wanitegeeza mwe miomo yao, iya mioyo yao ihae na mie.

7 Naho wanivikia buwe, kwaviya mbui wazihinyazo ni miagiiyo ya kiuntudu wakigombeka ayo ni mahinyo ya Muungu!'

8 "Nyie mwabada Miko ya Muungu na kutongea miagiiyo ya wantu."

9 Yesu akatendesa kugombeka, "Nyie mwadaha kuiemea kwa unyanyi Miko ya Muungu kwaajii ya kutongea mahinyo yenu!

10 Mana Musa kagombeka, 'Wategeezeni tati zenu na mami zenu naho mntu yoyose amdumuae tati yakwe au mami yakwe yakundigwa akomwe.'

11 Akini nywie mwahinya, inga mntu mwenacho kintu kidahacho kumwambiiza tati yakwe au mami yakwe, akini akamba kintu icho ni 'Kolobani' yani ni funge kwa Muungu.

12 Naho kheshuutiza vituhu kumwambiiza tati yakwe au mami yakwe.

13 Ivi ne mbeavyo mbui za Muungu, kwaajii ya mahinyo mhokezanayo. Naho mwagosoa mbui nyingi inga izi."

*Mbui zimtendazo mntu asekukudigwa na Muungu*
*Matayo 15:10-20*

14 Yesu ne awetanga vituhu zumwezumwe da wantu, akawamba, "Nitegeezani nyose, mmanye."

15 Khakuna kintu chengiacho kwa mntu kidahacho kumtenda asekukundigwa na Muungu, akini kilawacho ndani ya mntu nee kimtendacho mntu asekukudigwa na Muungu.

16 Mwenye magutwi ya kutegeeza na ategeeze!

17 Ekubadaho zumwezumwe da wantu na kwengia kaya, wahina wakwe wakamuuza mana ya msimo uwo.

18 Yesu akagombeka, "Hata nywie khamna umanyi? Khammanya kintu kimwengiacho mntu kulawa chongoi khakidaha kumtenda mntu asekukudigwa hemeso ya Muungu,

19 kwaviya khachekumwegia mwe moyo wakwe iya mwe ifu, naho chalawa chongoi mwe mwii." Kwa kugombeka ivyo, Yesu kauusu khande zose ziigwe.

20 Akatendesa kugombeka, "Kimlawacho mntu ndani yakwe ne kimtendacho asekukudigwa hemeso ya Muungu.

21 Kwaviya mwe moyo wa mntu kwalawa mbui zesazo kutama, na ukianga na ubavi na ukomaji,

22 na kianga na choyo na ubanasi na utiizi na umeo wa mai na kinyuu na kubea na kibui na ubahau.

23 Mbui zose izo zalawa mwe moyo wa mntu na kumtenda asekukudigwa hemeso ya Muungu."

*Kuzumiiya kwa mvyee yumwe*
*Matayo 15:21-28*

24 Yesu akahauka aho na kuita mwe si ya hehi na mzi wa Tilo. Uko akengia mwe kaya mwenga na khekukunda mntu yoyose ammanye, akini khekudaha kwefisa.

25 Aho mvyee yumwe kawa na mwanaye wa kindee mwekuwa na zaiko, ekutegezavyo mbui za Yesu akeza hada na aketambika asi hemeso ya Yesu.

26 Mvyee yuda khekuwa Myahudi, iya nee ni mwenyezi wa Silofoinike mwe si ya Siliya. Aho akamheembeza Yesu amlavye mazaiko yuda mwanawe.

27 Akini Yesu akamtambaisa, "Eka wana wegute, kwaviya khio vitana kudoa khande ya wana na kuwasia makui."

28 Yuda mvyee ne amtambaisa, "Zumbe" ni vitana, "Akini hata makui nayo yeaho asi ya meza yadaha kudodoa phugutio za khande vyekusigazwavyo."

29 Naho Yesu ne agombeka, "Kwaajii ya kutambaisa ivyo, hita kaya, naho wenda umbwiie mwanao zaiko dimlawa!"

30 Aho yuda mvyee akauya kaya na kumbwiia mwanawe kagona mwe usazi na dia zaiko dimlawa kae.

*Yesu amhonya mntu mwenye kisita kikai na kiziba*

31 Yesu ne alawa mwe mihaka ya mzi wa Tilo akemboka gatigati ya Sidoni akaita Dekapoli mana yakwe si ya mizi kumi, kwembokea tondoo da mazi ya Galilaya.

32 Aho wakamwegaiiya mwenye kisita kikai na kiziba, wakamheembeza amuiikie mikono.

33 Yesu akamuusa mwe dia zumwezumwe da wantu, akamgea vyaa mwe magutwi ya yuda mntu, ne aswa ovu mwe vyaa vyakwe na kumdonta mwe ulimi wakwe.

34 Naho akakauwa uwanga, akatoa mhezemuko akamwamba, "Efata," Mana yakwe, "Vuguka."

35 Ahoaho magutwi yakwe yakavuguka na ulimi wakwe ukaegea na kuvoka kutamwiiya vitana.

36 Yesu ne awaemeza wantu wasekumwamba mntu yoyose mbui izo. Akini ekuwaemezavyo ne watendesaho kuziambaza mbui izo.

37 Wantu wose wakahondomaa muno, wakagombeka, "Kagosoa yose matana kawajaiya viziba kutegeeza na mabubu kudaha kugombeka!"

# 8

*Yesu awekha khande wantu elufu nne*
*Matayo 15:32-39*

1 Kisingi icho, zumwezumwe da wantu dikakintana vituhu, na khawekuwa na khande. Aho, Yesu akawetanga wahina wakwe akawamba,

2 "Nawafiiya mbazi wantu awa kwaviya wawa na mie kwa misi mitatu, naho khawana khande.

3 Nikawabada waite kaya kwesaho kuda wenda wagwe msae siai, kwaviya watuhu walawa hae."

4 Wahina wakwe wakamuuza, "Hanu he kiwawe tendatikundigwe tipatie kuhi mabumunda ya kuwegusa wantu wose awa?"

5 Yesu akawauza, "Mna mabumunda mangahi?" Wakamtambaisa, "Tina mabumunda mfungate."

6 Aho Yesu akawamba wantu wekae asi, akayadoa yada mabumunda mfungate, akamtogoa Muungu, akayabendua yada mabumunda, akawekha wahina wakwe wawapangie wantu, ne wawapangia.

7 Naho kuwa na samaki wacheche. Yesu akamtogoa Muungu, na kuwekha wahina wakwe wawapangie wantu viyaviya.

8 Wantu wose wakada, na kweguta. Ne wahina wakwe wakadodoa phugutio za khande za vyekusigaavyo na kumemeeza ngahu mfungate.

9 Naho wekudao khande wabua wantu elufu nne, Yesu akabadana nao.

10 Ahoaho akakwea ngaawa hamwe na wahina wakwe na kuita mzi wa Dalumanuta.

*Mafalisayo wakunda tangio*
*Matayo 12:38-42; 16:1-4*

11 Wamwe wa Mafalisayo wakambasa Yesu na kuvoka kutambaisana nae. Wakamgeeza, wakakunda agosee tangio koonesha kuwa udaho wakwe walawa uwanga kwa Muungu.

12 Akini Yesu akoona usungu mwe moyo wakwe akagombeka, "Ni kwambwai wantu wa uvyazi unu wakunda tangio? Kwei nawamba khahana tangio zozose zendazo mwekhigwe uvyazi unu."

13 Aho akawabada na akakwea vituhu ngaawa, akavoka ntambo ya kuita phande ya kaidi ya mazimshindo.

*Hamila ya Mafalisayo na Helode*
*Matayo 16:5-12*

14 Wahina wakwe wajaa kudoa mabumunda ya kuiganyia. Ne wawa na bumunda dimwe mwe ngaawa.

15 Yesu akawaemeza, “Kauwani muno, na mwekae hae na hamila ya Mafalisayo na hamila ya Helode.”

16 Wahina wakavoka kuuzana, “Agombeka ivi kwaviya khatina mabumunda.”

17 Yesu kamanya ayo ne awamba, “Kwambwai mwauzana mbui ya kwesekupata mabumunda? Nyie khammanya au khamna umanyi? Kwambwai mioyo yenu yatoga?

18 Mna meso akini khamdaha kuona? Mna magutwi akini khamdaha kutegeeza? Khambukhua?

19 Kisingi kiya nikubenduaho yada mabumunda mashano na kuwekha wantu elufu shano? Mdodoa ngahu nyingahi za phugutio za khade za vyekusigaavyo?” Wahina wakatambaisa, “Ni ngahu kumi dimwe na viidi.”

20 Yesu akawauza, “Na hada nikubenduao yada mabumunda mfungate na kuwekha wantu elufu nne wakada, mdodoa ngahu nyingahi za phugutio za khande za vyekusigaavyo?” Ne wamtambaisa, “Ni ngahu mfungate.”

21 Aho akawauza, “Khamzati kumanya?”

*Yesu amhonya mntu tuntu uko Betisaida*

22 Yesu akabua mzi wetangwao Betisaida hamwe na wahinyi wakwe. Uko wantu wakamwegaiya mntu tuntu, wakamheembeza amdonte.

23 Yesu akamtoza mkono yuda tuntu na kumlavya chongoi ya mzi. Akamswiia ovu mwe meso, akamwiikia mikono kwe meso na kumuuza, “Wadaha koona chochose?”

24 Yuda tuntu akakauwa na kugombeka, “Naona wantu wakenda inga miti yendayo.”

25 Naho Yesu akamwiikia vituhu mikono yakwe mwe meso ya yuda tuntu, naye yuda mntu akafua meso, ne meso yakavuguka, koona kwakwe kukamuuiya akoona kia kintu pwii.

26 Yesu akamwamba aite kaya na kumuemeza, “Naho usekwengia mwe mzi.”

*Petulo agombeka pwii Yesu ne Klistu*
*Matayo 16:13-20; Luka 9:18-21*

27 Naho Yesu na wahina wakwe wakaita mwe mizi ya hehi na Kaisalia Filipi. Wekuwaho siai Yesu akawauza wahina wakwe, “Wantu wamba mie nndai?”

28 Wakamtambaisa, “Watuhu wamba wee ni Yohana mbatiiza, watuhu wamba u Eliya na watuhu wamba ni yumwe wa Waoni wa Muungu.”

29 Yesu akawauza, “Na nywie mwamba mie nndai?” Petulo akagombeka, “Wee ne Klistu.”

30 Naho Yesu akawaemeza wasekugombeka kwa mntu yoyose mbui zakwe.

*Yesu agombeka mbui ya suuba, ufe na kuyuyuka kwakwe*
*Matayo 16:21-28; Luka 9:22-27*

31 Naho Yesu akavoka kuwahinya wahina wakwe, nlazima Mwana wa Mntu ekhigwe usuumizi mwingi na kuemewa na wadaa na Waviki wakuu na Wahinyi wa Miko. Enda akomwe, akini mwe msi wa ntatu enda ayuyuke.

32 Yesu kagombeka mbui ida pwiii. Aho Petulo akamdoa Yesu khandani, na kuvoka kumuakia.

33 Akini Yesu akahituka na kuwakauwa wahina wakwe, akamuakia Petulo na akamba, “Hauke hemeso yangu Ibiisi wee! Umamakhanyo wako khio wa Muungu iya ni wa kiuntu.”

34 Naho akawetanga zumwezumwe da wantu hamwe na wahina wakwe akawamba, “Inga mntu yoyose akakunda kunitongea nlazima eemee mwenye, enue mhamba wakwe anitongee.

35 Kwaviya mntu yoyose akundae kuohoa ugima wakwe mwenye enda awaze, akini mntu mwaza ugima wakwe kwaajii ya mie na kwaajii ya Mbui Yedi za Muungu enda ayaohoe.

36 Mntu enda ekhigwe mbwai inga akekhigwa vintu vyose vya inusi na kuwaza ugima wakwe?

37 Khahana kintu wendacho ukilavye ili uupate ugima?

38 Mntu yoyose mwenda anionee soni mie na mahinyo yangu, mwe uvyazi unu wa kianga na cha mavigaviga, Mwana wa Mntu enda amuonee soni mntu uyo, kisingi endaho auye he ukuu wa Tati yakwe hamwe na wandima wa Muungu wa uwanga.”

## 9

1 Yesu akatendesa kugombeka, “Nawamba kwei, kuna wantu watuhu aha khawana wauye na nyuma, hadi wendaho wauone Useuta wa Muungu ukeza kwa udaho.”

*Yesu ahituka cheni*
*Matayo 17:1-13; Luka 9:28-36*

2 Yekwembokaho misi mtandatu, Yesu akawadoa Petulo na Yakobo na Yohana,

akaita nao uwanga ya muima ulehao kwe-
saho wantu. Uko Yesu akahituka cheni
hemeso yao.
3 Nguo zakwe zikang'aa pee, ung'ao
wakwe khahana mnyukuaji yoyose mwe
inusi mdaha kunyukuua nguo zing'ae inga
izo.
4 Naho Eliya na Musa wakalawiia
wakatamwiiya na Yesu.
5 Petulo akamwamba Yesu, “Mhinyi, ni
vitana sie tiwe aha. Ebae tikazenga
makumbi matatu, dimwe dako, dimwe da
Musa na dimwe da Eliya.”
6 Petulo na weziwe wakaogoha muno
hata wasekumanya da kugombeka.
7 Naho kukalawia zunde dikawagubika,
na mgutio ukategeezeka kulawa mwe dia
zunde, “Uyu ne Mwanangu wa kigosi
nimkundaye mtegeezeni.”
8 Ahoaho wahina wakakaua vituhu,
akini khawekumwona mntu mtuhu iya
Yesu ikedu.
9 Aho wekuwaho wakaseea ku-
lawa kwe muima, Yesu akawaemeza,
wasekumwamba mntu mbui zozose
wekuzionazo, adi aho Mwana wa Mntu
endaho ayuyuke.
10 Aho wakatoza miagiiyo iyo, akini
wakauzana, mana ya kuyuyuka ni mbwai?
11 Wahina wakamuuza Yesu, “Kwamb-
wai Wahinyi wa Miko wagombeka, Eliya
akundigwa avoke kweza?”
12 Yesu akawatambaisa, “Ni kwei, Eliya
avoke kweza na kuika mbui zose vi-
tana. Ata ivyo kwambwai iandikwa mwe
Maandiko ya Mungu, Mwana wa Mntu
enda asumizwe muno na kubewa?
13 Akini nawamba Eliya keza kae naho
wakamgosoa wakundavyo inga Maandiko
yekugombekavyo kwaajii yakwe.”

*Yesu amhonya mbwanga mwenye mazaiko*
*Matayo 17:14-21; Luka 9:37-43a*

14 Naho wekuwabwiaho wada wahina
watuhu, ne waona zumwezumwe kuu da
wantu diwaikia bunga. Na wamwe wa
Wahinyi wa Miko watambaisana nawo.
15 Ahoaho wada wantu wekum-
wonaho Yesu, wakahondomaa muno,
wakamguukia na kumuugusa.
16 Yesu akawauza wahina wakwe,
“Mwatambaisana mbwai?”
17 Aho mntu yumwe mwe dia
zumwezumwe akagombeka, “Mhinyi
khimueta mwanangu kwaviya ana
mazaiko yekumgosoayo asekudaha ku-
tamwiiya.
18 Naho zaiko ido dikamkwea mwanangu
damgwisa asi na kumtenda alawe fuo mwe
kanwa, na akeuma meno naho akakama
mwii wose. Kiwamba wahina wako
walavye ido zaiko, akini khawekudaha.”
19 Yesu akagombeka, “Nywie kivyazi
chesacho kuzumiiya! Nenda nekae na
nywie hata ini? Nenda niwazizimize hata
ini? Mweeteni hangu!”
20 Naho wakamweta yuda mbwanga kwa
Yesu. Na dia zaiko dekumuonaho Yesu
dikamsingisa, yuda mbwanga akagwa asi,
akagaagaa ne alawa fuo mwe kanwa.
21 Yesu akamuuza tate ya yuda mb-
wanga, “Mazaiko aya yamvoka ini?” Nee
amtambaisa, “Kuvokea udodo wakwe.
22 Maa zose zaiko idi damgwisa mwe
moto na mwe mazi, ili dimkome. Inga
ukadaha tifiiye mbazi na kutiambiza!”
23 Yesu akagombeka, “Ati ukadaha, Mbui
zose zadahika kwa yuda azumiiae.”
24 Aho tati yakwe yuda mbwanga akatoa
vuzo kwa mgutio mkuu, na akamba
“Nakuzumiia, niambiza kwesekudaha
kuzumiiya.”
25 Yesu ekuonaho zumwezumwe da
wantu dagenyea hemeso yakwe, ne
amwamba dia zaiko, “Wee zaiko umgosoae
mwana uyu asekudaha kugombeka
na kutenda kiziba, nakwamba mlawe
mbwanga uyu usekumuuwiya vituhu!”
26 Aho zaiko dia ne dagutia na kumgea
ugwa mtwi na kumgwisa yuda mbwanga
asi na kumlawa. Yuda mbwanga akekaa
inga kimba hata watuhu ne wamba,
“Kauya na nyuma!”
27 Akini Yesu akamtoza mkono yuda mb-
wanga, akamwenua, ne agooka.
28 Aho, Yesu akengia kaya, wahina
wakwe wakamuuza wekuwaho ikedu,
“Kwambwai swie khatekudaha kumlavya
yuda zaiko?”
29 Yesu akawamba, “Zaiko inga idi khadi-
daha kulawa, kwesiho kuvika.”

*Yesu agombeka vituhu ufe wakwe*
*Matayo 17:22-23; Luka 9:43b-45*

30 Yesu na wahina wakwe walawa hada,
ne waita wakembokea Galilaya, Yesu
khekukunda wantu wowose wamanye
weiho,
31 kwaviya ne awahinya wahina wakwe,
akawamba, “Mwana wa Mntu enda egalwe
kwa wantu wendao wamkome. Akini bada
ya msi wa ntatu enda ayuyuke.”
32 Akini wahina wakwe khawokumanya
mahinyo yada na wakaogoha kumuuza.

*Nndai mwekuwa Mkuu?*
*Matayo 18:1-5; Luka 9:46-48*

33 Naho wakabua Kapelinaumu, ekuaho
kaya, Yesu akawauza wahina wakwe, “Ne
mkatambaisana mbwai mwe sia?”
34 Akini khawokuandua, kwaviya ne
wakatambaisana wakamba nndai mkuu
gatigati yao.

35 Yesu akekaa asi, akawetanga wada wahina wakwe kumi dimwe na waidi na kuwamba, “Mntu akakunda awe mgookezi akundigwa awe wa kisikizi na mndima wa wose.”

36 Naho akamdoa mwana mdodo akamgoosa gatigati yao, akamuumbatia na kuwamba,

37 “Mntu yoyose amhokeae mwana inga uyu kwa zina dangu anihokea mie, naho mntu anihokeaye mie, khanihokea miedu iya amhokeea yuda mwekuniagiiya.”

*Mwesekuhigana na swie yu hamwe na swie*

*Luka 9:49-50*

38 Yohana akamwamba Yesu, “Mhinyi, timuona mntu yumwe akalavya zaiko kwazina dako, nee tageeza kumweemeza kwaviya khayuko hamwe na swie.”

39 Akini Yesu akagombeka, “Msekumweemeza, kwaviya khahana mntu agosoae tangio kwa zina dangu, na ahoaho akagombeka ufyaimu wa mbui zangu.”

40 Kwaviya mntu yoyose esaye kuhigana nasi, yu hamwe na swie.

41 Nagombeka kwei mntu yoyose endae amyekhe kikombe cha mazi ya kudomea kwaviya nywie ni wantu wa Klistu, na kwei enda ahokee funge.

*Mageezo ya kugosoa mavigaviga*

*Matayo 18:6-9; Luka 17:1-2*

42 Mntu yoyose endae amkindie yumwe wa awa wadodo wanizumiiyao agosoe mavigaviga ni ebae kwa mntu uyo azongomezwe he singo yakwe iwe kuu da kubundugia na kutambikwa mwe mazimshindo.

43 Mkono wako ukakutenda kugosoa mavigaviga, uusenge. Ebae wengie mwe ugima kwesaho mkono umwe, kusima na mikono miidi na kwengia mwe moto wa misi yose wesao kukomeka.

44 Umo minyula yakwe khaifa na moto wa misi yose kwesiho kisiikizi.

45 Na muundi wako ukakutenda kugosoa mavigaviga uusenge! Ebae kwengia mwe ugima kwesaho muundi umwe kusima na miundi yose miidi na kutambikwa mwe moto wa kae na kae.

46 Uko mafunyo yakwe khayafa na moto wa misi yose wesao kukomeka.

47 Ziso dako dikakutenda ugosoe mavigaviga diuse. Ebae kwengia mwe Uzumbe wa Muungu na ziso dimwe kusima na meso yose maidi na kutambwikwa mwe moto wa kae na kae.

48 Minyula yakwe khaifa na moto wa misi yose kwesiho kisiikizi.

49 Kwaviya kiya yumwe enda agewe munyu kwa moto.

50 “Munyu ni mtana akini inga ikabanika inda ikweezwe na mbwai? Muwe na munyu mwe mioyo yenu na kwekaisa kwevana gatigati yenu.”

# 10

*Yesu auzwa mbui ya kuteguana na kubadana.*

*Matayo 19:1-12; Luka 16:18*

1 Yesu akalawa hada na kuita si ya Uyahudi, akadumua zigizigi da mazi da wa Yolodani. Zumwezumwe da wantu dikambasa vituhu, ne awahinya vituhu inga viya agosoavyo.

2 Aho Mafalisayo watuhu wakambasa na kumuuza kwa kumgeeza wakagombeka, “Miko yamuekea mgosi kumbada mkaziwe?”

3 Yesu akawatambaisa kwa kuwauza. “Musa kawekha mwiko wani?”

4 Wowo wakagombeka, “Musa katiagiiya kuwa mgosi aluusiwa kuandika bauwa ya kumbada mkaziwe.”

5 Yesu akawamba, “Musa kagonda mwiko uwo, kwaajii ya kutoga kwa mioyo yenu.”

6 Akini kuvokea kugosolwa inusi, Muungu kaumba mgosi na mvyee.

7 Ivyo mgosi enda ambade tati yakwe na mami yakwe, enda awe hamwe na mkaziwe.

8 Na awa waidi wenda wawe mwii umwe. Kwaivyo wowo khio waidi vituhu iya mwii umwe.

9 Naho, ekukintanisacho Muungu, mntu asekukibahua.

10 Wekwengiaho kaya vituhu, wahina wakwe ne wamuuza Yesu mbui ida.

11 Akawamba, “Mgosi yoyose ambadae mkaziwe na kutegua mvyee mtuhu, agosoa kianga.

12 Mvyee naye akambada mgosi yakwe na kutegulwa na mgosi mtuhu, yee nae agosoa kianga.”

*Yesu awajaiya wana wadodo*

*Matayo 19:13-15; Luka 18:15-17*

13 Wantu wakamwetea Yesu wana wadodo awadonte, akini wahina wakwe wakawaemeza wantu wada.

14 Yesu ekuonaho ivyo akakimwa, akawamba wahina wakwe, “Waekeeni wana wadodo weze hangu, naho msekuwakindia, kwaviya Uzumbe wa Muungu ni kwa wantu inga awa wana wadodo.

15 Nawamba kwei, mntu yoyose mwesekuuhokea Useuta wa Muungu inga mwana mdodo, khana engie umo.”

16 Akawahokea wana wada akawaumbatia na kuwaikia mikono kwa kuwajaiya.

*Mntu mwekuwa na mai nyingi*
*Matayo 19:16-30; Luka 18:18-30*

17 Yesu ekuvokaho ntambo yakwe, mntu yumwe nee amguukia, akakin'ta mavindi hemeso yakwe, akamuuza, “Mhinyi yedi, nitende viivihi nidahe kuhokea ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi?”

18 Yesu akamtambaisa, “Kwambwai wanetanga yedi? Khahana mntu yedi iya Muungu ikedu.

19 Miko waimanya, ‘Usekuwa mkianga, Usekukoma, Usekubawa, Usekugombeka uhonko, Usekutiiya Wategeeze tati yako na mami yako.’ ”

20 Nee amtambaisa, “Mhinyi, ayo yose khiyatozeeza kuvokea udodo wangu.”

21 Yesu akamkauwa akamkundisa akamwamba, “Kuhungukiwa na kintu kimwe. Hita ukatage vyose wenavyo navyo uwekhe hea wakiwa, nawe wenda uwe na utajii mwingi uwanga kwa Muungu naho unibase.”

22 Ekutegeezavyo ayo, ne agumia, na kuhauka kwa usungu, kwaviya ne kawa na mai nyingi.

23 Yesu akamagaza magaza kia phande na kuwamba wahina wakwe, “Yenda iwe vyatoga kwa mwenye mai kwengia mwe Useuta wa Muungu!”

24 Wahina wakwe wakahondomaa kwa ida mbui, akini Yesu akawamba vituhu, “Wanangu, vyatoga muno kwa wenye mai kwengia mwe Useuta wa Muungu!

25 Vyadahika ng'ombe kwengia mwe ntundu ya singano iya khaidaika kwa mntu mwe mai kwengia kwe Useuta wa Muungu.”

26 Wahina ne wahondomaa na kuuzana, “Nndai mwenda adahae kuoholwa?”

27 Yesu akawafuiya meso na kuwamba, “Kwa wantu khavidahika, akini kwa Muungu vintu vyose vyadahika.”

28 Naho Petulo akamwamba, “Kauwa, tibada vyose, tikakutongea weye.”

29 Yesu akagombeka, “Nawamba kwei, kia mntu mwekubada kaya, na wanduguze wa kigosi na maumbu zakwe na mami yakwe na tati yakwe na wanawe na minda yakwe kwaajii ya mie na Mbui Zedi,

30 enda ahokee maa mia kisingi cha isasa, kaya na wanduguze wa kigosi na maumbu na mame na wana na minda hamwe na suuba. Na mwe kisingi chezacho enda ahokee ugima wa kae na kae.

31 Akini wantu wangi wabosi wenda wawe wa kisikizi, na wakisikizi wenda wawe wabosi.”

*Yesu agombeka maa ya ntatu mbui ya ufe na kuyuyuka kwakwe*
*Matayo 20:17-19; Luka 18:31-34*

32 Naho wawa siai kuita Yelusalemu, na Yesu ne mwekuwaongweea, wahina wakwe wakamema maatu, na wantu wekuwatongeao nee waogoha. Yesu akawadoa wada wahina kumi dimwe na waidi akavoka kuwamba mbui zendazo zimlawie.

33 “Tegeezani, taita Yelusalemu uko Mwana wa Mntu enda ekhiizwe kwa Waviki Wakuu na Wahinyi wa Miko wendao wamuamwiie akomwe na kumwekhiiza kwa wantu wesiho Wayahudi.

34 Naho wenda wambee na kumswiia ovu na kumtoa na koto na kumkoma, akini mwe msi wa ntatu enda ayuyuke.”

*Yakobo na Yohana weegaa ombezo kwa Yesu*
*Matayo 20:20-28*

35 Naho, Yakobo na Yohana wana wa Zebedayo, ne wambasa Yesu na kumwamba, “Mhinyi, takunda utigosoee kintu tendacho tiombeze.”

36 Yesu akawauza, “Mwonda niwagosoee mbwai?”

37 Ne wamtambaisa, “Hada wendaho wekae mwe kigoda chako cha ukuu cha Uzumbe, takunda tekae hamwe nawe, utigosoe kwekaa yumwe phande yako ya kumuso na mtuhu phande yako ya kuume.”

38 Yesu akawamba, “Khammanya ido mdiombezado. Mwadaha kuzizimiza kusuubikaa inga nendavyo nisuubike? Naho mwenda muwe tayali kuuya na nyuma inga nendavyo niuye na nyuma?”

39 Wakamtambaisa, “Tadaha” Yesu akawamba, “Suuba nendazo nipate mwendamzizimize kusuubika kwei, naho kwei mwenda muuye na nyuma inga nendavyo niuye na nyuma mie.

40 Akini khidaha kusagua ni yuhi endae ekae phande ya kuume hambu kumoso kwangu. Ni Muungu ne ahiganyaye yuhi ekae phande ya kuume hambu kumoso kwa wada ekuwasaguao.”

41 Wada wahina watuhu kumi dimwe wekutegeezaho mbui ida wekuombezayo Yakobo na Yohana ne wakimwa.

42 Yesu akawetanga wose na kugombeka, “Mwamanya kuwa wada wamamakhanywao kuwa waongoezi wa si wawagookea wantu wao kwa mdundugo, na wakuu awo wawashuutiza wantu wao.

43 Akini kwenu isekuwa ivyo, iya akundae kuwa mkuu gatigati yenu akundigwa awe mndima yenu.

44 Mntu yoyose akundae kuwa mwoongoezi wa wantu, akundigwa awe mndima wa wose.

45 Kwaviya Mwana wa Mntu khekweza kugosoewa ndima, iya keza kugosoea

wantu ndima na kulavya ugima wakwe kwajii ya kuohoa wantu wangi.”

*Yesu amhonya Batimayo tuntu*
*Matayo 20:29-34; Luka 18:35-43*

46 Naho wakabua Yeliko, Yesu ekuwaho akahauka mwe mzi uwo na wahina wakwe hamwe na zumwezumwe da wantu, tuntu yumwe etangwaye Batimayo mwana wa Timayo ne kekaa khandakhanda ya sia akaombeza.

47 Batimayo ekusikiaho Yesu Mnazaleti emboka hantu aho, ne avoka kukema, “Yesu! Mwana wa Daudi! Nifiie mbazi!”

48 Wantu wangi wakamwakia na kumwamba anyamae, akini ne aendeea kukema, “Mwana wa Daudi, nifiiye mbazi!”

49 Yesu nee kagooka na kugombeka, “Mwetangeni.” Wakamwetanga yuda tuntu, nee wamwamba, “Ekhe moyo! Gooka akwetanga.”

50 Akatambika gwanda dakwe, akahauka kinyinyio na kumbasa Yesu.

51 Yesu ne amuuza, “Wakunda nikugosoee mbwai?” Uyo tuntu akamwamba, “Mhinyi, nakunda nione.”

52 Yesu akamwamba, “Hita kuzumiiya kwako kukuhonya.” Ahoaho akoona, akamtongea Yesu na kuita nae.

# 11

*Yesu engia Yelusalemu kwa nyemi*
*Matayo 21:1-11; Luka 19:28-40; Yohana 12:12-19*

1 Wekuwaho wa hehi na Yelusalemu, hehi ya mizi ya Betifage na Besaniya, kwe muima wa mizaituni. Yesu akawaagiia wahina wakwe waidi.

2 Akawamba, “Hitani mwe mzi wehehi yenu. Mkabua uko mwenda mbwiie mwanaphunda kazengetezwa, naho khazati kugosoewa ndima. Mchopoeni mkamweete.

3 Ati mntu akawauza, ‘Kwambwai mwagosoa ivi?’ Mmwambe, ‘Zumbe amkunda na enda amvuze isasa.’ ”

4 Naho, wakaita, wakambwiiya mwanaphunda siai kafungwa he uvi. Wekuwaho wamchopoa,

5 wamwe wa wantu wekuwaho wagooka aho wakawauza, “Kwambwai mwamchopoa uyo mwanaphunda?”

6 Wahina wakawatambaisa inga viya wekwembigwavyo ni Yesu, naho wakawaeka waite.

7 Wakamwegaiiya Yesu yuda mwanaphunda, wakatandika nguo uwanga ya yuda mwanaphunda, Yesu ne ekaa uwanga yakwe.

8 Wantu wangi watandaza nguo zao siai, watuhu nao watandaza vihuto vya miti wekusengayo mwe minda kwaajii ya kumtogoa.

9 Wantu wose wekuongoao na wada wekuwabasao, wakalavya mgutio wakagombeka, “Zumbe atogolwe! Ajaiwe yuda ezae kwa zina da Zumbe!

10 Ujaiwe Uzumbe wezao wa zumbe Daudi tati yetu! Atogolwe Muungu mwe uko uwanga muno!”

11 Yesu akengia mwe mzi wa Yelusalemu, akaita mwe Nyumba ya Muungu na kukauwa kia kintu. Akini kwaviya ne diswa, akaita mwe mzi wa Besaniya hamwe na wahina wakwe kumi dimwe na waidi.

*Yesu aubadia lazi mti wa mtini*
*Matayo 21:18-19*

12 Msi wekutongeao wekuwaho wakauya kulawa Besaniya, Yesu akaumwa nsaa.

13 Aho kwa hae akaona mti umanyikanao kwa zina da mtini wenye mani mangi, ne aubasa aukaue inga enda apate tini. Ekubuaho akaubwiia khauna tini iya manidu, kwaviya kisingi chakwe cha kuvyaa khakizati kubua.

14 Aho Yesu akawamba mtini, “Kuvokea ivyeo hadi misi zose khahana mntu endae ade tini kulawa kwako vituhu.” Na wahina wakwe wakaitegeeza mbui iyo.

*Yesu engia he Nyumba ya Muungu*
*Matayo 21:12-17; Luka 19:45-48; Yohana 2:13-22*

15 Wakabua mzi wa Yelusalemu, Yesu akengia mwe Nyumba ya Muungu akavoka kuwaguusa wantu wose wekuwaho wakataga na kugua vintu. Akahitua meza za wada wabadiishao hea na kugwisa viti vya wada watagao suwa,

16 khekukunda mntu yoyose kwembokea kwe buha da Nyumba ya Muungu kudoa kintu chochose.

17 Naho ne awahinya, “Igondwa, ‘Nyumba yangu yetangwa Nyumba ya kuvikia kwaajii ya wantu wa si zose!’ Akini nywie muitenda phanga da wahokaji.”

18 Waviki wakuu hamwe na Wahinyi wa Miko, wekutegezavyo mbui izo, wakavoka kuondeza sia ya kumkoma Yesu. Akini wakamuogoha Yesu kwaajii ya wantu wose wekuhondomaao kwa mahinyo yakwe.

19 Ikubuaho guoni, Yesu na wahina wakwe wakahauka mwe mzi uda.

*Mahinyo kulawa mwe mti wa mtini*
*Matayo 21:20-22*

20 Keokeo da mtungaihu, wekuwaho wakemboka ne wauwona uda mtini unyaa wose hadi kwe sina.

21 Petulo akakumbuka akamwamba Yesu, “Mhinyi, kaua uda mtini wekuubadiao lazi, unyaa!”

22 Yesu akatambaisa, "Mzumieni Muungu."
23 Nawamba kwei mntu akawamba muima unu, ng'oka uketambike mwe mazimshindo naye khana matumatu mwe moyo wakwe, akini akazumiia mbui zose agombekazo zagosoka, enda agosoewe mbui iyo.
24 Kwaajii iyo nawagombekani, mvikaho na kuombeza kintu chochose, zumiani kwamba mkihokea, nacho chenda kiwe chenu.
25 Nyie mgookaho kuvika, mwekeeni kia mntu mwekukubanangia chochose, ili Tati yenu mwe uwanga awaekee masa yenu.
26 Akini mwesekuwaekea watuhu, hata Tati yenu mwe uko uwanga kwa Muungu khana awaekee masa yenu.

*Udaho wa Yesu*
*Matayo 21:23-27; Luka 20:1-8*

27 Naho wakabua Yelusalemu vituhu, Yesu ekuwaho akaita he Nyumba ya Muungu, Waviki wakuu na Wahinyi wa Miko na wadaa waongoezi wakambasa,
28 wakamuuza, "Ni kwa udaho uhi wagosoa mbui izi? Naho nndai mwekukwekha udaho wa kugosoa mbui izi?"
29 Yesu akawatambaisa, "Nendaniwauze mbui mwenga, mkanitambaisa nami nendaniwambe nagosoa aya kwa udaho wa ndai.
30 Nigombekani, udaho wa ubatiizo wa Yohana walawa kwa Muungu au walawa kwa wantu?"
31 Wakavoka kuuzana, "Tikamba walawa uko uwanga kwa Muungu endaatiuze, 'Kwambwai khamwekumzumiia Yohana?'
32 Na tikamba, 'Ulawiiya kwa wantu.' " Wakaogoha zumwezumwe da wantu kwaajii wose wamzumiiya Yohana kwei ni muoni wa Muungu.
33 Aho wakamtambaisa Yesu, "Swie khatimanya." Yesu akawamba, "Mie nami khinaniwambe nagosoa mbui izi kwa udaho wa ndai."

# 12

*Msimo wa mnda wa mizabibu na waimi*
*Matayo 21:33-46; Luka 20:9-19*

1 Naho Yesu akavoka kugombeka nao kwa misimo, "Mntu yumwe kaima mnda wa mizabibu akazenga ukanto, na gatigati akagosoa hantu ha kukamuiia divai, akazenga mnaa aho. Naho akauazima uda mnda kwa waimi akatamba kuita si
ya hae." 2 Kisingi cha ubosi chekubuaho,
akamwagiiya mndima wakwe kwa wada waimi, amwetee fungu dakwe da ubosi da yuda mwenye mnda.
3 Wada waimi wakamgwiiya, yuda mndima wakamtoa na kumvuza bue.
4 Mwenye mnda akamwagiiya mndima mtuhu, uyu nae wakamtoa mwe mtwi na kumtenda vyesavyo kutama.
5 Yuda mwenye mnda akamwagiiya mndima mtuhu, awo waimi wakamkoma na mwenye mnda akawaagiiya watuhu wangi, wakatoigwa na wangi wakakomwa.
6 Mwenye mnda akasigaa na mntu yumwe ni mwanawe amkundisae. Nae akamwagiiya uyo akagombeka, "Wenda wamtunye mwanangu!"
7 Akini wada waimi wakaambizana, "Uyo ne mpazi haya timkome, upazi utende wetu."
8 Kwaiyo wakamgwiiya, wakamkoma na kumtambika chongoi ya uda mnda wa mizabibu.
9 Aho Yesu akawauza, "Mwenye mnda endaatende viivihi? Endaeze awadagamize awo waimi na kuazimisha mnda uwo wa mizabibu kwa waimi watuhu.
10 Khamzati kusoma Maandiko aya? 'Iwe dekuemewado na wazengi isasa diwa iwe kuu da khandani.
11 Zumbe ne mwekugosoa mbui inu, nado ni utangio kwetu!' "
12 Waviki wakuu, Wahinyi wa Miko na wadaa wamanya yakuwa msimo uwo wawausu, wakageeza kumgwiya akini wakaogoha zumwezumwe da wantu aho wakambada wakaita.

*Kuiha kodi kwa Seuta mkuu wa Lumi*
*Matayo 22:15-22; Luka 20:20-26*

13 Naho, wamwe wa Mafalisayo na kizumwezumwe cha Helode, wakaagiiwa kwa Yesu wamtege kwa mbui zakwe.
14 Wakambasa Yesu wakamwamba, "Mhinyi tamanya wee ni mntu mzumizi, ugombekaye ukwei. Naho khukauwa ukuu wa mntu yoyose, akini wahinya kwei sia ya Muungu. Ni vyedi kuiha kodi kwa Seuta mkuu wa Lumi? Tiihe hambu tesekuiha?"
15 Akini Yesu ne amanya uhokho wao. Akawatambaisa, "Kwa mbwai mwanigeeza? Nekhani sensi niikauwe."
16 Wakamwegaiya sensi mwenga ne awauza, "Cheni na idi zina ni da ndai?" Ne wamtambaisa, "Ni vya Seuta mkuu wa Lumi."
10 Kwaviya Iyandikwa, endaawaagiiye Wandima wa uko uwanga kwa Muungu wakuinde,
11 vituhu, "Wendawakudoe mwe mikono yao, usekweza kwekungwaa muundi mwe iwe."
12 Akini Yesu akamtambaisa, "Iyandikwa, 'Usekumgeeza Zumbe Muungu yako.' "
13 Ibiisi ekubindaho kumgeeza kwa kiya sia, akambada kwa kisingi.

*Yesu avoka ndima yakwe uko Galilaya*
*Matayo 4:12-17; Maliko 1:14-15*

14 Aho Yesu akauya Galilaya, kamema udaho wa Muye wa Muungu, na mbui zakwe zikaambazika kiya hantu hehi ya mzi uda.
15 Naye nee akawahinya wantu mwe Nyumba za kukintania Wayahudi, na kiya yumwe akamtogoa.

*Yesu aemewa uko Nazaleti*
*Matayo 13:53-58; Maliko 6:1-6*

16 Viyaviya, Yesu akaita Nazaleti hantu ekueewaho, na Msi wa Kuhumwiza akengiya mwe Nyumba ya kukintania Wayahudi inga yekuwavyo mazweeya yakwe. Akagooka asome Maandiko ya Muungu kwa mgutio.
17 Akahokea kitabu cha Muoni Isaya, akakigubua na akabwiiya hantu hekuandikwaho,
18 "Muye wa Zumbe uhamwe nami,
Kwaviya kanisagua niwabikiiye, wakiwa Mbui Yedi.
Kaniagiiya niwabiikiye wada wekufungwao, mbui ya kuvugwiiwa kwao,
Na wada mantuntu wadahe kukauwa vituhu
Na kaniagiiya niwaohoe wasuumizwao,
19 Na kubiikiya kisingi kibua,
Zumbe eza kuwaohoa wantu wakwe."
20 Naho akakigubika kiya kitabu, akamwekha mndima, naho akekaa. Wantu wose wekuwao mwe Nyumba ya kukintania Wayahudi nee wamfwiiya meso.
21 Naho akavoka kuwamba, "Maandiko ya Muungu aya mwekutegeezayo yaigania ivyeo."
22 Wose wakatamiwa naye, wakahondomaa kwa mbui ntana ekugombekazo. Wakauzana, "Huyu khio mwana wa Yusufu?"
23 Naye akawamba, haika mwendamnigombeke mtamwiiyo unu, "Mganga ehonye mwenye. Vituhu mwendamgombeke, 'Yose tekuyategeezayo kuyagosoa kuda Kapelinaumu, yagosoe hanuhanu mwe mzi wako.' "
24 Akaendeea kutamwiiya, "Nawamba kwei, khahana Muoni mzumiiwa mwe mzi wakwe."
25 Akini tegeezani! Kwei, kuwa na wavyee wangi wekufiiwao ni wagosi mwe si ya Isilaeli kisingi cha Eliya. Uwanga kwekufungwaho, kisingi icho fua iyeka kunya kwa kisingi cha myaka mitatu na miongo mtandatu, nekuwa na saa khai mwe si yose.
26 Ivyo Eliya khekuagiiwa kwa mntu yoyose wa Isilaeli, iya kwa mvyee yumwe ekufiiwaye ni mgosi wa Salepta mwe si ya Sidoni.
27 Naho, mwe si ya Isilaeli kisingi cha Muoni Elisha nekuwa na wenye utamu wa nyoka wangi, akini khahana yoyose ekusuntwaye iya Naamani mwenyezi wa si ya Shamu.
28 Wose wekuwao mwe ida Nyumba ya kukintania Wayahudi wekusikiaho ayo nee wakimwa muno.
29 Wakagooka wakamlavya chongoi ya mzi wao wekuzengwao uwanga ya muima, wakamwegaa hadi mwe kisiikizi cha muima wamwase asi.
30 Akini Yesu akemboka ahoaho gatigati ya zumwezumwe da wantu akaita.

*Mntu mwenye zaiko*
*Maliko 1:21-28*

31 Naho Yesu akaseeya Kapelinaumu,
mwe mzi wa Galilaya, nee akahinya wantu
Msi wa Kuhumwiza.
32 Wakahondomaa muno kwa mahinyo
yakwe, kwaviya nee akahinya kwa udaho.
33 Na mwe ida nyumba ya kukinta-
nia Wayahudi nekuwa na mntu ekuwaye
mwekukwewa na zaiko fyaimi, akatoa
vuzo kuu.
34 “Una mbwai na swie, wee Yesu wa
Nazaleti? Kweza kutidagamiza? Naku-
manya undai. Weye ni Mng'azi wa
Muungu.”
35 Yesu akadiwakiya ido zaiko fyaimi
akadigombeka, “Nyamaa na umlawe mntu
uyu!” Yuda zaiko akamgwisa yuda mntu
asi hemeso yao wose, akamlawa kwesao
kumuumiza hantu.
36 Wantu wose wakahondomaa, nee
waambizana, “Inu ni mbui yevivihi,
kwaviya kwa udaho na nguvu agombeka
mazaiko walawe, nao walawa!”
37 Mbui zakwe Yesu zikavoka kuam-
bazika kiya hantu mwe si ida.

*Yesu awahonya wantu wangi*
*Matayo 8:14-17; Maliko 1:29-34*

38 Yesu nealawa mwe ida Nyumba ya
kukintania Wayahudi akaita kaya kwa Si-
moni. Mvyee yumwe, mkwewe da Si-
moni nekawa na bombom khai, wakam-
wombeza amhonye
39 Yesu akeza akagooka hehi
naye akawakia diya bombom, nado
dikamwekea. Yuda mvyee akenuka
ahoaho, kuwembikia khande.
40 Zuwa dekuswaho, wose wekuwao
na watamu wao mbaimbai nee wegalwa
kwakwe, naye akawadonta kwa mikono
yakwe, akawahonya.
41 Mazaiko nee yawalawa wantu
wangi wakatoa vuzo wakagombeka,
“Wee ni Mwana wa Muungu!” Akini
Yesu akawawakia, naho khekukunda
wagombeke, kwa viya wammanya yee nee
Klistu.

*Yesu abiikia uko Uyahudi*
*Maliko 1:35-39*

42 Kioi dakwe keo, Yesu akahauka
akaita hantu heikedu. Wantu wawa
wakamwondeza. Awo wantu wekubuaho
hantu ekuwaho, wakageeza kumuemeza
asekuhauka kwao.
43 Akini yee akawamba, “Nakundigwa
kubiikia Mbui Yedi za Useuta wa Muungu
mwe mizi mituhu, kwaviya khiagiiwa
kwaajii iyo.”
44 Nekawa abiikia mwe Nyumba za kuk-
intania Wayahudi mwe mzi wa Yudea.

# 5

*Yesu awetanga wahinyi wa bosi*
*Matayo 4:18-22; Maliko 1:16-20*

1 Msi umwe, Yesu ekuwaho kagooka
khandakhanda ya tondoo da mazi ya Gene-
saleti, na wantu wangi newamzunguuka
uku wakefintafinta, wategeeza mbui ya
Muungu.
2 Akoona ngaawa mbii khandakhanda
ya tondoo da mazi. Walowa wa samaki
newalawa, wasunta nyavu zao.
3 Yesu akengia mwe ngaawa mwenga
yekuwayo ya Simoni, nee amuombeza
Simoni aisogeze mwe tondoo da
mazi kulawa mpwani, Yesu akahinya
zumwezumwe da wantu uku kekaa mwe
ngaawa.
4 Ekubindaho kuhinya, akamwamba
Simoni, “Yegae ngaawa adi mwekiindi,
mkazitambike nyavu mdahe kulowa
samaki.”
5 Simoni akamtambaisa, “Zumbe titenda
ivyo kio kigima khatokuambua kintu, akini
kwaviya kugombeka, nenda nizitambike
nyavu.”
6 Ekubindaho kugosoa ivyo, wakalowa
samaki wangi, ivyo nyavu zao zikavoka
kudumuka.
7 Wakawetanga wezwao wekuwao
mwe ngaawa ntuhu weze kuwaambiza.
Wakeza, wakamemeeza ngaawa zose mbii
samaki, zikawa hehi na kuzama.
8 Simoni Petulo ekuonaho ayo, akakinta
mavindi hemeso ya Yesu akamba, “Hauke
he meso yangu ee Zumbe, kwaviya mie ni
mwenye mavigaviga!”
9 Simoni hamwe na weziwe wose waka-
hondomaa kwa ugenyezi wa samaki wangi
viya.
10 Viyaviya Yakobo na Yohana, wana wa
Zebedayo wekuwao walowa wa samaki
weziwe Simoni, Yesu akamwamba Simoni,
“Usekuogoha kuvokea isasa wendauwe
mlowa wa wantu.”
11 Naho, bada ya kuzieta zia ngaawa
mpwani, wakabada vyose wakamtongea.

*Yesu amhonya mntu mwenye utamu nyoka*
*Matayo 8:1-4; Maliko 1:40-45*

12 Aho Yesu ekuwaho mwe mzi umwe-
wao, mntu yumwe mwenye utamu wa
nyoka mwii mgima Yesu akamwona. Naho,
mntu uyo akagonea ifu akamwombeza
Yesu, “Zumbe, ukakunda wadaha kun-
ing'aza!”
13 Yesu akenua mkono, akamdonta na
kugombeka, “Nakunda, ng'azika!” Ahoaho
akahona utamu wa nyoka.
14 Yesu akamwagiiya akamwamba,
“Usekumwamba mntu yoyose mbui izi,
iya hita mwenga kwa mwenga kwa Mviki,

ukalavye lavyo kwa Mviki inga Musa
ekuagiiavyo na kuwa uvuhuzi kwa wantu
wose kuwa kusuntwa."
15 Akini mbui za Yesu zikaendeeya kuam-
bazika kiya hantu. Mazumwezumwe
mangi ya wantu wakakintana kumtegeeza
na kuhonywa matamu yao.
16 Akini yee akaita hantu hesahokuwa na
wantu uko akavika.

*Yesu amhonya mntu mwekuhoowa*
*Matayo 9:1-8; Maliko 2:1-12*

17 Msi umwe, Yesu nekawa akahinya.
Mafalisayo na Wahinya wa Miagiiyo ku-
lawa mwe kiya mzi wa Galilaya na Yudea
na Yelusalemu, newekaa aho. Udaho wa
Zumbe ne uwa hamwe naye kwaajii ya
kuhonya watamu.
18 Ahoaho wantu wakeza, wamwenua
mntu yumwe mwekuhoowa mwii, kagona
mwe usazi wakageeza kumwengiza ndani,
wamwiike hemeso ya Yesu.
19 Kwaajii ya zumwezumwe da wantu
dekumemado, khawokudaha kubua
hehi na Yesu. Ivyo wakabovoa hantu
ha chusi yekuwayo uwanga ya hantu
ekuwaho Yesu, nee waseeza javi da
yuda mwekuhoowa. 20 Yesu ekuon-
aho wekuwavyo na uzumizi mkuu,
akamwamba mntu uyo, "Mmbuya
kuekewa mavigaviga yako."
21 Wahinya wa Miagiiyo na Mafalisayo
wakavoka kweuza wenye, "Nindai uyu
atamwiaye mbui zakufuu? Khahana mntu
adahae kuekea mavigaviga iya Muungu
ikedu!"
22 Yesu akawamanya mamakhanyo zao,
akawauza, "Mwamamakhanya mbwai
mwe mioyo yenu?
23 Ni dihi dekuhuhado muno Ku-
gombeka, 'Kuekewa mavigaviga,' hambu
kugombeka, 'Gooka, uite?'
24 Naho nakunda mmanye kwaviya
Mwana wa Mntu ana udaho wa kuekea
wantu mavigaviga mwe inusi." Aho
akamwamba uyo mwekuhoowa, "Gooka,
doa javi dako, uite kaya."
25 Ahoaho uyo mntu mwekuhoowa ak-
agooka hemeso ya wose, akadoa usazi
wakwe akaita kaya kwake uku amtogoa
Muungu.
26 Wose wakatozwa na umako na
kwengiwa ni maatu, nee wamtogoa
Muungu wakagombeka, "Ivyeo tiona
ntangio."

*Yesu amwetanga Lawi*
*Matayo 9:9-13; Maliko 2:13-17*

27 Yekwembokaho ayo, Yesu akalawa
chongoi akamwona mtoza kodi yumwe
etangwaye Lawi, kekaa hantu hakwe haku-
doea kodi. Yesu akamwamba, "Nitongea"
28 Naye akavibada vyose akamtongea.
29 Naho Lawi akamgosoeya Yesu ntafuno
mwe nyumba yakwe, na zumwezumwe
kuu dawatoza kodi na wantu wangi wawa
wekaa hamwe nae.
30 Akini Mafalisayo na Wahinyi wa mi-
agiiyo wakawa wawang'ung'uzikia wahina
wakwe na kuwamba, "Kwa mbwai mwada
na kudomea na watozao kodi na wenao
mavigaviga?"
31 Yesu akawatambaisa, "Wenye mii mi-
tana khawakunda mganga, wamkundao ni
wada wekuwao watamu.
32 Nchekweza kuwetanga wantu wedi,
iya wenye mavigaviga, wadahe kuhituka."

*Mbui ya kwehiniza kuda*
*Matayo 9:14-17; Maliko 2:18-22*

33 Wantu watuhu wakamwamba,
"Wandima wa Yohana mbatiiza wehiniza
kuda kiya maa na kuvika, na wandima
wa Mafalisayo wagosoa ivyoivyo. Akini
wahina wako wada na kudomea."
34 Yesu akawatambaisa, "Wada wagonek-
wao mwe ndoza khawakundigwa kwe-
hiniza kuda kwaviya Zumbe wa ndoza yu
hamwe nao?"
35 Akini kisingi chendakibue ambaho
Zumbe wa ndoza* enda ausigwe gatigati
yao, kisingi icho nee wendaho wehinize
kuda.
36 Yesu akawamba msimo unu, "Khahana
mntu asengae kilaka mwe gwanda dihya
na kuika mwe gwanda dekusakaado, inga
akatenda ivyo endaawe kasenga ido dihya,
na kida kilaka cha gwanda dihya khakina
chendane na ido gwanda dekusakaado.
37 Naho wantu khawageya divai mphya
mwe mikwiji ya babu yekusakaayo, inga
akatenda ivyo iyo divai mphya yendaitatue
iyo mikwiji ya babu na divai yendayetike
na mikwiji iyo yendaibanike.
38 Divai mphya yagewa mwe mikwiji ya
babu mihya.
39 Khahana mntu atamiwaye kudomea
divai mphya bada ya kudomea divai ya
kae kwa kugombeka 'Ida ya kae ni ntana
muno.' "

# 6

*Yesu nee Zumbe wa Msi wa Kuhumuiza*
*Matayo 12:1-8; Maliko 2:23-28*

1 Msi umwe wa kuhumwiza, Yesu
nekawa akemboka mwe minda ya
uhemba, na wahina wakwe waka-
voka kusenga masuke ya uhemba na
kuyahugusua mwe mikono yao na kuda.

* **5:35 5:35** Zumbe wa ndoza yaonyesha ni Yesu

2 Wamwe wa Mafalisayo wakawauza
wahina, “Kwa mbwai mwagosoa
yesayokukundigwa Msi wa Kuhumwiza?”
3 Yesu akawatambaisa, “Khamkusoma
viya ekugosoavyo Daudi hamwe na wen-
ziwe wekuwaho na saa?
4 Daudi nee engiya mwe Nyumba
ya Muungu, akadoa yada mabumunda
yekuikwayo hemeso ya Muungu akada na
kuwekha wenziwe. Na khayokukundigwa
mntu yoyose kuda mabumunda ayo, iya
Waviki wowodu.”
5 Yesu akawamba, “Miye mwana wa
Mntu nee Zumbe wa Msi wa Kuhumwiza.”

*Yesu ahonya mntu mwekuhoowa mkono*

*Matayo 12:9-14; Maliko 3:1-6*

6 Msi mtuhu wa Kuhumwiza, Yesu neen-
gia mwe Nyumba ya kukintania Wayahudi,
nee awahinya. Mwe nyumba iyo, nekuwa
na mntu ambae mkono wakwe wa kuume
neuwa uhooa.
7 Wahinya wa miagiiyo ya Muungu na
Mafalisayo nee wakoondeza kumkoeya
masa Yesu, ivyo wakamkauwa kwa hehi ati
endaahonye Msi wa Kuhumwiza.
8 Akini Yesu akamanya mamakhanyi zao,
akamwamba yuda mwe mkono wekuhoao,
“Enuka, gooka gatigati yao.” Yuda mntu
akagooka gatigati yao.
9 Naho Yesu akawamba wada Wahinyi
wa miagiiyo na Mafalisayo akagombeka,
“Nawauza nywie, kulawana na miagi-
iyo yetu ni dihi tana kugosoa msi wa
kuhumwiza, kugosoa mbui ntana hambu
kugosoa mbui ya ufyaimi? Kuohoa ugima
hambu kuyadagamiza?”
10 Akawafuiya meso phande zose,
akamwamba yuda mntu, “Enua mkono
wako.” Akawenua mkono wakwe ukawa
mgima vituhu.
11 Wada wakuu wakakimwa muno,
wakeambizana wowo kwa wowo, ni viivihi
wendacho wamgoswee Yesu.

*Yesu asagua Wagiiwa kumi dimwe na waidi*

*Matayo 10:1-4; Maliko 3:13-19*

12 Msi umwe Yesu akaita kwe muima
kuvika, akacheeza uko kiyo kigima
akamvikia Muungu.
13 Kwekuchaho akawetanga wahina
wakwe, nae akasagua kumi dimwe na
waidi nee awetanga wagiiwa,
14 Simoni, yuda Yesu ekumwekhaye zina
da Petulo na Andulea nduguye na Yakobo
na Yohana na Fiipo na Batolomayo,
15 Matayo na Tomaso na Yakobo wana wa
Alifayo na Simoni ekwetangwaye Zelote
mntu mwekuwa mvunizi wa si yakwe,
16 Yuda mwana Yakobo na Yuda Isikalioti
yuda mwe kumhituka Yesu.

*Yesu ahinya na kuwahonya wantu*

*Matayo 4:23-25*

17 Yesu ekuseeaho kwe muima hamwe
na waagiiwa wakwe, Yesu akagooka hantu
ekuwaho tambalale. Aho nekuwa na
zumwezumwe kuu da wahina wakwe
na zumwezumwe da wantu wekulawao
phande zose za si ya Yudea na mzi wa
Yelusalemu na mpwani ya mizi ya Tilo na
Sidoni,
18 Wose wakabua kumtegeeza Yesu na
kuhonywa matamu yao. Nee awahonya
wose wekuwao na mazaiko.
19 Wantu wose newakunda kumdonta,
kwajii ya udaho wekulawao kwakwe na
kuwahonya wose.

*Kinyemi na usungu*

*Matayo 5:1-12*

20 Yesu akawahitukia wahina wakwe,
akamba,
“Mjaiwa nywie wakiwa, kwaviya
Useuta wa Muungu ni wenu!
21 Mjaiwa nywie mwenao saa isasa,
Kwa viya msi weza mwendamweguswe,
Mjaiwa nywie mwiiyao isasa,
Kwaviya misi yezayo mwendamseke kwa
kinyemi.
22 “Mjaiwa nywie wantu wenda-
howawakimwe, na kuwabahuwa, wen-
dawawadumue, na kuwabanangia zina
kwaajii ya Mwana wa Mntu.
23 Aho kae wadaa wenu wagosoa ivy-
oivyo kwa waoni wa Muungu ivyo yen-
dahoyalawiie kuwani na nyemi na kuvina
kwaviya funge yenu ni khuu huko uwanga
kwa Muungu.
24 Akini mmbwii yenu nywie mwenao
vintu vingi.
Kwaviya mbinda kwekhigwa kae nyemi
yenu.
25 Mmbwii yenu nywie mwegutao isasa,
Kwaviya misi yeza mwendamuwe nasaa.
Mmbwii yenu nywie msekao kwa kinyemi
isasa,
Kwaviya misi yeza mwendamuomboleze
na kuiya.
26 “Mmbwii yenu nywie hada wantu
wose wanitogoao, kwaviya wadaa wao
wawagosweeya waoni wa uwokho ivy-
oivyo.

*Kuwakunda wamasa*

*Matayo 5:38-48; 7:12*

27 “Akini nawagombekea nywie
mnitegeezao, wakundiseni wamasa wenu,
wagosweeni vyedi wada wamikimao.
28 Wajaiyeni wada wawabadiao lazi, na
wavikieni wada wamigosweeyao ufyaimi.
29 Mntu akakutoa funda dimwe mhituiye
dakaidi. Mntu akakuhoka gwanda dako
mbadie na shati dako viyaviya.

30 Mntu akakuombeza kintu mwekhe, na mntu akakuhoka vintu vyako vyose usekukunda akuvuzie.

31 Mkundavyo wantu wawagoswee nywie, wagosweeni ivyoivyo.

32 “Na mkawa mwawakundisa wada wawakundao nywie, ivi, mwenda mpate funge dani? Kwaviya hata wenye mavigaviga wawakunda wada wawakundao wowo.

33 Naho, inga mkawagosweeya mbui ntana, wada du wawagosweeyao matana, mwenda mpate funge dani kwaviya wenao mavigaviga wagosoa ivyoivyo.

34 Naho inga mkawekha wada du mkauwiyao wendawamiihe, ivi mwenda mpate funge dani? Hata wenao mavigaviga wawekha wenye mavigaviga wezwao ili wawavuzie kihimo kiyakiya.

35 Iya nywie wakundiseni wamasa wenu na kuwagosoea mbui ntana, wekheni msekukauwiya kuvuziwa. Naho funge yenu yendaiwe khuu, nanywi mwenda muwe wana wa Muungu mwe uko uwanga kwa Muungu. Kwaviya yee ni mng'azi kwa wada wesao ntogoo na wafyaimu.

36 Kuwani na mbazi inga Tate yenu ekuwavyo na mbazi.

*Kuwekha sugusa watuhu*
*Matayo 7:1-5*

37 “Msekuwekha sugusa watuhu, na nywie mwenda mwekhigwe sugusa, msekuwalaumu watuhu, na nywie khamna mlaumiwe, waekeni watuhu, nanyi mwenda muekewe.

38 Wekheni watuhu vintu, nanyi mwendamwekhigwe. Eehe, mwendamhokee he mikono yenu kihimo chekumemacho, na kuomoewa na kwetika etika. Kwaviya kihimo kiyakiya muhimiacho kwa watuhu nee endachoahimie Muungu kwenu.”

39 Yesu akawamba msimo unu akawauza, “Ivi tuntu adaha kumuongweeya tuntu mweziwe?. Eehe wose waidi wenda wengie mwe tubwi”

40 Mhina khamwemboka mhinyi wakwe, akini kiya mhina akabinda kuhinywa awa inga mhinyi wakwe.

41 “Kwa mbwai waona kibasi mwe ziso danduguyo na ahoaho khuona basi mwe sizo dako?

42 Wadaha viivihi kumwamba nduguyo, ‘Ndugu, goja nikuuse kibasi mwe ziso dako,’ na uku khuona basi mwe ziso dako mwenye? Mbakha weye! Voka kulavya basi deumo mwe ziso dako, na aho nendiho wendaho uwone vitana na kudaha kuusa basi dekuwado mwe ziso da nduguyo.”

*Mti na matunda yakwe*
*Matayo 7:16-20; 12:33-35*

43 “Mti mtana khauvyaa matunda yesayo kutama, naho mti wesao kutama khauvyaa matunda yatamayo,

44 kiya mti wamanyika kwa matunda yakwe. Kwaviya wantu khawatunda tini mwe misongoma wala zabibu mwe miwa.”

45 Mntu mtana alavya matana kulawa mwe moyo wakwe na mntu mfyaimi hulavya yesayo kutama mwe moyo wakwe, kwaviya mntu ugombeka kulawana na yada yekumemayo mwe moyo wakwe.

*Wazengi waidi*
*Matayo 7:24-27*

46 “Kwambwai mwanetanga, ‘Zumbe, Zumbe’, na uku khamgosoa yada nigombekayo?

47 Nendaniwaonyeshe ni viivihi eivyo mntu yuda ezae kwangu na kutegeeza mbui zangu na kuzigosoa.

48 Uyo aigana na mntu azengaye nyumba, mwekufuka asi na kuika msingi wakwe uwanga ya iwe na yakalawiiya mafuiko ya zigizigi da mazi, mfeeji wa mazi ukaitoa ida nyumba, iya khaidaha kusingisika, kwaajii nee iwa izengwa vyedi.

49 Akini yoyose ategeezaye mbui zangu na akesekugosoa chochose, uyo aigana na mntu ekuzengaye nyumba uwanga ya msanga kwesiho kuika msingi. Mafuiko ya zigizigi da mazi neyalawiiya, mfeeji wa mazi ukaitoa nyumba ida, ikagwa na kubanika na kubondekabondeka.”

# 7

*Yesu amhonya mndima wa mkuu wa Lumi*
*Matayo 8:5-13*

1 Yesu ekubindaho kugombeka mbui yedi kwa wantu, akengia mzi wa Kapelinaumu.

2 Uko nekuwa na mkuu yumwe wa asikai wa Kilumi neekawa na mndima wakwe, neakamkundisa muno. Uyu mndima nekawa mtamu hehi na kuuya na nyuma.

3 Mkuu wa asikai wa Lumi ekusikiaho mbui za Yesu, neawaagiiya wadaa wa Kiyahudi, wakamwombeze eze amhonye mndima uyo wa mkuu wa Lumi.

4 Wekubuwaho kwa Yesu, ne wamhembeeza muno, wakamba, “Mntu huyu afaa kuambizwa,

5 kwaajii yee aikundisa si yetu, na nee mwekutizengea ida Nyumba ya kukintania Wayahudi.”

6 Naho, Yesu akaita hamwe nao. Ekuwaho hehi na kubua kwe nyumba ya yuda mkuu wa maasikai, yuda mkuu wa masikai wa Lumi akawaagiiya wambuya wakwe wamwambe Yesu, “Zumbe, usekwepisha muno, kwaviya

miye khifaa weye wengie mwe nyumba
yangu.
7 Naho miye nchekweona inga nafaa
kweza kwako. Akini gombeka mbui du, na
mndima yangu enda ahone.
8 Kwamana hata miye uwanga yangu
kuna wagookezi, na nenao asikai asi
yangu. Nikamwamba yumwe 'Hita,' naye
aita, nikamwamba mtuhu 'Soo,' naye eza.
Nikamwamba mndima yangu,, 'Gosoa idi'
nae agosoa."
9 Yesu ekusikiaho mbui iyo akahondo-
maa, naho akahitukia diya zumwezumwe
da wantu wekuwao wamuondeza akamba,
"Nchekuona mwenye uzumizi inga unu
mwe wantu wose wa Isilaeli."
10 Naho wada wantu wekuwao waagiiwa
kwa Yesu wekuuyaho kaya nee wambwiiya
yuda mndima kahona.

*Yesu amyuyusa mwana wa mvyee ekufi-
iwaye ni mgosi*

11 Kisingi kwemboka, Yesu akaita mwe
mzi umwe wetangwao Naini. Na wahina
wakwe na zumwezumwe kuu da wantu
wakaita hamwe naye.
12 Naho, ekuwaho yu hehi na uvi mkuu
wa mzi, wakalawiiya wantu wenua ki-
imba cha mwana kigosi yumwe, mwana
wa ikedu wa mvyee mwekufiiwa ni mgosi.
Wantu wangi wa mzi uda neswawa hamwe
na uyo mvyee.
13 Zumbe Yesu ekumwonaho mvyee uyo
akamfiiya mbazi, akamwamba, "Usekui-
iya."
14 Naho akatimia hehi akadidonta
diya tusi, na wada wekuwao wadenua
wakagooka. Yesu akamba, "Mbwanga,
nakwamba enuka."
15 Yuda Mbwanga ekuyae na nyuma ak-
enuka na kwekaa, akavoka kutamwiiya.
Na Yesu akamwegaa yuda mwana kwa
mami yakwe.
16 Wantu wose wakaogoha muno na
kumtogoa Muungu na kugombeka, "Muoni
wa Muungu mkuu kalawiiya gatigati yetu.
Muungu keza kuwaohowa wantu wakwe."
17 Mbui izo ekuzigosoazo Yesu zikaam-
bazika kose mwe si ya Yudea na mizi yose
ya hehi.

*Wahina kulawa kwa Yohana Mbatiiza*
*Matayo 11:2-19*

18 Wahina wa Yohana Mbatiiza
wakamwamba Yohana mbui izo zose
ekugosoazo Yesu. Nee Yohana awetanga
wahina wakwe waidi,
19 nee awagiiya kwa Zumbe Yesu
wamuuze, "Wee nee yuda tekuwaye
tikamkauwia, hambu tigoje mtuhu?"
20 Wada wahina wekumbwiiyaho
Yesu wakamwamba, "Yohana mbatiiza
katiagiiya kwako tikuuze, 'Wee nee yuda
mwekuwa tikamkauwia, hambu tigoje
mtuhu?' "
21 Kisingi ichoicho, Yesu nee ahonya
wantu wangi wekuwao wasuumizwa ni
matamu na wekukwewao na mazaiko na
matuntu wangi wakadaha kuona.
22 Ivyo Yesu akawatambaisa, "Hi-
tani mkamwambe Yohana yada yose
mwekuyaonayo na kuyategeeza, matuntu
waona, wekuviao miundi wenda,
wenye utamu wa nyoka wang'azika,
viziba wasikiya, wekuuyao na nyuma
wayuyuswa, na wakiwa wabiikiwa Mbui
Yedi."
23 Kajaiwa mntu yuda ambae khana ma-
tumatu nami.
24 Wahina wa Yohana Mbatiiza
wekuhaukaho, Yesu akavoka kugombeka
na diya zumwezumwe da wantu mbui
za Yohana Mbatiiza, "Mwekuitaho kwe
kiwawe mwona mbwai? Nee ni inde
dikasingiswa nkhusi?
25 Hambu mwita kukauwa mbwai?
Nee mwita kumkauwa mntu mwe kuvaa
gwanda ntana? Manyeni kuwa wavaao
magwanda ya hea nyingi na kwekaa
wekazi wa ntunyo na makwasukwasu
wekaa mwe mazumba ya maseuta.
26 Naho nambiani, mwita koona mbwai?
Nee mwita kumwona Muoni wa Muungu?
Eehe, nkwei akini yee mwekumuonaye
kembokesa Muoni.
27 Mwe Maandiko matana Muungu
atamwiiya uwanga ya Yohana
akamwamba, 'Yesu kuwa namuagiiya
mndima yangu Yohana akuongwee na
kukuikia vitana sia yako.' "
28 Yesu akabiindizia kwa kugombeka,
"Nawamba, mwe wantu wekwekaisao
mwe inusi khahana ekuwaye mkuu
kusima Yohana Mbatiiza. Na ivyo, yuda
ekuwaye mdodo mwe Useuta wa Muungu
ni mkuu kusima yee."
29 Wantu wose wekusikiaho ayo na wa-
toza kodi nee watogoa wedi wa Muungu,
aho nee wada wekuwao wauhokea ubati-
izo wa Yohana.
30 Akini Mafalisayo na wahinyi wa mi-
agiiyo newaemea nteganyi ya Muungu
yekukundigwayo wakaemea kubatiizwa ni
Yohana.
31 Yesu akaendeea kugombeka, "Naho,
nendaniwaiganize wantu wa kivyazi iki na
kintu chani? Ni wantu wa namna yani?
32 Ni inga wabwanga wekwekao
gwiiyo na kwambizana, kizumwezumwe
kimwe na kituhu, 'Tiwatoea fiimbi wala
khamwekuvina, titoa wiya wa bwaimbwo
wala kamwekuiya'
33 Kwaviya Yohana mbatiiza keza, ake-
hiniza kuda na khekudomea divai, nanywi
mkamba, 'Kakwewa ni mazaiko!'

[34] Mwana wa Mntu keza, ada na kudomea, nanywi mwamba, 'Mkauweni uyu ni mmeo na mkozi, ni mmbuya wa watoza kodi na wenye mavigaviga!'
[35] Na ivyo, umanyi wa Muungu yamanyika kuwa ni ntana kwa wantu wose waizumiiyao."

*Yesu mwe nyumba ya Simoni Mfalisayo*

[36] Mfalisayo yumwe nee kamgoneka Yesu kuda khande mwe nyumba yakwe. Na Yesu akengia mwe nyumba ya uyo Mfalisayo, na akekaa kuda khande.
[37] Naho mwe mzi uda nekuwa na mvyee yumwe mwekuwa na mavigaviga. Ekusikiaho Yesu yuuko mwe nyumba ya uyo Mfalisayo, akadoa nchupa yekugosolwayo na iwe detegwado alabasta yekumemezwayo mavuta matana ya hea nyingi.
[38] Akeza, akagooka hehi ya miundi ya Yesu, akaiya na mesozi yakwe yakamwetikiya Yesu mwe miundi. Uyo mvyee akaihangusa miundi ya Yesu kwa fii zakwe. Naho akaiyumbatia na kuihaka yada mavuta matana.
[39] Mfalisayo yuda ekumgonekae Yesu ekuonaho ayo, akamamaakhanya mwe moyo wakwe, "Inga mntu uyu nee ni muoni wa Muungu wa kwei nee kamanya mvyee uyu niwa viivihi, ni mwenye mavigaviga."
[40] Yesu akamwamba uyo Mfalisayo, "Simoni, nna mbui ya kukugombeka."
Naye Simoni akamwamba, "Eehe! Mhinyi, nigombeka."
[41] "Wantu waidi newawa wamkopa mntu hea. Yumwe nee kamwekha vintii vya madini ya feza mia shano, na mtuhu vintii vya madini vya feza elufu shano.
[42] Wekuvotwaho kuiha madeni yao. Uyo mntu wakaekewas wose waidi. Isasa ni yuhi gati ya aho waidi enda amkundise muno zumbe?"
[43] Simoni akamtambaisa, "Ni kwei yuda ekuekeewaye deni kuu endaamkundise yuda zumbe."
Yesu akamwamba, "Ni kwei."
[44] Naho akamhitukia yuda mvyee na kumwamba Simoni, "Wamwona mvyee uyu? Aho miye nekwengiaho hanu he nyumba yako khwekunekha mazi ya kusunta miundi yangu, akini mvyee uyu kanisunta miundi yangu kwa mesozi yakwe na kunihangusa kwa fii zakwe.
[45] Wee khwekuniugusa kwa kuniumbatia, akini mvyee uyu kuvokea nekwengiaho hanu kawa akaumbatia miundi yangu.
[46] Wee khwekunionyesha untana wako kwa kunihaka mavuta ya mzaituni mwe mtwi, akini uyu mvyee katenda ivyo kwa kunihaka mavuta matana mwe miundi yangu.
[47] Kwa iyo nakwamba kaekewa mavigaviga yakwe kwaviya kaonesha ukundiso mkuu. Mwenye kuekewa vidodo mavigaviga, kakundisa vidodo."
[48] Aho, Yesu akamwamba yuda mvyee, "Kuekewa mavigaviga yako."
[49] Naho wada wekuwaaho wekaa hamwe wakauzana, "Ni ndai uyu adahaye kuekea mavigaviga?"
[50] Naye Yesu akamwamba yuda mvyee, "Uzumizi wako ukuohowa, hita kwa uivanisa."

# 8

*Wavyee wekutongeanao na Yesu*

[1] Yekwembokaho ayo, Yesu nee kemboka mwe mizi na mizi akabiikia Mbui Yedi za Useuta wa Muungu. Wada wahina kumi dimwe na waidi wakatongeana naye.
[2] Hamwe na wavyee watuhu Yesu ekuwalavyao mazaiko na kuwahonya matamu, wakatongeana naye. Awo nee wakina Malia mwekwetangwae Magidalene, mwe kuavigwa mazaiko mfungate,
[3] Yoana na mkaza Kuza, mndima mkuu wa Helode na Susana na wavyee watuhu. Awo wavyee nee wakamgosweeya ndima kwa vintu vyao vyose Yesu hamwe na wahina wakwe.

*Msimo wa mntu mhanda mbeyu*
*Matayo 13:1-9; Maliko 4:1-9*

[4] Kisingi kimwe zumwezumwe kuu da wantu nediwa dakintana, na wantu nee wamwezea Yesu kulawa kwe kiya mzi. Na Yesu akawamba msimo unu.
[5] "Mhasi kenda kuhanda mbeyu zakwe. Ekuwaho aketia mbeyu ntuhu zikagwa mwe sia, na wemboka sia wakazijata na wadege wa uwanga wakazida.
[6] Ntuhu zikagwa mwe uongo wekuwao na maiwe, na zekuhotao zikanyaa kwaajii ya kwesekuwa na uwisiuwisi.
[7] Mbeyu ntuhu zikagwa kwe miti ya misongoma, na ida miti ya miwa yekuhotaho hamwe nazo nakuzifintafinta iyo mitengea ikanyaa.
[8] Ntuhu nezigwa mwe sanga wenye khande, zikahota na kuvyaa vitana."
Ekubindaho kugombeka ayo, Yesu akalavya mgutio, akamba, "Mwenye magutwi na ategeeze!"

*Niya ya kuhinya kwa misimo*
*Matayo 13:10-17; Maliko 4:10-12*

[9] Wahina wakwe Yesu wakamuuza mana ya msimo uwo.
[10] Naye akawatambaisa, "Nywinywi mwekhigwa umanyi wa kumanya ukwei wa Useuta wa Muungu ambao aho kae khawekumanyika akini isasa uikwa pwii, akini awo watuhu wendawembigwe kwa

misimo, wakakauwa wasekudaha kuona, na wakategeeza wasekumanya."

*Yesu asosoa msimo wa mhasi*
*Matayo 13:18-23; Maliko 4:13-20*

11 Mana ya msimo unu ni inu, Mbeyu ni mbui ya Muungu.

12 Ziya zekugwazo mwe sia zaonyesha wantu wada wategeezao ida mbui, ikaukaaho ibiisi akeza na kudihusa mwe mioyo yao wasekweza kumzumiia na kuoholwa.

13 Ziya zekugwazo mwe maiwe zaonyesha wada wantu wategeezaho ida mbui wakaihokea kwa kinyemi. Akini inga ziya mbeyu, wantu awo khawana mazindo na mbui iyo khayekaa mwe mioyo yao kwaviya wazumiiya kwa kisingi du, na kisingi wageezwaho kubadana na mbui iyo.

14 Ziya mbeyu zekugwazo mwe miti ya miwa ni wantu wada wategeezao ida mbui, akini kisingi si kisingi, wahaukao wafintwafintwa na maatu, na vintu vyao vyose, na wekazi wa kiya msi nao khawakua mwe mbui ya Muungu.

15 Na ziya zekugwazo mwe sanga ntana nee wada wategeezao ida mbui wakaizumiiya kwa moyo mtana na wa kutegeeza. Awo kuzizimiza na kuendeea kugosoa mbui zimkundisazo Muungu.

*Taa yekugubikwayo kwa nyungu*
*Maliko 4:21-25*

16 Wantu khawawasha taa na kuigubika kwa nyungu hambu kuiika mzungui. Akini waika uwanga ya kiango ili wantu wengiaho gati wadahe kuona ung'azi.

17 "Ivyoivyo chochose chekufiswacho chenda kigubulwe, na sii yoyose yesayokumanyika na yendaimanyike pwii.

18 "Kwa iyo, muwe meso mtegeezavyo. Kwaajii yoyose mwenacho endaekigwe na ngeeko, akini yuda mwesena, hata kiya afikiicho anacho, chendakidoigwe."

*Ndugu wa kwei wa Yesu*
*Matayo 12:46-50; Maliko 3:31-35*

19 Aho mami yakwe da Yesu na wanduguze wakamwezea, akini khawokudaha kumwezea hehi kwaajii ya zumwezumwe da wantu.

20 Mntu yumwe akamwamba Yesu, "Mami yako na wanduguzo wagooka chongoi, wakunda wakuone."

21 Akini Yesu akawamba wantu wose, "Mmaa yangu na wandugu zangu ni wada wategeezao mbui ya Muungu na kuditoza."

*Yesu atwiiza khusi*
*Matayo 8:23-27; Maliko 4:35-41*

22 Msi umwe, Yesu nekakwea ngaawa hamwe na wahina wakwe, akawamba, "Tidumuwe ntondoo da mazi tiite adi phande ya kaidi." Naho, wakavoka ntambo.

23 Ekuwaho wakatamba kwa ngaawa iyo, Yesu akagona. Ahoaho khusi khai ikavoka kuvuma, mazi yakavoka kwengia mwe ngaawa, newawa hehi na kudagamia.

24 Wada wahina wakamtimia Yesu, wakamwenua wakamwamba, "Zumbe, Zumbe! Tadagamia!"

Yesu akenuka akaiwakia ida khusi na mkubwaniso wa mazi, navyo vikatwiiya, nee kwatuiiya.

25 Naho akawamba, "Uzumizi wenu u hahi?"

Akini wowo wakatozwa ni umako na kuogoha uku wakagombekana, "Uyu ni ndai, ata agiiya khusi na mkubwaniso wa mazi, navyo vyamtegeeza?"

*Yesu amhonya mntu mwekukwewa ni mazaiko*
*Matayo 8:28-34; Maliko 5:1-20*

26 Waendeeya na ntambo, wakabua mpwani ya si ya Wagelasi zekuhakanazo na ntondoo da mazi da Galilaya.

27 Ekuwaho aseeya mpwani, mntu yumwe ekuwaye kakwewa na mazaiko akamwezea kulawa he mzi uda. Kwa misi mingi mntu uyo kheekuwa akavaa magwanda, wala khekuwa akekaa mwe nyumba iya mwe mambiya.

28 Ekumuonaho Yesu, aketambika ahosi hemeso yakwe na kugombeka kwa mgutio mkuu, "Wee Yesu Mwana wa Muungu ekuwaye uko uwanga, una mbui yani na miye? Nakuhembeeza usekunisumiiza!"

29 Nee kamba ivyo kwaviya Yesu nekamwamba uyo zaiko amlawe mntu uyo. Zaiko ido ne dikamkwea mntu uyo maa kwa maa, na etiho wantu wamuika ndani na kumzengeteza kwa minyololo na mphingu, akini kiya maa akazidumua mphingu izo, akegalwa na zaiko ido adi he kiwawe.

30 Naho, Yesu akamuuza, "Zina dako ni ndai?" Yee akamtambaisa.

"Zina dangu ni 'Hindoo' " kwaajii mazaiko mangi nee yammema.

31 Ayo mazaiko wakamhembeeza Yesu asekuwegaa tubwi dilehado desado kuwa na kisiikizi.

32 Hantu aho nekuwa na tintimo kuu da nguuwe wakaiswa mwe mpolomoko wa muima. Naho ayo mazaiko wakamhembeeza awabade wawengie wada nguuwe. Naye Yesu akawabada wawengie.

33 Kwa iyo mazaiko ayo yakamlawa yuda mntu, yakengia kwa wada nguuwe na wakaseeya kwa kinyionyio mwe uda mpolomoko mkai, wakengia mwe ntondoo da mazi, wakafa.

34 Wada waisi wekuonaho yose yekuawiiayo wakaguuka, wakaita kuwekha wantu mbui mwe mzi na mwe minda.

35 Wantu wakeza kukauwa yekulawiiayo. Wakamtimia Yesu, wakamwona yuda mntu mwe kulavigwa mazaiko kekaa hehi na Yesu kavaa magwanda, na akii zakwe zimuuiya, wakaogoha.

36 Wada wantu wekuonaho ida mbui wakawagombekea wada wantu wekwezaho hada viya yuda mntu mwekuwae na mazaiko ekuoholwavyo.

37 Wantu wa si ya Gelasi wakaogoha muno. Ivyo wakamuombeza Yesu ahauke. Ivyo Yesu akakwea vituhu ngaawa ahauke.

38 Yuda mntu mwe kuavigwa yada mazaiko akamhembeeza aite hamwe naye.

Yesu akamwemeza, na akamwamba,

39 “Uya kaya ukawambe yose Muungu ekukugosweyavyo.”

Aho, yuda mntu akaita akabiikia kiya hantu mwe mzi uda mbui zose Yesu ekumgosweyavyo.

*Yesu amhonya mvyee na kumyuyusa mndee*

*Matayo 9:18-26; Maliko 5:21-43*

40 Yesu ekuuyaho phande ya kaidi ya ntondoo da mazi, zumwezumwe da wantu dikamhokea, kwaviya wose nee wakamgoja.

41 Aho akeza mntu yumwe zina dake Yailo, muongoezi wa Nyumba ya kukintania Wayahudi, nee etambika he meso ya Yesu, akamhembeeza aite kaya kwakwe.

42 Kwaajii ni mwana waikedu wa kivyee, mwenye myaka kumi dimwe na mbii, nekawa yu hehi na kuuya na nyuma.

Yesu ekuwaho akaita wantu ne wamfintafinta kiya phande.

43 Kuwa na mvyee yumwe gatigati ya diya zumwezumwe da wantu, nekawa akalawa phome kwaviya nekawa na utamu wa mtuo kwa kisingi cha myaka kumi dimwe na mbii. Naho nekabinda vintu vyakwe vyose kwa waganga, khahana ekudahae kumhonya.

44 Uyo mvyee ne amtongea Yesu nyuma, akadonta msao wa gwanda dakwe. Ahoaho, akahonywa utamu wakwe wakulawa phome.

45 Yesu akauza, “Nndai mwekunidonta?”

Wose wakaemea wakamba khahana mntu ekukudontae. Naye Petulo akamba, “Zumbe, zumwezumwe da wantu wakuikia bunga na kukufintafinta!”

46 Akini Yesu akamba, “Kuna mntu kanidonta, mana khimanya kihinya mntu kwa udaho wangu.”

47 Yuda mvyee ekuonaho khadaha kwefisa, akeaviiza huku akakama kwa kuogoha aketambika hemeso ya Yesu. Aho akawamba wantu wose chekumwekacho kumdonta Yesu na kwaviya ekuhonywavyo vuu puu.

48 Yesu akamwamba, yuda mwana kivyee, “Hita kwa uivanisa, kuzumiiya kwako kukuhonya.”

49 Ekuwaho aendeeya kugombeka, Yailo yuda muongoezi wa nyumba ya kukuntania Wayahudi akaetewa mbui kulawa kaya, “Mwana yako wakivyee kauya kaye na nyuma, usekumpisha Mhinyi.”

50 Yesu ekusikiaho ayo akamwamba Yailo, “Usekuogoha zumiiya du, naye endaahone.”

51 Ekubuwaho nyumbani kwa Yailo khawekumbada mntu kwengia ndani hamwe naye, iya Petulo, na Yohana, na Yakobo na wavyazi wa mndee uyo.

52 Wantu wose nee wakiiya na kuomboeza kwaajii ya uyo mndee ekuyae na nyuma. Aho Yesu akawamba, “Msekuiiya, kwaajii mwana khekuuya na nyuma, kagona du!”

53 Nawo wakamseka Yesu kwaajii nee wamanya kauya kae na nyuma.

54 Akini Yesu akamtoza mkono akamba, “Mwana enuka!”

55 Muye wakwe ukamuuwiya, vuu puu akenuka, Yesu akawamba wamwekhe khande.

56 Wavyazi wakwe nee wahondomaa, aho Yesu akawaemeza wasekumwamba mntu yeyose aya yekugosokayo.

# 9

*Yesu awagiiya wada wahina kumi dimwe na mbii*

*Matayo 10:5-15; Maliko 6:7-13*

1 Yesu nee awetanga wada wahina kumi dimwe na mbii, akawekha udaho wa kuguusa mazaiko yose, na udaho wa kuhonya matamu.

2 Naho akawagiiya waite kubiikia wantu mbui za Useuta wa Muungu na kuhonya wantu matamu.

3 Akawamba, “Mwendahomtambe msekudoa chochose, msekudoa ngoda wala jumu, wala khande, wala hea hata gwanda tuhu.”

4 Nyumba yoyose mwendayo mwengie na kuhokewa, ekaani umo hadi mwendaho mhauke mwe mzi uwo.

5 Wantu wendaho wawaemee kuwahokea, lawani mwe mzi uwo, nanywi mlawaho kung'untani sanga mwe miundi yenu, ili kuwa uvuhuzi kwao.

6 Naho wahina awo wakavoka kutamba, wakemboka mwe mizi wabiikia wantu Mbui Yedi na kuhonya watamu kiya hantu.

*Seuta Helode engiwa na maatu*

*Matayo 14:1-2; Maliko 6:14-29*

[7] Naye, seuta Helode mgookezi wa si ya Galilaya ekutegeezaho mbui ya yose yekulawiiayo, neawa ni maatu kwaajii wantu watuhu ne wakagombeka kuwa Yohana Mbatiiza kayuyuka.
[8] Watuhu ne watamwiiya Eliya mwekuwa muoni wa Muungu kalawiiya, na watuhu wakatamwiiya kwamba yumwe wa waoni wa kae kayuyuka.
[9] Helode akamba, "Uyo Yohana nekhimsenga mtwi, isasa nndai uyu nitegeezaye mbui zakwe?" Ne awa na hovu ya kumkauwa.

*Yesu awekha khande wantu elufu shano*
*Matayo 14:13-21; Maliko 6:30-44; Yohana 6:1-14*

[10] Wada wagiiwa wekuuyaho, wakamgombeka Yesu yose wekuyagosoayo. Yesu akawadoa, wahina wakwe wakaita hikedu mwe mzi wa Betisaida.
[11] Akini wada wantu wekumanyaho ekuitaho, wakamtongea. Yesu akawahokea ne atamwiiya nao kuusu mbui ya Useuta wa Muungu na akawahonya wada wekukundao kuhonywa.
[12] Zua dekuswaho, wada wahina kumi dimwe na mbii wakamwiitia na kumwamba, "Wabade wantu waite mwe mizi na mwe minda ya hehi wakaondeze khande na hantu hakugona, kwaviya aha teiho ni mwe nyika."
[13] Yesu akawamba, "Wekheni nywinywi khande."

Wakamtambaisa, "Khatina chochose iya mabumunda mashano na samaki waidi. Wakunda swie tikawagwiiye khande wantu wose hawa?"
[14] Wekuwaho hada nee ni wagosidu elufu shano.

Naho, Yesu akawamba wahina wakwe, "Wagombekeni wantu wekae kwe mazumwezumwe ya wantu makumi mashano."
[15] Wahina wakagosoa inga wekugombekwavyo, wambeni wantu wose wekae.
[16] Naho Yesu akayadoa yada mabumunda mashano na wada samaki waidi, akakauwa uwanga kwa Muungu na kumtogoa Muungu, akavijaiya, akabendua, akawekha wahina wakwe wawekhe wantu.
[17] Wantu wose wakada na kweguta. Wahina wakadodoa phuguntio za khande, wakamemeeza ngahu kumi dimwe na mbii.

*Petulo agombeka kwei Yesu kuwa ni Klistu*
*Matayo 16:13-19; Maliko 8:27-29*

[18] Msi umwe, Yesu ekuwaho avika ikedu, na wahina wakwe ne wawa hehi naye. Naho akawauza, "Wantu wamba miye ni ndai?"
[19] Nao wahina wakamtambaisa, "Watuhu wamba kuwa wewe ni Yohana mbatiiza, watuhu wamba ni Eliya muoni wa Muungu, na watuhu wamba ni yumwe wa waoni wa kae ambae kayuyuka."
[20] Aho akawauza, "Na nywinywi, mwamba miye ni ndai?"

Petulo akamtambaisa, "Wee nee Klistu ekusagulwaye ni Muungu."

*Yesu agombeka usuumizi wakwe na ufe wakwe*
*Matayo 16:20-28; Maliko 8:3; 9:1*

[21] Yesu akawawakia wasekumwamba mntu yoyose mbui iyo.
[22] Yesu nee aendeea kugombeka kuwa nlazima Mwana wa Mntu* endaasuumizwe na kuemewa na wadaa na waviki wakuu na wahinyi wa miko na kukomwa, akini mwe msi wa ntatu endaayuyuke.
[23] Naho akawamba wantu wose, "Mntu yoyose akundaye kunibasa nlazima eemee mwenye, adoe mhamba wakwe kia msi na anibase.
[24] Kwaviya, mntu akundaye kuohowa ugima wakwe mwenye, enda awaze, akini awazae ugima wakwe kwaajii yangu, enda auohoe.
[25] Mntu endaekhingwe myengizo yani ati akekhigwa vintu vyose vya mwe inusi, akini akawaza ugima wakwe mwenye hambu kwedagamiza mwenye?
[26] Mntu akanionea soni miye na mahinyo yangu, Mwana wa Mntu endaamwonee soni mntu uyo kisingi endachoeze mwe Ukuu wakwe na wa Tate na wandima wa uko uwanga kwa Muungu wang'azi.
[27] Nawamba kwei, kuna wamwe wenu aha khawana wauye na nyuma adi aho wendao wauwone Useuta wa Muungu."

*Yesu ahituka cheni*
*Matayo 17:1-8; Maliko 9:2-8*

[28] Yekubuwaho msi wa nane bada ya kutamwiiya ayo. Yesu ne awadoa Petulo, na Yohana na Yakobo, akaita nao mwe muima kuvika.
[29] Ekuwaho avika, cheni chakwe kikahituka, na magwanda yakwe ne yakang'ang'azika pee.
[30] Ahoaho wantu waidi wakaawiiya wakatamwiiya nae, nao ne wawa Musa na Eliya,
[31] ambao walawiiya wakawa wenye ukuu, wakatamwiiya nae kuusu kulawa kwakwe endavyo aiganye uko Yelusalemu.

* **9:22 9:22** Mwana wa mntu inamuwakilisha Yesu

32 Petulo na wenziwe ne wagona fofofo,
wekwenukaho, wakoona Ukuu wakwe, na
wada waidi wekugokao hamwe nae.
33 Naho wantu awo waidi wekuwaho
wakahauka, Petulo akamwamba Yesu,
“Zumbe ni vyedi swiswi tiaha. Naho
tizenge makumbi matatu, dimwe dako, na
dimwe da Musa na dimwe da Eliya.” Kwa
kwei khekumanya agombeka mbwai.
34 Petulo ekuwaho agombeka ayo, vuu
puu zunde dikaawiia na kuwagubika na
zunde ido dekuwezeaho wada wahina
wakaogoha muno.
35 Mgutio ukategeezeka kulawa mwe
ido zunde, “Uyu nee Mwanangu nekum-
saguaye, mtegeezeni.”
36 Wekwembokaho uwo mgutio
kutegeezeka, Yesu nekaoneka yu ikedu.
Wahina wakanyamaa myee khawokuiyan-
dua mbui iyo, na kisingi kiya kha-
wokumgombekea mntu yoyose mbui izo
wekuonazo.

*Yesu amhonya mbwanga mwenye zaiko*
*Matayo 17:14-18; Maliko 9:14-27*

37 Kioi dakwe Yesu hamwe na wahina
wakwe watatu wekuwaho waseeya kuda
kwe muima, zumwezumwe kuu da wantu
dikakintana na Yesu.
38 Aho, mntu yumwe mwe diya
zumwezumwe akatoa mgutio, akamba,
“Mhinyi! Nakuhembeeza umhonye
mwanangu wa ikedu.
39 Maa kwa maa zaiko damkweya, na
kumtenda atoe vuzo, naho damgwisa na
kumgea ugwa mtwi na kulawa fuo mwe
kanwa. Uyo zaiko amsumiiza muno na
khadimbada kwa kinyio.
40 Khiwaombeza wahina wako wadigu-
use akini khawokudaha.”
41 Yesu akamba, “Enyi uvyazi wesaho
na uzumizi, na chenye mavigaviga nn-
danekae nanyi na kuwazizimiza adi ini?”
Aho akamwamba uyo mntu, “Mwete uyo
mwanao hanu.”
42 Kisingi uyo mwana ekuwaho amwezea
Yesu, yuda zaiko neamgwisa asi na kumgea
ugwa mtwi. Akini Yesu akamwakia yuda
zaiko, na akamhonya yuda mwana na
kumwegaa mwana kwa tati yakwe.
43 Wantu wose wakahondomaa kwa
udaho mkuu wa Muungu.

*Yesu atamwiiya vituhu ufe wakwe*
*Matayo 17:22-23; Maliko 9:30-32*

Wada wantu wekuaho watozwa ni
umako kwa mbui zose ekugosoazo, Yesu
akawamba wahina wakwe.
44 “Tegezani vitana aya niyagombekayo
isasa, Mwana wa Mntu endaahitukwe na
kugewa mwe mikono ya wantu.”
45 Akini wowo khawekumanya mana ya
chekutamwiwacho. Mbui iyo iwa ifiswa
kwao wasekumanya, nao wakaogoha ku-
muuza kuusu chekugombekwacho iko.

*Mkuu nndai?*
*Matayo 18:1-5; Maliko 9:33-37*

46 Naho wahina wa Yesu wakavoka ku-
uzana kugombeka ni ndai mkuu gatigati
yao.
47 Yesu akamanya mamakhanyi
zekuwazo mwe mioyo yao, nee amdoa
mwana akamuika hehi naye.
48 Akawamba, “Yoyose amhokeaye
mwana uyu mdodo kwa zina dangu kwaa-
jii anihokeya miye. Na yoyose anihokeaye
miye, amhokea yuda mwekuniagiiya.
Kwaajii yuda ekuwaye mdodo gatigati
yenu, yee ni mkuu kusima wose.”

*Mwesekuhigana nanywi yu hamwe nanyi*
*Maliko 9:38-40*

49 Yohana akagombeka, “Zumbe tim-
woona mntu yumwe alavya mazaiko kwa
wantu kwa zina dako ne tamwemeza
kwaviya yeye khayuho hamwe naswi.”
50 Akini Yesu akamwamba, “Msekumwe-
meza, kwaviya yoyose mwesekuhigana
nanywi yu hamwe nanywi.”

*Wantu wa mzi umwe wa Samalia wae-mea kumhokea Yesu*

51 Kisingi chekubuaho hehi Yesu
kudoigwa kuita uwanga kwa Muungu,
akoona avoke ntambo ya kuita Yelusalemu.
52 Naho akawagiiya wagiiwa wamuon-
goee, nao wakaita wakengia mwe mzi
umwe wa wantu Wasamalia wamgoswee
kia kintu.
53 Akini wenyezi wa mzi uda ne wae-
mea kumhokea kwaviya nekawa akaita
Yelusalemu.
54 Wahina wakwe, Yohana na Yakobo
wekuonaho ayo wakamba, “Zumbe
wakunda tiuwagiiye moto kulawa uwanga
kwa Muungu uwadagamize?”
55 Akini Yesu neawahitukia, na kuwakia.
56 Wakalawa, wakaita mwe mzi mtuhu.

*Wakundao kumbasa Yesu*
*Matayo 8:19-22*

57 Wekuwaho watamba mwe sia,
mntu yumwe akamwamba Yesu, “Nen-
danikubase hohose uitako.”
58 Yesu akamba, “Mbweha wana phanga
na wadege wa uwanga kwa Muungu wana
masasa, akini Mwana wa Mntu khana
hantu ha kugona.”
59 Naho akamwamba mntu mtuhu, “Ni-
tongea.”
Mntu uyo akamba, “Zumbe, nieka nivoke
kuita kwe uzisi wa tate.”
60 Yesu akamwamba, “Wabade wantu
wekuwao wauya na nyuma mwe mioyo

yao wazike wekuyao na nyuma wezwao, iya wee hita ukabiikie Useuta wa Muungu."
61 Na mntu mtuhu akamwamba, "Zumbe
nendanikubase, akini eka nkaage wada wekuwao mwe kaya yangu."
62 Yesu akamwamba, "Mntu yoyose
atozaye gembe na yutayali kuima na uku akauwa nyuma, khafaa kwa Useuta wa Muungu."

# 10

*Yesu awagiiya wandima makumi mfungate na mbii*

1 Yekwembokaho ayo Zumbe akasagua
watuhu makumi mfungate na mbii, akawagiiya wandima waidiwaidi wamuongwee mwe kiya mzi ambao yee mwenye ne akakunda kuita.
2 Akawamba, "Ubosi ni mwingi
akini wabondaji ni wacheche, kwa iyo mwoombezeni Zumbe wa ubosi agiiye wantu wakabonde."
3 Isasa hitani, manyeni kuwa nawagiiya
nywinywi inga ngoto waitao gatigati ya makui ya mzitui.
4 Msekudoa kifuko cha hea, jumu wala
sabana, msekumuugusa mntu yoyose mwe sia.
5 Mkengia mwe kaya yoyose mvoke
kuwaugusa ivi, "Uivanisa uwe mwe nyumba inu."
6 Akawaaho mntu akundaye uivanisa,
ugusi wenu wa uivanisa wenda usigae, ama khivyo uugusi uwo wa utuivu undauwauwie.
7 Ekaani mwe nyumba iyo mkada na
kudomea wendavyo wawekhe, kwaviya mndima afaigwa kwekhigwa kima chake. Msekusama nyumba inu na nyumba ida.
8 Ati mkabua mzi wowose na wantu
wakawahokea, daani wendavyo waviete hemeso yenu.
9 Honyani watamu wekuwao uko, wag-
ombekeni wantu, "Useuta wa Muungu u hehi."
10 Akini mkengia mwe mzi wowose,
wakesekumihokea, lawani, nanyi mwembokaho mwe sia zao gombekani,
11 Hata sanga za mzi wenu yeku-
tozananayo, na miundi yetu tayakung'uta iwe tangio ya mavigaviga yenu. Akini manyani kuwa, "Useuta wa Muungu uhehi."
12 Kwei nawamba, msi wa kuamuiwa
mzi uwo wendawekhigwe sugusa khuu kusima yada mavigaviga ya wantu wa mzi wa Sodoma.

*Wantu wa mizi yesayo kuzumiiya*
*Matayo 11:20-24*

13 Mmbui yenu wantu wa Kolazini!
Mmbwii yenu wantu wa Betisaida, inga vihii vyekugosokazo kwako ati ne vigosoka kuda Tilo na Sidoni, nee wawa wavaa kae magunia na kwesisa mazeu na ili koonyesha kuhituka na kubada mavigaviga yao.
14 Hata ivyo, msi wakuamuiwa nywinywi
mwenda mwekhigwe sugusa khuu kusima ida ya wantu wa Tilo na Sidoni.
15 Nywie wantu wa Kapelinaumu,
"Mweona mwenda mwekhigwe ntogoo adi uwanga kwa Muungu? Eehe, mwendamseezwe adi asi kwe si ya wantu wekuuyao na nyuma."
16 Yesu akawamba wahina wakwe,
"Endaeawategeeze nywinywi, anitegeeza miye, na endayeawaemee kuwahokea nywinywi, aemeya kunihokea miye. Na yoyose aemeaye kunihokea, aemea kumhokea yuda ekuniagiiaye ambae ni Muungu."

*Kuuya kwa wada wahina kumi mfungate na mbii*

17 Naho wada makumi mfungate
na mbii newauya wamema kinyemi, wakagombeka, "Zumbe hata mazaiko yatutegeeza tekuyawakiaho kwa zina dako."
18 Yee akawatambaisa, "Khimwona ibiisi
ekuwavyo akagwa inga umweko wa umbauwa kulawa uwanga kwa Muungu.
19 Kauwa khiwekha udaho wa ku-
jata nyoka na visuse, na udaho wose wakumvota yuda mmasa, wala khahana kintu chochose chendachokimizuu.
20 Naho msekuwa na kinyemi kwaajii
mazaiko wamitegeeza, iya kuwani nanyemi kwaajii mazina yenu yaandikwa uwanga kwa Muungu muwe wantu wa Muungu."

*Yesu awa na nyemi*
*Matayo 11:25-27; 13:16-17*

21 Saa idaida, Yesu nekawa na nyemi
kwa udaho wa Muye wa Muungu, akamba, "Nakutogoa ee Tate, Zumbe wa uwanga kwa Muungu na inusi, kwaajii mbui izi wekuwafisazo wenye akii na umanyi, ukawamanyisa wadodo. Eehe Tate, ne vyekukutamiavyo."
22 Ne agombeka, "Tati yangu kanekha
vintu vyose. Khahana ammanyaye Mwana iya Tate, wala ammanyaye Tate iya Mwana, na yoyose yuda ambae Mwana endaakunde kumgubuiya."
23 Naho akawabasa wahina wakwe
akawamba he ikedu, "Wajaiwa wada wakauwao mbui izi mkauazo nywinywi!
24 Kwei nawamba, waoni na maseuta
watamiwa kukauwa yada muyakauwayo nywinywi akini khawekuyaona na kuyategeeza yada mtegeezayo akini khawadaha."

*Msamalia yedi*

25 Aho mhinyi wa miagiiyo yumwe
akagooka, akamuza Yesu, akakunda
kumgeeza, “Mhinyi, nigosoe mbwai nidahe
kwekaa misi yose kwesaho kisiikizi?”
26 Yesu akamtambaisa, “Yamba mbwai
mwe miagiiyo? Mwamamakhanya vi-
ivihi?”
27 Yuda mntu akamtambaisa Yesu,
“Mkundise Zumbe Muungu yako kwa moyo
wako wose, kwa muye wako wose, kwa
udaho wako wose na kwa akii zako zose.
Na mkunde mntu wa hehi nawe inga
wekundavyo wee mwenye.”
28 Yesu akamwamba, “Kutambaisa vyedi!
Gosoa ayo, nawe wendauwe na ugima wa
misi yose kwesaho kisiikizi.”
29 Akini yuda Mhinyi wa miagiiyo
neakakunda kweonyesha kuwa ni mtana
akamuuza Yesu, “Na mntu wa hehi yangu
ni ndai?”
30 Yesu akamtambaisa, “Mntu yumwe
kawa akaseeya kulawa Yelusalemu kuita
Yeliko. Ekuwaho mwe sia, neafuntiwa ni
mabagaa, na kumhoka vintu vyake vyose
na kumtoa na kumbada kagona hada hehi
na kuuya na nyuma.”
31 Ahoaho mviki yumwe nekawa akem-
boka mwe sia idaida, ekumuonaho akem-
boka khandani.
32 Nee eza Mlawi yumwe, ekubuwaho
hada hantu akamwona, naye akemboka
khandani.
33 Akini Msamalia yumwe nekawa
akatamba, neabuwa hada kwa yuda mntu
ekufintwae ekuwaho, naye ekumuonaho
akamfiiya mbazi.
34 Akambasa, akamfunga vionda vyakwe
kwa vibwende na kumsisa mavuta ya mza-
ituni na divai, akamkweza uwanga ya
phunda wakwe, akamwegaa mwe nyumba
ya kuhumuizia wageni akamhumiza.
35 Kioi yakwe akalavya ntii mbii vya
madini ya feza akamwekha yuda mwenye
nyumba akamwamba, “Mhumize mntu
uyu na chochose wendachoutumie, nen-
danikuihe nendahoniuye.”
36 Naho Yesu akauza, “Gatigati ya awo
watatu, ni yuhi mwekweonyesha kuwa
mntu wa hehi yakwe yuda ekufuntiwaye
na mabagaa?”
37 Yuda mhinyi wa miko akamtambaisa,
“Ni yuda ekumfiiaye mbazi.”
Yesu akamwamba, “Hita ukagosoe ivy-
oivyo.”

*Yesu awavuia Malita na Malia*

38 Yesu na wahina wakwe wekuwaho
watamba kuita Yelusalemu, wakengia
mwe mzi umwe na mvyee zina dakwe
Malita, akamhokea kaya kwakwe.
39 Malita ne kawa na dadiye etang-
waye Malia uyu ne kekaa hehi na Zumbe
akategeeza mahinyo yakwe.
40 Akini Malita nekawa akagosoa ndima
za zikoi na mbui nyingi, nee akamwiitia
Yesu akamwamba, “Zumbe ivi khupatiiza
kwambwai dada yangu kanibada nagosoa
ndima za zikoi ikedu? Umgombeke ani-
ambiize.”
41 Akini Zumbe akamtambaisa, “Malita,
Malita kwambwai wepisha kwa ndima
nyingi.”
42 Akini kuna mbui mwenga ntana
kusima yose, mbui iyo ni kunitegeeza.
Malia nee ekusaguado na khahana mntu
yoyose adahae kumhoka.

# 11

*Yesu ahinya kuvika*
*Matayo 6:9-13; 7:7-11*

1 Msi umwe, Yesu kawa hantu akavika.
Ekubindaho kumvika Muungu, yumwe
wa wahina wakwe akamwamba, “Zumbe,
takunda utihinye kuvika inga Yohana
mbatiiza ekuwahinyavyo wahina wakwe.”
2 Yesu akawamba, “Mkavika Muungu,
gombekani ivi,
‘Tate yetu weuko uwanga kwa Muungu
Zina dako ditogolwe,
Useuta wako weze.
3 Utekhe khande yetu kiya msi.
4 Utiekee mavigaviga yetu,
Kwaajii swie tiwaekeavyo wose weku-
tikoseao,
Wala wesekutingiza mwe mageezo.’ ”
5 Naho Yesu akawamba wahina
wakwe, “Nndai gatigati yenu mwenye
mmbuya wakwe akamwezea na kio
kikuu akamwamba, ‘Mmbuya nekha
mabumunda matatu.
6 Kwaajii mmbuya wangu kanezea
alawa ntambo, namiye khina khande ya
kumwekha.’
7 Naho yuda mwe kuwa gati akamtam-
baisa, ‘Usekunipisha uvi uvugalwa kae,
miye na wanangu tigona kae, khidaha
kwenuka na kukwekha ukundacho.’
8 Kwei nawagombeka inga uyo mntu
khana enuke na kumwekha ayo mabu-
munda kwaajii ni mmbuya wakwe, akini
kwaajii ya uyo mntu kwesekuona soni
kuendeea kwakwe kumwetanga enda
enuke na kumwekha kia ekukikundacho.
9 “Ivyo nawagombakeni, ombezani
nanywi mwondamwekhigwe, ondezani na
nywie mndampate, kontani uvi nanywi
mwenda mvuguiwe.
10 Kwaviya kia aombezaye ekhigwa, na
kia aondezaye endaekhigwe na kia akon-
taye uvi avugwiiwa.

11 Hambu kuna yoyose gatigati mwenu, mwana yakwe akamwombeza samaki, enda amwekhe nyoka na khiyo samaki?

12 Hambu mwana akamwomba tagi, endaamwekhe kisuse?

13 Naho nywinywi wenye mavigaviga mwadaha kuwekha wana wenu vintu vyedi, kwei tati yenu wa uwanga kwa Muungu endaagosoe muno, endaawekhe Muye wa Muungu wada wamuombezao!"

*Yesu na Belizebuli*
*Matayo 12:22-30; Maliko 3:20-27*

14 Naho Yesu ekuwaho amlavya zaiko mwe kuwa kwa mntu ekuwaye khadaha kutamwiiya. Yuda zaiko ekumlawaho yuda mntu mwekuwa khadaha kutamwiiya, nee avoka kutamwiiya na zumwezumwe da wantu dikahondomaa.

15 Akini wamwe wa wantu awo wakagombeka, "Aguusa mazaiko kwakwekhigwa udaho wa Belizebuli, yuda muongoezi wa Mazaiko."

16 Wantu watuhu wakamgeeza, wakaonda awaonyeshe utangio kulawa uwanga kwa Muungu.

17 Akini yee, akamanya mamakhanyi zao, akawamba, "Useuta wowose wekuiganyikao vizumwezumwe vihiganavyo khaudaha kwekaisa, naho wandugu wowose wenao khumbizi wadagamia."

18 Inga Ibiisi akahigana yee mwenye, useuta wakwe wendagooke viivihi? Isasa mwadaha viivihi kugombeka ati nalavya mazaiko kwa udaho wa Belizebuli?

19 Naho, inga miye nkawaguusa mazaiko kwa udaho Belizebuli, hata wahina wenu pia wawaguusa kwa udaho wakwe, kwaajii iyo wahina wenu nee wendaowawamuiye nywinywi.

20 Akini ikawa naguusa mazaiko kwa udaho wa Muungu, manyeni kuwa useuta wa Muungu ubuakae kwenu.

21 "Mntu mwenye muku aindaho nyumba yakwe kwa guha na uta, vintu vyakwe vyose vyendaviwe mwe uivanisa.

22 Akini akeza mwenye muku muno, akamfuntia na kumvota, mntu uyo endaadoe vitoanavyo vyakwe ekutegemeavyo na kudoa vintu vyakwe vyose."

27 Aho wahina wakwe wakauya, wakamaka koona atamwiiya na mvyee, akini khahana yumwe yao ekumuuzae yuda mvyee, “Waondeza mbwai?” Wala khahana ekumuuzae Yesu, “Kwa mbwai watamwiiya na mvyee?”
28 Yuda mvyee akabada biga dakwe hada, akaita mwe mzi na kuwamba wantu.
29 “Sooni mumkauwe mntu mwekunamba mbui zangu zose nigosoazo. Ivi, adahika yee nee Klistu.”
30 Wantu wakalawa mwe si ya Samalia wakambasa Yesu.
31 Kisingi icho wahina wakwe wamuombeza Yesu, “Mhinyi, daa khande.”
32 Akini Yesu akawamba, “Miye nina khande mwesayo kuimanya nywie.”
33 Wahina wakwe wakauzana, “Ivi kuna mntu mwekumweetea khande?”
34 Yesu akamba, khande yangu ni kugosoa akundavyo yuda mwekuniagiiya na kubindiiza ndima ekunekhayo kuigosoa.

35 Nywie mwagombeka, “Isigaa miongo minne kisingi cha ubosi kibua.” Akini miye nawamba, kauwani minda, khande zidahaa na zihehi kubondwa.

36 Mbosi ekhigwa maiho yakwe, na akusanya khande kwaajii ya ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi, ivyo mhasi na mbosi, wendawawe na nyemi hamwe.

37 Msimo unu ni kwei, “Yumwe ahanda mtuhu abonda.”

38 Miye khiwagiiya mkabonde ubosi mwe minda ambayo khamwekuiima, watuhu nee wakagosoa ndima uko, akini nywinywi mwapata myengizo kwembokea ndima yao.

39 Wasamalia wangi wa mzi uda wakamzumiiya Yesu kwaajii ya mbui ekugombekazo yuda mvyee kuwa, “Kanivuhuzia mbui zose nekuzigosoazo.”

40 Wasamalia wakambasa Yesu wakamuombeza ekae nawo, akekaa mwe mzi uwo misi miidi.

41 Wantu wangi wamzumiiya Yesu kwaajii ya mbui zakwe

42 Wakamwamba yuda mvyee, “Khatizumiiya du kwaajii ya mbui zako, akini swie wenye timtegeeza na timmanya kuwa uyu nee kwei Mwohozi wa inusi.”

*Yesu amhonya mwana wa mgookezi yumwe*

43 Yekwembokaho misi miidi, Yesu akahauka hada akaita mwe si ya Galilaya.

44 Kwaviya Yesu mwenye kavuhuzia pwii, “Muoni khana atunywe mwe mzi wakwe mwenye.”

45 Ekubuaho mwe si ya Galilaya, wantu wa Wagalilaya wangi wakamhokea, kwaajii nao nee waita kwe sikukhuu ya Pasaka Yelusalemu, nako nee wawa wayaona yose ambayo Yesu kayagosoa.

46 Yesu akabua vituhu mzi wa Kana uko Galilaya, hantu ekuhituaho mazi na kuwa divai. Nee kuwa na mgookezi yumwe ekuwae na mwana mtamu uko Kapelinaumu.

47 Muongoezi uyo ekusikiaho Yesu kalawa Uyahudi na kubua Galilaya akambasa akamwoombeza aite akamhonye mwanawe mwekuwa mtamu wa kukauwiiwa.

48 Yesu akamwamba, “Mkesekuona utangio na vihii khamna mzumiiye.”

49 Uyo Mwoongoezi akamwamba, “Zumbe chondechonde tite mwanangu asekweza kuuya na nyuma.”

50 Yesu akamwamba, “Hita mwanao ni mgima.”

Uyo muongoezi nee azumiiya mbui za Yesu, akaita zakwe.

51 Ekuaho yu siai, akakintana na wandima wakwe wakamwamba, “Yuda Mwana kindee kahona.”

52 Naye akawauza neeiwa saa nyingahi mwana ekuhoneaho, wakamwamba, “Zana saa mfungate wa musi, utamu ukamuweekea”.

53 Uyo tati yakwe akakumbuka iwa saa idaida Yesu ekumwambaho, “Mwanao ni mgima.” Aho akazumiiya hamwe na nyumba yakwe yose.

54 Unu nee utangio wa kaidi ekugosoao Yesu ekuaho akaawa Uyahudi kuita Galilaya.

# 5

*Yesu amhonya mtu uko Betisaza*

1 Yekwembokaho ayo, Yesu akaita Yelusalemu kwe sikukhuu ya Wayahudi.

2 Uko Yelusalemu, hehi na uvi wetangwao uvi wa ngoto, nehawa na tondoo da mazi detangwado kwa kiebulania Betisaza ambado nee dizunguukwa na mabaaza mashano.

3 Aho nehawa na watamu wangi wekaa, matuntu, na wesao kudaha kwenda, na wekuhooawo. Newawa wakagoja mazi yatibulwe.

4 Kwaviya mndima wa uwanga wa Muungu kuna kisingi aseeya na kuyavuuga mazi mwe tindiziwa ido, mtamu yoyose avokae kwengia mwe mazi aho mazi yakatibulwa, ahona utamu wakwe wowose ekuwao nao.

5 Aho, hana mgosi mwekuwa mtamu kwa kisingi cha myaka makumi matatu na minane.

6 Yesu ekumuonaho kagona aho na kumanya kuwa kawa mtamu kwa misi mingi, akamwamba, “Ivi, wakunda kuhona?”

7 Yuda mtamu akamtambaisa, “Zumbe khina mntu wa kunegaa mwe tondoo da mazi kisingi yakatibulwa, kia nikageeza kwengia mntu mtuhu aniongweeya.”

8 Yesu akamwamba “Gooka, na doa javi dako wende.”

9 Vuupuu uyo mntu akahona, akadoa javi dakwe.

Akavoka kwenda, mbui inu igosoka Msi wa Kuhumwiiza.

10 Wamwe wa waongoezi wa Wayahudi wakamwamba yuda mwe kuhonywa, “Ivyeeo ni Msi wa Kuhumwiiza kwa miko yetu khukundigwa wenue javi dako.”

11 Yee akawatambaisa, “Yuda mntu mwekunihonya nee mwekunamba udoe javi dako wende.”

12 Nawo wakamuuza, “Uyo mntu mwekukwamba udoe javi dako wende ni ndai?”

13 Iya yuda mntu khekummanya mntu mwekumhonya, Yesu nee kahauka kae hantu hada, kwaajii nee hana zumwezumwe kuu da wantu.

14 Naho bada ya ayo, Yesu akambwiiya yuda mntu mwekumhonya mwe Nyumba ya Muungu akamwamba, “Isasa kuhona, wesekugosoa mavigaviga vituhu, usekweza kubwiiwa ni mbui fyaimi muno.”

15 Yuda mntu akaita, akawamba wakuu wa Kiyahudi, Yesu nee mwekunihonya.

16 Kwaviya Yesu ida mbui kaigosoa Msi wa Kuhumwiiza, Wayahudi wakavoka kumkefyakefya Yesu.

17 Yesu akawamba, “Tate yangu agosoa ndima misi yose, na miye nagosoa ndima kwesiho kueka.”

18 Kwa mbui izi waongoezi wa Kiyahudi wakoondeza sia ya kumkoma Yesu, khio kwaviya kabananga miko ya Msi wa Kuhumwiiza du, akini kamba Muungu ni Tati yakwe ivyo ketenda aigana na Muungu.

*Udaho wa Mwana wa Muungu*

19 Yesu akawamba, “Kwei nawamba, Mwana khadaha kugosoa kintu ikedu, adaha kugosoa kia amuonacho Tate agosoacho, kwaviya agosoacho Tate, Mwana nae akigosoa viyaviya.”

20 Kwaviya Tate amkundisa Mwana, na kumuonyesha kia kintu agosoacho mwenye. Naho endaamuonyeshe mbui khuu kusima izi, nanywi mwendamhondomae.

21 Inga viya Tate ayuyusavyo wekuuyao na nyuma, na kuwekha ugima, ivyoivyo Mwana naye awekha ugima wada awakundisao.

22 Tate khamuamuiiya mntu yoyose, iya kamtenda mwana awaamwiiye wantu wose.

23 Ili wantu wamtegeeze Mwana inga wamtegeezavyo Tate, yoyose esaekumtegeeza Mwana khamtegeeza Tate wekumwaagiiaye Mwana.

24 “Nawamba kwei, wada wategeezao mbui zangu na kumzumiia yuda mwekuniagiiya wana ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi, khana aamuiiwe katu, kwaviya wavota kae ufe na kwengia mwe ugima misi yose kwesiho kisiikizi.”

25 Nawamba kwei, kisingi cheza, naho kibuwa kae, na wada wekuwao hae na Muungu, wenda wategeeze mgutio wa Mwana wa Muungu, awo wenda wahokee ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi.

26 Inga viya Tate awekhavyo wantu ugima, viyaviya kamtenda Mwana awekhe wantu ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi.

27 Naho kamwekha Mwana udaho wa kuamuiiya, kwaviya ni Mwana wa Mntu.

28 Msekuhondomaa kwaajii ya mbui inu, kisingi cheza ambacho wose wekuuyao na nyuma wenda wategeeze mgutio ambao wose wekuwao mwe mambiya.

29 Nawo wendawalawe mwe mambiya wada wekugosoao matana, wenda wayuyuke na kwekaa, wada wekugosoao yesayokutama wenda wayuyuswe na kuamuiiwa.

*Wavuhuzi wa Yesu*

30 Yesu akaendeea kugombeka, “Khidaha kugosoa kintu kwa udaho wangu mwenye, miye neamuiiya inga nitegeezavyo kulawa kwa Tate na uwo wedi wangu ni wa kwei, kwaviya khigosoa nikundavyo mwenye, iya akundavyo yuda mwekuniagiiya.”

31 “Inga nawagombeka nywie mbui zangu mwenye, naho yada nigombekayo khamyavuhuzia kuwa ni ya kwei.

32 Akini hana mntu mtuhu avuhuziae mbui zangu kwenu, na namanya agombeka kwei.

33 Nywie nee muagiiya wantu kwa Yohana wamuuze mbui zangu, nae akawavuhuzia ni kwei.

34 Khio inga nakauwiiya wantu wanivuhuzie, akini nayagombeka aya ili mdahe kuoholwa.

35 Yohana nee kawa inga taa yekuwayo ikaka na kulavya ung'azi, nanywi muwa na nyemi na ung'azi uwo kwa kisingi kijihi.

36 Akini kuna mbui khuu muno iyonyeshayo miye ni ndai kusima yada ekugombekayo Yohana mbatiiza. Mbui yenye ni zia ndima ekunekhazo Tate nizigosoe, ayo yose yanivuhuzia miye ni ndai na yaonyesha Tate nee mwekuniagiiya.

37 Naye tate mwekuniagiiya kanivuhuzia miye ni ndai, akini khamzati kutegeeza mgutio wakwe, naho kumwona yee eivyo,

38 na mbui yakwe khayekwekaa mwe mioyo yenu, kwaviya khamwekumzumiiya yuda mwekumuagiiya.

39 Nywie mwayasunguumanya muno Maandiko ya Muungu kwaviya mwamamaakhanya mwe ayo mwendampate ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi, na Maandiko ayo yanivuhuzia miye!

40 Ata ivyo khamkunda kweza kwangu ili mhokee ugima.

41 “Miye khiondeza kutunywa na wantu.

42 Akini nawamanya nywie ni wantu wa namna yani, na viyaviya khamna ukundiso wa Muungu mwe mioyo yenu.

43 Miye ncheza kwa udaho wa Tate, akini khamnihokea, akini akeza mntu mtuhu kwa udaho wakwe mwenye, mwenda mumhokee.

44 Mwakunda kuhokea ntunyo kulawa
kwenu nywie wenye, akini khamkunda
kuhokea ntunyo kulawa kwa Muungu
mwenye, kwaajii iyo mwadaha viivihi ku-
nizumiiya?
45 Akini wesekufanyanya kuwa miye ne-
nendae niwaahie masa kwa Tate, Musa
ambae mwamkauwiya neendae awaahie
masa.
46 Ati kwei nee mkamzumiiya Musa,
nee mkanizumiiya na miye, kwaviya Musa
kaandika mbui zangu.
47 Akini kwaviya khamyazumiiya yada
ekuyaandikayo Musa, mwadaha viivihi
kuzumiia kiya nigombekacho?"

# 6

*Yesu awekha khande wantu elufu shano*
*Matayo 14:13-21; Maliko 6:30-44; Luka 9:10-17*

1 Yekwembokaho ayo, Yesu akadumua
tindiziwa da mazi da Galilaya. Kwa zina
tuhu detangwa ziwa da Tibelia.
2 Zumwezumwe kuu da wantu dika-
tendesa kumbasa kwaajii waona ntangio
nyingi na vihii ekugosoazo kwa watamu.
3 Yesu akakwea kwe muima, akekaa
hamwe na wahina wakwe.
4 Na Sikukhuu ya Wayahudi yetangwayo
Pasaka iwa hehi.
5 Naho Yesu ekukauwaho, na kuona
zumwezumwe da wantu dikeza kwakwe,
akamwamba Fiipo, "Tendatigue hahi
mabumunda, wantu awa wadahe kuda?"
6 Nee kauza mbui iyo kumgeeza Fiipo
kwaviya kamanya endachoagosoe.
7 Fiipo akamtambaisa, "Ata inga tikawa
na hea dinali mia mbii nee khatokudaha
kugua mabumunda ya kuwekha wantu
awa."
8 Mhina yakwe yumwe mwetangwa And-
ulea uyo nee kawa nduguye Simoni Petulo
akamwamba Yesu,
9 "Yuhanu mbwanga yumwe ana mabu-
munda mashano ya shaili na samaki vi-
dodo viidi, akini vyendavitoshe mbwai
kwa wantu wangi inga awa?"
10 Yesu akamba, "Waikeni wantu," hantu
hada nehawa na ulondo mtana, wantu
wakekaa, na wagosi du nee wawa elufu
shano.
11 Naho Yesu akadoa yada mabumunda
akamtogoa Muungu, akawapangia wantu
wekuawo wekaa, akagosoa viyaviya na
wada samaki, kia mntu akahokea na akada
inga akundavyo kuda.
12 Wantu wekwegutaho Yesu akawamba
wahina wakwe, "Dodoani phuguntio
zekusigaazo kisekwaga chochose."
13 Wakadodoa phuguntio zia za mabu-
munda ya shaili vyekusigazwavyo na wada
wantu wekudao, wakamemeeza ngahu
kumi dimwe na mbii.
14 Wantu wekuonaho ntangio icho
ekugosoacho Yesu wakamba, "Kwei uyu
nee muoni tekumkauwiaye endaeze mwe
inusi."
15 Yesu akamanya kuwa wantu waon-
deza kumdoa wamtende Seuta, akahauka
vituhu akaita kwe muima yee ikedu.

*Yesu enda uwanga ya mazi*
*Matayo 14:22-33; Maliko 6:45-52*

16 Yekubuaho guoni wahina wakwe Yesu
wakaseeya mwe mazimshindo,
17 wakakwea ngaawa ili wemboke waite
Kapelinaumu. Kiza nee chengia kae, na
Yesu nee khazati kuseeya mwe muima ili
awe nawo.
18 Tindiziwa da mazi dikavoka kuvu-
ugika kwaajii khusi khai neiwa yavuma.
19 Wahina wakwe Yesu newawa waka-
toa makasia kuita inga uhae wa kilomita
shano hambu mtandatu, wakamwona Yesu
akenda uwanga ya mazi, akaitimia ngaawa
wakaogoha muno.
20 Akini Yesu akawamba, "Ni miye
msekuogoha."
21 Nee wakoondeza kumwegaa Yesu he
mpwani ahoaho ngaawa ibuwa mwe si
khavu wekuwayo waita.

*Wantu wamuondeza Yesu*

22 Kioi dakwe zumwezumwe da wantu
wada wekuwao wekaa phande ya kaidi ya
tindiziwa da mazi nee wakabukhua kuwa
hawa na ngaawa mwengadu hantu hada,
Yesu khekwengia mwe ida ngaawa hamwe
na wahina wakwe, iya wahina awo nee
waita kae ikedu.
23 Wantu watuhu kulawa Tibelia wak-
abuwa na ngaawa, hantu hada wantu
wekudaho mabumunda, Zumbe ekumto-
goaho Muungu.
24 Naho wantu wekumanyaho ati Yesu
na wahina wakwe khawekuwaaho hantu
hada, wakakwea mwe ngaawa izo na
wakaita Kapelinaumu kumuondeza Yesu.

*Yesu nee bumunda da ugima*

25 Wada wantu wekumbwiiaho Yesu
phande ya kaidi ya tondoo da mazi waka-
muuza, "Mhinyi, kubuwa ini aha?"
26 Yesu akawatambaisa, "Nawamba kwei
mwaniondeza khio kwa viya muona ntan-
gio nekugosoavyo, iya kwaajii nee mda
yada mabumunda mkeguta.
27 Msekugosoa ndima kwaajii ya
kwepata khande ibanikayo, iya gosoani
ndima kwaajii ya khande yesayo kubanika
vyekaa misi yose kwesiho kisiikizi. Khande
izo zendaziwekhe ugima wa misi yose kwe-
siho kisiikizi kulawa kwa Muungu. Mwana
wa Mntu nee endayeawekhe khande iyo,

kwaajii Tate Muungu khamwekha udaho
wa kugosoa ivyo."
28 Wowo wakauza, "Titende mbwai
tidahe kugosoa ndima za Muungu?"
29 Yesu akawatambaisa, akawamba,
"Ndima ambayo Muungu akunda mwi-
igosoe nikunizumiiya mie, ambae kiagiiwa
nae."
30 Aho wakamwamba, "Wendaugosoe
ntangio yani ili tiikauwe tidahe kukuzumi-
iya?
31 Mababa zetu wada khande yekwe-
tangwayo mana kuda kwe kiwawe, inga
yagombekavyo Maandiko ya Muungu,
'Kawaisa mabumunda kulawa uwanga.'
"
32 Yesu akagombeka, "Nawamba kwei,
Musa khekuwekha mabumunda kulawa
uwanga kwa Muungu, iya Tate yangu nee
awekhae nywie bumunda da kwei, kulawa
uwanga kwa Muungu.
33 Kwaviya bumunda da Muungu ni yuda
ekuseeaye kulawa uwanga kwa Muungu,
ili awekhae wantu wa inusi inu ugima wa
misi yose kwesiho kisiikizi."
34 Aho wakamwamba, "Zumbe, kuvoka
isasa tekhe bumunda ido misi yose."
35 Yesu akawamba, "Miye nee bumunda
da ugima." Na mntu yoyose ezae kwangu
na kunizumiiya khanaawe na saa wala
khiu katu.
36 Akini nawamba kuwa, mniona akini
khamnizumiiya.
37 Wose anekhao Tate, wendaweze
hangu na mie katu khina nimwase chongoi
yoyose mwendaeeze hangu,
38 Kwaviya khiseeya kulawa uwanga
kwa Muungu, khio kwaajii ya kugosoa
yada niyakundayo mie, iya kugenyeza
yada akundayo Muungu mwekuniagiiya.
39 Na yada akundayo Muungu mweku-
niagiiya nee aya, nesekumwaza ata
yumwe gatigati ya wada ekunekhao, iya
niwayuyuse wose msi wa kisikizi.
40 Kwaviya akundavyo Tate, nee iki kia
mntu amkauwaye Mwana na kumzumi-
iya, awe na ugima wa misi yose kwesiho
kisiikizi, naho nenda nimyuyuse msi wa
kisiikizi.
41 Aho Wayahudi wakavoka kung'ung'uzika
kwaviya kagombeka, "Miye ni bumunda
dekuseeyado kulawa uwanga."
42 Wakamba, "Uyu khi Yesu mwana wa
Yusufu? Tammanya tati yakwe na mami
yakwe naho, adaha vivihi kugombeka ati
kaseeya kulawa uwanga kwa Muungu?"
43 Yesu akawatambaisa, "Ekani ku-
nung'unika nywinywi kwa nywie.
44 Khahana mntu adahae kweza kwangu,
inga Tate mwekuniagiiya khekumuongoea
kwangu, na miye nendanimyuyuse mntu
uyo msi wa kisiikizi.
45 Muoni yumwe wa Muungu nee
kaandika mwe kitabu cha Muungu, 'Wantu
wose wenda wahinywe ni Muungu.' Kia
mntu amtegeezaye na kumzumiia Tate,
eza kwangu.
46 Inu khaina mana kuwa, yuuko mntu
yee ikedu mwekumuona Tate, iya ni yuda
ekulawae kwa Muungu, uyo nee mweku-
muona Tate.
47 Kwei nawamba, mnizumiiya ana
ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi.
48 Miye ni bumunda da ugima.
49 Mababa zenu nee wada khande yek-
wetangwayo mana kuda kwe kiwawe,
akini wauya na nyuma.
50 Akini idi ni bumunda diseeyado ku-
lawa uwanga kwa Muungu, mntu yoyose
adae khadaha kuuya na nyuma.
51 Miye ni bumunda da ugima
wekuseeao kulawa uwanga kwa Muungu,
mntu yoyose mwendaye ade bumunda
idi endaekae misi yose kwesiho kisiikizi,
na bumunda nendado nimwekhe ni mwii
wangu naulavya kwa ugima wa inusi."
52 Aho Wayahudi wakavoka kuhigana
wowo wenye wakauzana, "Adaha viivihi
kutekha mwii wakwe tiude?"
53 Yesu akawamba, "Nawamba ukwei,
mkesekuuda mwii wa Mwana wa Mntu na
kudomea phome yakwe khamnamuwe na
ugima mwe mii yenu.
54 Adae mwii wangu na kudomea phome
yangu anawo ugima wa misi yose kwesiho
kisiikizi, na miye nenda nimyuyuse msi wa
kisiikizi.
55 Kwaviya mwii wangu ni khande ya
kwei na phome yangu ni kidomewacho cha
kwei.
56 Yoyose adae mwii wangu na kudomea
phome yangu ekaa umu mwangu na miye
nekaa kwakwe.
57 Tate wa ugima kaniagiiya nigosoe
ndima na miye nekaa kwaajii yakwe, ivyo
anidae miye naye endaekae kwaajii yangu.
58 Naho idi nee bumunda dekuseeyado
kulawa uwanga, khio inga bumunda weku-
dayo mababa zenu, ata ivyo wakauya na
nyuma, adae bumunda idi endaawe na
ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi."
59 Yesu kagombeka ayo ekuaho akahinya
he Nyumba ya kukintania Wayahudi uko
Kapelinaumu.

*Mbui zietazo ugima wa misi yose kwe-
siho kisiikizi*

60 Ivyo, wahina wakwe wekutegeezaho
mbui inu wakamba, "Mahinyo aya khayava
ni ndai adahae kuyahokea?"
61 Yesu akamanya kwesiho kugombekwa
ni mntu kuwa wahina wakwe nee
wang'ung'uzika kwa mbui iyo akawauza,
"Ivi mbui inu yawatenda muwe na maatu?

62 Yendaiwe viivihi mwendaho mmuone Mwana wa Mntu akakwea na kuita uwanga kwa Muungu kuda ekulawako?

63 Muye wa Muungu nee uetao ugima, mwii khauna udaho wakugosoa kintu. Mbui nekuwagombekazo zalawa kwa Muye wa Muungu na yaeta ugima.

64 Akini, wantu watuhu gatigati yenu khawazumiiya." Yesu kagombeka ivyo kwaviya kamanya kuvokea aho bosi, wada ambao khawana wamzumiye gatigati yao na yuda ambae enda amhituke.

65 Akatendesa kugombeka, "Kwaajii inu, nee nekuwambavyo kuwa khahana mntu adahae kweza hangu kwesiho kuongoewa na Tate yangu."

66 Kwaajii ya ayo, wahina wakwe wangi wekumtongeao Yesu, wakauya mgeeka, wasekutongeana nae vituhu.

67 Ivyo Yesu akawauza wada kumi dimwe na mbii, "Nanywi mwakunda kuhauka?"

68 Simoni Petulo akamtambaisa, "Zumbe tendatiite kwa ndai? Wee una mbui za ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi.

69 Swie tazumiiya na kumanya kuwa wee nee Klistu mwekusagulwae kulawa kwa Muungu."

70 Yesu akawauza, "Ivi ncheekuwasagua nywie kumi dimwe na mbii? Na yumwe aongoewa na Ibiisi."

71 Yesu kagombeka ayo kwaajii ya Yuda, mwana wa Simoni Isikaliote kwaviya uyu nee endaeamhituke, etiho ni yumwe da wada kumi dimwe na mbii.

# 7

*Yesu na wanduguze*

1 Yekwembokaho ayo, Yesu nee avoka kuzunguka kia hantu mwe mizi ya Galilaya, khekukunda kuita si ya Yudea kwaajii waongweezi wa Kiyahudi nee wakaondeza kumkoma.

2 Kisingi cha sikukhuu mwenga ya Wayahudi yetangwayo sikukhuu ya vikumbi nee iwa hehi.

3 Naho nduguze da Yesu wakamwamba, "Hauke aho uite si ya Yudea ili wahina wako wakaone ndima uzigosoazo.

4 Mntu khagosoa mbui kwa sii inga akakunda kumanyika kwa wantu, kwaviya wagosoa mbui izi, naho eambaze mwe inusi wantu ili wakumanye."

5 Naho ata wanduguze wagombeka ivyo kwaviya khawekumzumiiya.

6 Yesu akawamba, "Kisingi changu cha kuita uko Yelusalemu khakizati kubuwa, akini nywie mwadaha kuita kisingi chochose.

7 Wantu wa mwe inusi inu khawamiemea nywie, akini miye waniemea kwaajii nawavuhuzia kuwa wagosoa mafyaimi.

8 Nywie hitani kwe sikukhuu iyo, miye khina niite kwe sikukhuu iyo, kwaviya mda wangu ukundigwao khauzati kubuwa."

9 Yesu ekubindiizaho kugombeka ivyo, akasigaa uko Galilaya.

*Yesu kwe sikukhuu ya makumbi*

10 Wanduguze nee waongowa kuita kwe sikukhuu Yelusalemu, Yesu naye akaita, akini kwa sii.

11 Naho Waongoeezi wa Kiyahudi kisingi waaho mwe sikukhuu na kuwauza wantu, "Yu hahi mtu uyu?"

12 Hawa na mipokoso mingi mwe zumwezumwe da wantu, wamwe wakamba, "Ni mntu yedi." Watuhu wakamba, "Khivyo kwaviya awaza wantu."

13 Na ivyo khahana mntu mwekugeeza kugombeka mbui zakwe hewazo kwa kuogoha waongoezi wa Kiyahudi.

14 Sikukhuu iyo yekubuaho gatigati, Yesu nee aita he Nyumba ya Muungu, akavoka kuhinya.

15 Naho Wayahudi wakahondomaa na kugombeka, "Mntu uyu kamanya viivihi mbui izi kwesiho kuhinywa?"

16 Yesu akawatambaisa, "Mahinyo nihinyayo khio yangu, iya yalawa kwa Muungu mwekuniagiiya.

17 Mntu mkunda kugosoa yada akundayo Muungu, endaamanye mahinyo yangu yalawa kwa Muungu, hambu negombekea ni yamie mwenye.

18 Yee egombekeaye mwenye aondeza Ukuu mwenye, akini aondezae ukuu kwa yuda mwekuniagiiya, uyo agombeka yekuwayo kwei na khagombeka uhokho.

19 Ivi Musa khekuwekha miagiiyo ambayo kekhigwa ni Muungu? Na ivyo khahana katu mntu yumwe mtoza miko kwa mbwai mwaonda kunikoma?"

20 Aho wantu wakamtambaisa, "Wee una zaiko, nindai muondeza kukukoma?"

21 Yesu akawatambaisa, "Kuna mbui mwenga nekugosoayo nanywi yawahondomaza.

22 Musa nee kawaagiiya nywie kugwisa wana wenu wakigosi. Kugombeka kwei mbui iyo ivoka kwa mababa zenu, akini nywie mwawagwisa wana wenu ata Msi wa Kuhumwiiza.

23 Ikawa mntu adaha kugwiswa ata Msi wa Kuhumwiiza ili kuitoza miagiiyo ya Musa, kwambwai mwanikima kwaviya khihonya mntu Msi wa Kuhumwiiza?

24 Mwesekumuamuiya mntu kwa mbui zionekazo kwa chongoi, iya mumuamuiiye mntu kwa wedi na ikundigwavyo."

*Yesu nee Klistu Mwohozi?*

25 Wamwe wa wantu wa Yelusalemu nee
wagombeka, "Ivi, uyu khio yuda mntu ambae waongweezi wakunda kumkoma?
26 Mbona yuaha atamwiiya hemeso ya
wantu, naho khahana mntu agombekae
mbui yoyose! Ivi yadahika waongoeezi
wamanya kwei inga uyu nee Klistu?
27 Endahoeze Klistu Mwohozi, khahana
mntu endayeamanye hantu ekulawiako,
akini swie tamanya alawiako."
28 Aho Yesu ekuwaho akahinya he
Nyumba ya Muungu, akagombeka kwa
mgutio mkuu, "Inga mwanimanya,
uko nilawiako mwakumanya na ivyo
ncheekweza kwa udaho wangu iya ni yuda
mwekuniagiiya miye ni wa kwei, nywie
khamummanya,
29 akini miye nammanya kwaviya kilawiya kwakwe na yee nee mwekuniagiiya."
30 Naho, wantu nee wakaondeza kumgwiya akini khahana mwekudaha kumgwiya kwaviya mda wakwe nee khauzati
kubua.
31 Wantu wangi mwe dia zumwezumwe
da wantu nee wamzumiiya na kugombeka,
"Ivi, Klistu akeza endaagosoe ntangio vikuu
kusima ekugosoazo uyu?"

*Wagoji waagiiwa kumgwiya Yesu*

32 Mafalisayo wawategeeza wantu
wakapokosa mbui izo za Yesu, aho wowo
hamwe na waviki wakuu wakawaagiiya
wagoji wamgwiye.
33 Yesu akamba, "Nikeaho na nywie kwa
kisingi kijihi, nikabinda nendaniuye kwa
yuda mwekuniagiiya.
34 Mwenda mniondeze akini khamna
mnione na hada nendahoniwe, nywie
kwamdaha kubua."
35 Waongoeezi wa Kiyahudi wakauzana
wowo kwa wowo, "Mntu uyu enda aite
kuhi ambaho khatina tidahe kumuona?
Endaaite kwa Wayahudi wekuambazikao
gatigati ya Wagiiki na kuwahinya Wagiiki?
36 Ivi akunda kugombeka mbwai
agombekaho, mwenda mniondeze akini
khamna mnione na hada nendaho niwe
nywie khamdaha kubua."

*Vizigizigi vya mazi vietavyo ugima*

37 Msi wa kisiikizi wa sikukhuu iyo nee ni
msi maalum, Yesu akagooka, akagombeka
kwa mgutio mkuu, "Mtozwa ni khiu na eze
kwangu adomee mazi,
38 inga yagombekavyo Maandiko ya
Muungu, 'Mnizumiiya miye, vizigizigi vya
mazi ya ugima vyenda vimwamwaike kulawa mwe moyo wakwe.' "
39 Kagombeka ayo kuusu Muye kwa
wada wamzumiiao yee wendawamhokee,
kisingi icho Muye khazati kweza, kwa ivyo
Yesu nee khazati atogolwe.

*Kwepanga gati ya wantu mwe mbui ya Yesu*

40 Wantu watuhu he dia zumwezumwe
wategeeza mbui izo, "Kwei mntu uyu
Muoni."
41 Watuhu wamba, "Uyu nee Klistu."
Akini watuhu wamba, "Yadahika viivihi
Klistu akalawiiya mwe si ya Galilaya!
42 Maandiko ya Muungu yamba kuwa,
Klistu endaalawiiye he muango wa Seuta
Daudi, na endaavyaigwe Betilehemu mzi
ekuwao akekaa Daudi."
43 Nee kwalawiiya kwepanga kwaajii
yakwe he dia zumwezumwe da wantu.
44 Wantu watuhu nee wakoondeza
kumgwiya Yesu, akini khahana mntu
mwekugeeza kumgwiya.

*Waongoezi wa Wayahudi khawazumiiya Yesu*

45 Naho wada wagoji wakauya
kwa waviki wakuu na Mafalisayo na wakauzwa, "Kwa mbwai
khamwekumweeta Yesu?"
46 Wagoji wakawatambaisa, "Khahana
mntu ekulawiyae na kugombeka mbui
khuu inga mntu uyu!"
47 Mafalisayo wakawauza, "Ivi nywie
nanywi mtiiwa?"
48 "Ivi, mwammanya mwoongoezi
yoyose, hambu yumwe wa Mafalisayo
mwekumzumiiya mntu uyu?
49 Akini zumwezumwe da wantu
wamzumiiao, khawamanya miagiiyo ya
Musa, kubadiwa lazi na Muungu."
50 Yumwe yao kawa Nikodemo uyo
nee mwekumbasa Yesu na kio, naho nee
mwekugombeka.
51 "Miagiiyo tekwekhigwayo na Muungu
kwembokea Musa yatiemeza kumuamuiiya mntu kabla ya kumtegeeza na kumanya kia ekugosoacho."
52 Nawo wakamtambaisa, "Wee nawe kulawa si ya Galilaya? Ni vyedi, kayasunguumanye Maandiko ya Muungu nawe wendauone kuwa Galilaya khakulawa katu
muoni."
53 Naho wose wakahauka, kiya mntu
akaita kwakwe.

# 8

*Mvyee mwekutozwa ugoni*

1 Akini Yesu akaita he muima wa Mizaituni.
2 Kioi dakwe keokeo, Yesu nee aita vituhu
kwe Nyumba ya Muungu, wantu wose
wakambasa, nae akekaa akahinya.
3 Naho Wahinya wa miagiiyo na
Mafalisayo wakamweeteya mvyee yumwe
mwekutozwa heugoni, wakamgoosa
gatigati yawo.

4 Nee wamuuza, "Mhinyi!" "Mvyee uyu timbwiiya he ugoni.

5 Mwe miagiiyo yetu Musa katiagiiya mvyee inga uyu atoigwe maiwe adi auye na nyuma, tambe nawe wambaze?"

6 Wowo wagombeka ivyo, ili wapate mbui yendayoiwatende wamuahiye masa. Akini Yesu akenama na kuaandika asi kwa chaa.

7 Wekutendesaho kumuuza, Yesu akenuka akawamba, "Yumwe yenu mwesekuwa na mavigaviga na avoke kumtambikia iwe."

8 Naho akenama vituhu, na kuandika ahosi kwa chaa chakwe.

9 Wekutegeezaho ayo, wakavoka kuhauka yumweyumwe, wakaongoa wadaa, Yesu akasigaa ikedu kidege na yuda mvyee kagooka hadahada.

10 Yesu ekwenukaho akamuuza yuda mvyee, "Wahahi wada wantu? Ivi khahana katu ata yumwe mwekukuamuiiya?"

11 Uyo mvyee akamtambaisa, "Zumbe khahana ata yumwe!"

Na Yesu akamwamba, "Miye nami khinanikuamuiiye, hita na usekugosoa mavigaviga vituhu."

### *Yesu ni ung'azi wa inusi*

12 Yesu akatamwiiya nao vituhu, akawamba, "Mie nee ung'azi wa inusi, yoyose anibasae endaawe na ung'azi umuongoeae mwe ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi, naho khanaende mwe kiza katu."

13 Mafalisayo wakamwamba kwei Yesu, "Mbui zako wegombekea mwenye, ivyo khahana mntu akuvuhuziae mbui zako."

14 Yesu akawatambaisa, "Ata inga nevuhuzia mwenye, yada nigombekayo ni ya kwei, kwaviya namanya nilawako na niitako, akini nywie khammanya nilawako wala niitako.

15 Nywinywi mwaamuiiya wantu kwakuwakauwa viya wagosoavyo, akini mie khiamuiiya mntu.

16 Etiho nikaamuiiya, uwamuiiyo wangu ni kwei, kwa ivyo miye khio ikedu, Tate mwekuniagiiya yu hamwe na miye.

17 Iyandikwa mwe miagiiyo yenu, kuwa uvuhuzi wa wantu waidi, mbui iyo ni kwei.

18 Miye nevuhuzia mwenye na Tate mwekuniagiiya nae anivuhuzia."

19 Aho wakamuuza Yesu, "Tati yako yu hahi."

Yesu akawatambaisa, "Nywie khamnimanya miye naho khamummanya Tate, ati nee mkanimanya nee mkammanya na Tate."

20 Yesu kagombeka mbui izo mwe chumba cha kiikizo, ekuwaho akahinya kwe Nyumba ya Muungu, naho khahana mntu mwekumgwiya, kwaviya mda wakwe khauzati kubua.

### *Yesu awagombeka wantu mbui ya ufe wakwe*

21 Yesu akawamba vituhu, "Miye naita na nywie mwenda mniondeze, akini mwenda muuye na nyuma kwa mavigaviga yenu, niitako miye, nywie khamdaha kweza."

22 Waongoeezi wa Kiyahudi wakauzana, "Ivi endaekome mwenye? Kwambwai amba, niitako khamna mbue."

23 Yesu akawamba, "Nywie mlawa ahaaha asi, miye nalawa uwanga kwa Muungu, nywie ni wa mwe inusi inu, miye khio wa mwe inusi inu.

24 Nee mana nikawamba, 'mwenda muuye na nyuma he mavigaviga yenu mkesekuzumiiya kuwa miye nee mweaho ambae niaho mwenda muuye na nyuma kwa mavigaviga yenu.' "

25 Wowo wakamuuza Yesu, "Wee ni ndai?"

Yesu akawatambaisa, "Miye nee yuda nekuwagombekae aho bosi.

26 Ninayo mangi ya kugombeka na kuwamuiiya uwanga yenu, akini yuda mwekuniagiiya ni kwei nami nawamba wantu wainusi mbui ziyadu nekuzitegeezazo kulawa kwakwe."

27 Khawekuva ati Yesu kagombeka nawo kuusu Tati yakwe wa uwanga kwa Muungu.

28 Yesu akawamba, "Mwendaho mmwenue Mwana wa Mntu aho ndiho mwendaho mmanye, 'Mie nee uyo' na kuwa khigosoa chochose mie kwa udaho wangu akini nagombekadu yada Tate ekunihinyayo.

29 Yuda mwekuniagiiya yuhamwe namiye, yee khekunibada ikedu kwaviya nagosoa yada yamtamiayo misi yose."

30 Ekubindaho kugombeka ayo wantu wangi wakamzumiia.

### *Wahina wa kwei*

31 Yesu akawamba wada Wayahudi wamzumiiao, "Ati mkayatozeeza mahinyo yangu, mwendamuwe wahina wangu kwei.

32 Naho Mwenda mmanye kwei, kwasia ya ukwei uwo Muungu eza kuwaekea kulawa mwe utumwa."

33 Wowo wakamuuza, "Swie tiuvyazi wa Ibulahimu na khatizati katu kuwa watumwa wa mntu yawa viivihi ukamba tenda tiekewe?"

34 Yesu akawatambaisa, "Nawamba kwei kia mntu mgosoa mavigaviga ni mtumwa wa mavigaviga.

35 Mtumwa khana chekao cha kwekaa mwe nyumba, akini Mwana anacho chekao kisingi chose.

36 Inga Mwana akawaekea kulawa mwe utumwa wa mavigaviga, mwenda muwe muekewa kweikwei.

37 Namanya nywie ni muango wa Ibulahimu, na ivyo mwaondeza kunikoma kwaviya muyaemea mahinyo yangu.

38 Miye nagombeka ekunionyeshayo Tate, akini nywie mwagosoa yada yekugombekwayo na Tati yenu."

39 Wowo wakamtambaisa, "Swie tiwana wa Ibulahimu."

Yesu akawamba, "Inga nywie ni wana wa Abulahamu, nee mkagosoa inga yada ekugosoayo Abulahamu.

40 Nawamba ukwei, nekuutegeezao kwa Muungu, na ivyo nywie mwaondeza kunikoma, Ibulahimu khekugosoa ivyo.

41 Nywie mwagosoa mbui ziyaziya ekugosoazo tati yenu."

Wowo wakamwamba, "Swie khio wanahalamu na tinae Tate yumwedu na nee Muungu yetu!"

42 Yesu akawamba, "Inga Muungu nee tati yenu nee mkanikundisa, kwaviya miye nalawa kwa Muungu isasa niaha, ncheekweza kwa udaho wangu mwenye, iya yee Muungu mwekuniagiiya.

43 Kwa mbwai khamva ayo nigombekayo? Kwaviya muemea kutegeeza mbui yangu.

44 Nywie ni wana wa tati yenu Ibiisi mwaondeza kugosoa mbui akundazo tati yenu. Yee kawa mkomaji kuvokea aho bosi, wala khekugooka mwe ukwei, kwaviya kwei khaimo umo mwakwe. Kia agombekaho uhokho, agombeka uhokho kwaajii nee eivyo, kwaviya yee ni mhokho na tate wa uwo uhokho.

45 Akini mie nagombeka ukwei, nee kiekacho nywie msekunizumiiya.

46 Yuhi gatigati yenu adahae kumanya ati mie nina mavigaviga? Ati nagombeka ukwei kwa mbwai khamnizumiiya?

47 Mntu wa Muungu ategeeza mbui za Muungu akini nywie khamtegeeza, ivyo nywie khio wantu wa Muungu."

*Yesu na Ibulahimu*

48 Wayahudi wakamtambaisa Yesu, "Uwo khatekugombeka ukwei ati wee umsamalia naho una zaiko?"

49 Yesu akawatambaisa, "Mie khina mazaiko, mie namtegeeza Tate, iya nywie khamnitegeeza mie.

50 Miye khiondeza wantu wanitunye akini yuaho akundae wantu wanitunye na yee nee mwaamua inga nagosoa ikundigwavyo.

51 Kwei nawamba, mwekutozeeza mbui zangu khana auye na nyuma kisingi chose."

52 Aho Wayahudi wakamba, "Isasa tamanya kwei kuwa wee una zaiko! Ibulahimu kauya na nyuma, Waoni nawo wauya na nyuma, wee wamba mtozeeza mbui zangu khana auye na nyuma kisingi chose.

53 Ivi wetenda umkuu kusima tati yetu Ibulahimu mwe kuuya na nyuma? Na waoni nawo wauya na nyuma, asa wee wetenda kuwa undai?"

54 Yesu akawatambaisa, "Inga nikefena mwenye, kwetogoa kwangu ni bue. Akini tate yangu uyo mgombekaye nee Muungu yenu, nee anitogoae.

55 Nywie khamzati kummanya akini mie nammanya, nikamba khimmanya nendaniwe mhokho inga nywinywi, mie nammanya na natoza mbui yakwe.

56 Baba yenu Ibulahimu kawa na nyemi muno kumanya kuwa miye nendaneze. Neekawa inga kaniona, nee kawa na nyemi muno."

57 Aho Wayahudi wakamwamba, "Wee khuzati kubuza myaka makumi mashano nawe kumwona kuhi Ibulahimu?"

58 Yesu akawamba, "Kwei nawamba kisingi Ibulahimu khazati kuvyaigwa, 'Mie nee Niuko.' "

59 Aho wakadoa maiwe ili wamtambikie, akini Yesu akefisa akalawa kwe Nyumba ya Muungu.

# 9

*Yesu amhonya mntu mwekuvyaigwa tuntu*

1 Yesu ekuaho akemboka, akamuona mntu yumwe mwekuvyaigwa tuntu.

2 Aho, wahina wakwe wakamuuza, "Mhinya! Ni yuhi mwekugosoa mavigaviga, mntu uyu hambu wavyazi wakwe ata avyaigwe tuntu?"

3 Yesu akawatambaisa, "Mbui inu khayokulawiiya kwaajii ya mavigaviga yakwe wala mavigaviga ya wavyazi wakwe, iya kavyaigwa tuntu ili udaho wa Muungu uoneke ukagosoa ndima umo mwakwe.

4 Kukawa kuke musi takundigwa titendese kugosoa ndima za yuda mwekuniagiiya, mana kio cheza mntu khadaha kugosoa ndima.

5 Kisingi nike mwe inusi, mie ni ung'azi wa inusi."

6 Ekubindaho kugombeka ayo, akaswa ovu ahosi, akagosoa ntope kwa dia ovu, akamsisa yuda tuntu he meso.

7 Akamwamba, "Hita ukesunte cheni he tondoo da mazi da siloamu" mana ya zina idi ni mwekuagiiwa, aho yuda tuntu akaita, akesunta akauya uku aona.

8 Naho wahehi yakwe, na wada wekuwao wakammanya aho bosi kawa mkiwa mwekuwa akaombeza, wakamba,

"Ivi, uyu khie yuda mkiwa mwekuwa
akekaa na kuombeza?"
9 Wamwe wao wakamba, "Ndie." Watuhu
wakamba, "Khio iya waigana nae."
Akini yuda ekuae khaona akamba "Ni
miye."
10 Nae wakamuuza "Isasa meso yako
yadaha vivihi kugubuka?"
11 Naye akawatambaisa, "Yuda mntu
etangwae Yesu, kagosoa ntope akanisisa
mwe meso na kunamba, hita ukesunte he
tondoo da siloamu, aho nee naita nike-
sunta nikadaha kuona."
12 Wakamuuza, "Yee yu hahi?"
Akawatambaisa, "Mie khimanya."

*Mafarisayo wamuuza yuda ekuwae tuntu*

13 Nee wamwegaa yuda mntu
mwekuwae tuntu kwa mafalisayo.
14 Msi uwo Yesu ekugosoaho ntope na
kumgubua meso mntu uyo iwa Msi wa
Kuhumwiiza.
15 Naho mafalisayo wakamuuza mntu
uyo, "Kudaha viivihi kuona? Akawamba
kanisisa ntope mwe meso, nami nikesunta,
na isasa naona."
16 Wamwe wa Mafalisayo wakamba,
"Mntu uyu khee kulawa kwa Muungu
mana khatoza miagiiyo ya Msi wa
Kuhumwiiza."
Akini watuhu wakamba, "Mntu mwenye
mavigaviga adaha kugosoa viivihi utangio
inga unu?" Ivyo Mafalisayo khawekwe-
vana wowo wenye.
17 Wakamuuza vituhu yuda mwekuwa
tuntu, "Kwa kuwa kakugubua meso
wambaze uwanga ya mntu uyo?"
Nae akawamba, "Yee ni Muoni wa
Muungu."
18 Waongoezi wa Kiyahudi khawekumzu-
miiya ati mntu uyo nee kawa tuntu aho
bosi, na isasa aona, adi wekuwetangaho
wavyazi wakwe.
19 Aho, wakawauza, awo wavyazi, "Uyu
ni yuda mwana yenu mwekugombekae
kavyaigwa tuntu? Kadaha viivihi kuona?"
20 Wavyazi wakwe wakatambaisa,
"Tamanya uyu ni mwana yetu na
kavyaigwa tuntu.
21 Akini kadaha viivihi kuona, kha-
timanya, nahodu khatimmanya yuda
mwekumgubwiiya meso, muuzeni yee
mwenye ni mntu mgima adaha ku-
gombeka yee mwenye."
22 Wavyazi wakwe wamba ivyo kwa
kuwaogoha waongoeezi wa Kiyahudi, kwa
kuwa waongoeezi awo wevana kae, kuwa
mntu yoyose agombeke Yesu nee Klistu,
endaaguuswe he Nyumba ya kukintania
Wayahudi.
23 Nee mana wavyazi wakwe wakamba,
"Yee ni mntu mgima muuzeni."
24 Naho wakamwetanga vituhu
yuda mwekuwa tuntu, wakamwamba,
"Gombeka ukwei mwekhe Muungu Ukuu
swie tamanya ati mntu uyu ni mwenye
mavigaviga."
25 Yee akatambaisa, "Ati ni mwenye mav-
igaviga miye khimanya, akini kintu kimwe
nakimanya, cheekuwa nikaona, na isasa
naona!"
26 Aho wakamuuza, "Kakugosweea mb-
wai? Ayo meso yako kayagubua viivihi?"
27 Uyo mntu akawatambaisa, "Khiwamba
kae na nywie khamwekunitegeeza, kwa
mbwai mwakunda kutegeeza vituhu? Ivi,
mwakunda na nywie mtende wahina
wakwe?"
28 Akini wowo waongoezi wa Wayahudi
wakamdumua, wakamba, "Wee nawe ni
mhina wakwe, akini swie ni wahina wa
Musa.
29 Swie tamanya kuwa Muungu
kagombeka na Musa, akini mntu uyu
khatimmanya kalawiiya kuhi."
30 Naye akatambaisa, "Inu ni mbui
ya kuhondomaza! Nywie khammanya
kalawiiya kuhi, akini kanigubua meso
yangu!
31 Tamanya kuwa Muungu khawa-
tegeeza wantu wenye mavigaviga, iya
amtegeeza yoyose, mwenye hofu ya
kumwogoha Muungu na kugosoa viya
akundayo.
32 Kuvokea aho bosi wa inusi, khatizati
kutegeeza kuwa mntu kamhonya yoyose
ekuwae tuntu.
33 Inga mntu uyu kheekulawa kwa
Muungu kheekuwa adahe kugosoa cho-
chose."
34 Wowo wakamtambaisa, "Wee ku-
vyaigwa na kweewa he mavigaviga
wadaha viivihi kutihinya swie?" Aho
wakamguusa he Nyumba ya kukintania
Wayahudi.

*Waongoezi wa Wayahudi khawammanya Klistu*

35 Yesu ekusikiaho kuwa wamguusa
mntu uyo he Nyumba ya kukintania
Wayahudi, akaita kumuondeza. Kisingi
ekumbwiiaho akamuuza, akamba "Ivi wee
wamzumiiya Mwana wa Mntu?"
36 Uyo mntu akamtambaisa, "Mkuu nam-
biya ni ndai, nidahe kumzumiiya."
37 Yesu akamwamba, "Kumwona kae na
nee agombekae nawe isasa."
38 Aho uyo mntu akamba, "Zumbe, Nazu-
miiya" akamkintia mavindi na kumvikia.
39 Yesu akamba, "Miye ncheza mwe inusi
kwaajii ya kuwekha sugusa wantu, ili
wantu wada wesaokuona wadahe kuona

na wamamaakhanyao waona, wesekudaha kuona."

40 Wamwe wa Mafalisayo wekuwao hamwe nae, nee wasikia mbui izo wakamuuza, "Tambe swie ni matuntu?"

41 Yesu akawatambaisa, "Ati nee nimatuntu, neekhamwekuwa na mavigaviga, akini isasa nywie mwamba, 'Swie taona,' na iyo yaonyesha ati mke na masa."

# 10

*Msimo wa muisi yedi*

1 Yesu akawamba, "Nawamba ukwei, yoyose yuda mwesaekwengia mwe dewa da ngoto kwa kwembokea he uvi, iya ahenya na kwengia sia ntuhu, uyo ni mbavi na mhokaji.

2 Akini mwengia kwa kwembokea he uvi wa dewa, uyo nee muisi wa ngoto.

3 Mgoji wa dewa amvugwiiya, na ngoto ava mgutio wakwe, na awetanga ngoto zakwe kia yumwe kwa zina dakwe, na kuwalavya chongoi.

4 Akabinda kuwalavya chongoi, aziongweeya na awo ngoto wamtongea, kwaviya waumanya mgutio wakwe.

5 Ngoto izo khazidaha kutongea muisi mgeni, iya wendawamguuke kwaviya khawamanya mgutio wakwe."

6 Yesu akawamba msimo uwo akini wowo khawekumanya ekukundavyo kuwamba.

*Yesu muisi yedi*

7 Yesu akagombeka vituhu, "Kwei nawamba, miye ni uvi wa ngoto.

8 Wada watuhu wose wekuniongweeao miye ni wabavi na wahokaji, akini ngoto khawekuwategeeza.

9 Miye ni inga uvi, mntu yoyose mwengia kwembokea kwangu endaaoholwe, endaengiye na kulawa chongoi na endaapate kia akundacho.

10 Mbavi eza kwa kuondeza kubawa na kukoma, na kubananga. Miye ncheza ili muwe na ugima, naho wawe nao mwingi.

11 "Miye ni muisi yedi. Muisi yedi ni yuda azumiiyae kuulavya ugima wakwe kwaajii ya ngoto zakwe.

12 Mntu agosoae ndima ya kibauwa cha kuisa ngoto ili ekhigwe hea naho ngoto khio mai yakwe, aonaho kui da mzituni dikeza, abada ngoto na kuguuka, naho kui da mzituni dawagwiya na kuwamwaganisa.

13 Yee khapatiiza kintu kuusu ngoto, kwaviya yee ni mkibauwa apatiiza kuihwa hea.

14 Miye ni muisi yedi wada wakwangu nawamanya, na wakwangu wanimanya.

15 Inga Tate animanyavyo, ivyoivyo na miye nammanya Tate, miye nazumiiya ata kuulavya ugima wangu ili ngoto wasekwaga.

16 Naho ninao ngoto watuhu, awo khawamo mwe dewa dangu, awo nakundigwa kuwaeta, naho wenda wategeeze mgutio wangu, kwenda kuwe na tintimo dimwe na muisi yumwe.

17 "Tate anikundisa kwaviya miye mwenye naulavya ugima wangu, ili nidahe kuwa na ugima vituhu.

18 Khahana mntu mnihoka ugima wangu, miye naulavya kwa kukunda kwangu mwenye. Ninao udaho wa kuulavya na udaho wa kuudoa vituhu, mwiko unu nee Tate ekunigombekavyo nigosoe."

19 Wekusikiaho mbui izo kukalawiiya kwepanga vituhu gatigati ya Wayahudi.

20 Wangi wao wakamba, "Ana zaiko uyu, naho ni mkiau! Kwa mbwai kumtegeeza?"

21 Wantu watuhu wakamba, "Izi khizo mbui za mntu mwenye zaiko, kwaani zaiko dadaha kugubua meso ya matuntu?"

*Yesu aemewa na Wayahudi*

22 Uko Yelusalemu nee kuwa na sikukhuu ya kuvugua Nyumba ya Muungu, kisingi icho kiwa cha pheho.

23 Yesu nae kawa akenda he Nyumba ya Muungu he ukumbi wa Selemani.

24 Wayahudi wakamuikia bunga wakamuuza, "Watibada mwemamaakhanyi adi ini? Ati wee ni Klistu isasa tambie ukwei."

25 Yesu akawatambaisa, "Khiwagombeka kae akini khamwekuzumiiya, ndima nizigosoazo ni kwa udaho wa zina da Tate yangu zanivuhuzia.

26 Akini nywie khamzumiiya, kwaivyo nywie khio ngoto zangu.

27 Ngoto zangu zategeeza mgutio wangu, miye nawamanya, nawo wanitongea.

28 Miye nawekha ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi, naho khawana wage kisingi chose, wala khahana mntu mdaha kuwadoa kulawa hangu.

29 Tate yangu nee mwekunekha awo, ni mkuu kusima wose, naho khahana mntu mdaha kuwadoa he mikono ya Tate.

30 Miye na Tate ni kintu kimwe."

31 Wayahudi wakadoa maiwe wamtambikie ili wamkome.

32 Yesu akawamba, "Khiwaonyesha ndima nyingi zilawazo kwa Tate, ni kihi icho kimiekacho mnitoe maiwe?"

33 Wayahudi wakamtambaisa, "Khatikutoa maiwe kwaajii ya ndima ntana, iya ni kwa kumkufuu Muungu! Kwaviya wetenda u Muungu ikawa wee ni mntu du inga wantu watuhu."

34 Yesu akawatambaisa, "Iyandikwa mwe miagiiyo yenu kuwa, Muungu kagombeka, 'Nywie ni miuungu.'

35 Muungu kawetanga *miiuungu wada wekwekhigwao mbui zakwe, tamanya kuwa Maandiko ya Muungu yagombeka ukwei misi yose.

36 Ivi, mwadaha viivihi kumwamba yuda ambae Tate akamuika kwaajii ya ndima yakwe na kumwagiiya mwe inusi adumuwa? Ivi ni kwaviya khigombeka miye ni Mwana wa Muungu?

37 Inga khigosoa ndima za Tate yangu, msekunizumiiya.

38 Akini ati nazigosoa ndima za Tate yangu, ata inga khamnizumiiya, naho zizumiieni ndima izo, ili mdahe kummanya kuwa Tate yuumu mwangu na miye niumo mwakwe."

39 Wakageeza vituhu kumgwiya, akini akahauka gatigati yao.

40 Yesu akaita khandakhanda ya zigizigi da mazi ya Yolodani, hantu Yohana ekubatiizaho, akekaa uko.

41 Wantu wangi wakambasa wakamba, "Yohana kheekugosoa ntangio yoyose, akini mbui zose za Yesu zia ekugombekazo Yohana neziwa za kwei."

42 Wantu wangi wekuwaho hantu hada, wakamzumiia Yesu.

# 11

*Ufe wa Lazalo*

1 Mntu yumwe etangwae Lazalo, mwenyezi wa Besania, nekawa mtamu. Mntu uyo neakekaa mwe phaamo ya Besania ekuwayo akekaa Maliamu na umbude da Yesu.

2 Maliamu nee yuda mwekumsisa Zumbe mavuta ya mzingo mtana na kumhangusa kwa fii zakwe, Lazalo, kakie nee mwekua mtamu.

3 Ivyo awo waumbude Lazalo, Malia na Masa wakaagiiya mbui inu kwa Yesu "Zumbe, mbuyayo umkundisae ni mtamu."

4 Yesu ekusikiaho ivyo akamba, "Utamu unu khio wa ufe iya wendauwatende wantu wamtogoe Muungu na kwa sia iyo, Mwana wa Muungu viyaviya endaatogolwe."

5 Yesu kawakundisa muno Masa na Malia maumbude da na Lazalo.

6 Yesu ekwembigwaho Lazalo ni mtamu, Yesu akaendeea kwekaa hantu aho ekuaho kwa misi miidi.

7 Naho akawamba wahina wakwe, "Titeni vituhu mwe si ya Yudea."

8 Wahina wakwe wakamwamba, "Mhinyi! Kisingi kijihi chekwembokacho tangia Wayahudi wekukundaho kukukoma kwa maiwe, nawe waonda ukuite uko vituhu?"

9 Yesu akawamba, "Ivi saa za musi khio kumi dimwe na mbii? Naho mntu akenda musi khadaha kwekungwaa kwaviya aona ung'azi wa zua mwe inusi.

10 Akini mntu akenda na kio, ekungwaa kwaviya ung'azi khaumo umo mwakwe."

11 Yesu ekubindaho kugombeka mbui izo, akawamba, "Mmbuya wetu Lazalo kagona akini miye naita nikamwenue."

12 Wahina wakwe wakamwamba, "Zumbe, inga kagona usisiza, endaenuke."

13 Wowo wamamakhanya kuwa kagona usisiza, akini Yesu kamanya kae ati Lazalo kauya na nyuma.

14 Yesu akawamba pwii, "Lazalo kauya na nyuma,

15 akini natamiwa kwaviya nchekuwa uko ekuuyaho na nyuma Lazalo, ili mdahe kunizumiiya, aya titeni kwakwe."

16 Tomaso yuda mwetangwa phasa akawamba wahina weziwe "Titeni na swie tiuye na nyuma hamwe nae!"

*Yesu nee ayuyusaye wantu na kuwekha ugima*

17 Yesu ekubuaho uko, akabwiiya Lazalo kagewa kae mwe mbiya kwa misi mine.

18 Phaamo ya Besania neiwa hehi, na Yelusalemu uhae ubuwao kilomita ntatu.

19 Wayahudi wangi waita kwa Masa na Malia kuwahongeza kwa ufe wa kaka yao.

20 Naho Masa ekusikiaho Yesu eza, akenda kumhachiiza, akini Malia kasigaa kaya.

21 Masa akamwamba Yesu, "Zumbe ati nekuwa aha, kaka yangu kheekuwa auye na nyuma.

22 Akini namanya isasa chochose wendacho umuombeze Muungu, endaakwekhe."

23 Yesu akamwamba, "Kakio endaayuyuke na kuwa mgima vituhu."

24 Masa akatambaisa "Namanya endaayuyuke kisingi wantu wendaho wayuyuswe, msi wa kisiikizi."

25 Yesu akamwamba, "Miye nee niwayuyusae wantu na kuwekha ugima na mntu yoyose anizumiiyae ata inga kauya na nyuma, endaawe na ugima.

26 Na mntu yoyose ekaae na kunizumiiya kisingi chose khana auye na nyuma katu, ivi wayazumiiya ayo?"

27 Masa akamtambaisa, "Eehe Zumbe miye nazumiiya ati wee nee Klistu Mwana wa Muungu yuda ezae mwe inusi."

*Yesu aiya mesozi*

28 Ekugombekayo ayo, Masa akenda kumwetanga Malia umbude, akampokosa he ikedu, "Mhinyi yuaha akwetanga."

29 Maliamu ekusikiaho ayo, akenuka kinyio akambasa Yesu.

* **10:35 10:35** Miuungu hanu ina mana wantu wose wa Isilaeli

30 Yesu nee khazati kwengia mwe
phaamo akini kawa hadahada Masa
ekumhokeaho.
31 Aho, Wayahudi wekuwao hamwe na
Malia kwa kumhongeza wamwona enuka
na kulawa chongoi kinyio wakambasa,
wakimamaakhanya kuwa enda kuiya kwe
mbiya.
32 Naho Malia ekubuaho hantu Yesu
ekuaho nakumuona, akakinta mavindi
akamwamba "Zumbe inga nekuwa aha
kaka yangu kheekuwa akauya na nyuma."
33 Yesu ekumuonaho aiya, wada
wayahudi wekwezao hamwe naye wose
wakaiya, akengiwa ni mbazi na kug-
widukwa moyo.
34 Yesu akawauza "Mmwika hahi?"
Wakamtambaisa, "Zumbe soo ukauwe."
35 Yesu nee aiya.
36 Wayahudi wakamba, "Kauwani
ekumkundisavyo Lazalo!"
37 Wantu watuhu wakamba, "Ivi nee
yuda mwekumgubua meso yuda tuntu?
Isasa khekudaha kumtenda Lazalo aseku-
uya na nyuma?"

*Yesu amyuyusa Lazalo*

38 Naho Yesu akawa na usungu vituhu
mwe moyo wakwe, akaita he mbiya. Mbiya
denye nediwa phanga, nado digubikwa
kwa iwe kuu.
39 Yesu akawamba, "Usani ido iwe!"
Masa umbude da uyo mwekuuya na
nyuma akamtambaisa Zumbe, "Kwaviya
kekaa mwe mbiya misi mine isasa kavoka
kae kunukha!"
40 Yesu akawamba, "Ivi ncheekukwamba
inga ukanizumiiya wendauuone ukuu wa
Muungu?"
41 Wakadiusa dia iwe, Yesu akakauwa
uwanga kwa Muungu akamba, "Nakutogoa
Tate kwaviya wanitegeeza uviki wangu.
42 Namanya inga wanitegeeza kia msi,
akini nagombeka aya kwaajii ya wantu
awa weaha wadahe kuzumiia ati wee nee
mwekuniagiiya"
43 Ekubindaho kugombeka ayo, aketanga
kwa mgutio mkuu "Lazalo, lawa chongoi!"
44 Lazalo akalawa chongoi, uku
kazengetezwa sanda mwe mwii wakwe,
miundi na mikono ifungwa na cheni
chakwe kigubikwa leso, Yesu akamba,
"Mchopoeni mmweeke aite."

*Nteganyi ya kumkoma Yesu*

*Matayo 26:1-5; Maliko 14:1-2; Luka 22:1-2*

45 Ivyo wayahudi wangi wekwezaho kwa
Malia yekuonaho mbui ida ekugosoayo
Yesu wakamzumiia.
46 Akini watuhu wakaita kwa Mafalisayo
na kuwagombeka mbui ida ekugosoayo
Yesu.
47 Kwa ivyo, waviki wakuu na mafal-
isayo wakawetanga waongoezi wakuu wa
Wayahudi wa mkonga na kugombeka "Ti-
tende viivihi? Mntu uyu agosoa ntangio
nyingi.
48 Inga tikamwekea aendeee, wantu
wose wendawamzumiiye, na awo Wa-
lumi wendaweze waibanange Nyumba ya
Muungu na kuwakoma wantu wa si yetu!"
49 Yumwe yawo etangwae Kayafa, yuda
mwekuwa Mviki Mkuu kwa mwaka uda,
akawagombeka "Nywie khammanya kintu!
50 Khammanya ati ni vyedi kumkoma
mntu yumwe kwaajii ya wantu, kusima
wantu wose wa si ngima wadagamiye?"
51 Kheekugombeka akundavyo mwenye,
kwaviya kawa Mviki Mkuu kisingi icho,
nee kamanya Yesu endaauye na nyuma
kwaajii ya si yawo,
52 na khio kwaajii ya si iyo ya Wayahudi
iya ni kwaajii ya wantu wa Muungu
wekumwaganikao ili kuwaeta hamwe na
kuwatenda kuwa kintu kimwe.
53 Nee kuvokea msi uwo, waongoezi wa
Kiyahudi wakaondeza kintu chendacho ki-
watende wamkome Yesu.
54 Ivyo Yesu khekuita vituhu hemeso ya
Wayahudi iya akalawa aho, akaita hehi
na kiwawe, he mzi wetangwao Eflaimu,
akekaa uko hamwe na wahina wakwe.
55 Sikukhuu ya Wayahudi ya pasaka iwa
hehi na wantu wangi wakaita Yelusalemu
wadahe wezingue hemeso ya Muungu
kabla ya sikukhuu iyo.
56 Wantu nee wakamuondeza Yesu,
nawo wekukintanaho hantu he Nyumba
ya Muungu wakauzana, "Ivi mntu uyu
khanaeze he sikukhuu?"
57 Waviki wakuu na Mafalisayo nee
walavya miko kuwa mntu akamanya
hantu Yesu eiho, awatonye wadahe
kumgwiya.

# 12

*Maliamu amwetiiya Yesu mavuta*

*Matayo 26:6-13; Maliko 14:3-9*

1 Misi mtandatu nee khaizati sikukhuu
ya Pasaka, Yesu akaita Besania ekuwako
akekaa Lazalo, yuda ambae Yesu
ekumyuyusaye.
2 Uko wakamuiikia khande ya guoni,
Masa nee mwekuwa akawagosweea
ndima, na Lazalo kawa yumwe wa wada
wekuwao wekaa hamwe na Yesu.
3 Aho, Malia akadoa hindi ya mavuta ya
mzingo mtana yekugosolwayo na nalido na
ya yombe khuu, akamwetiiya Yesu mwe
miundi na kumhangusa kwa fii zakwe,
nyumba yose ikamema mzingo mtana wa
mavuta.

4 Yuda wa Isikaliote, yumwe wa wada wahina kumi dimwe na mbii nauyo nee mwenda amhituke Yesu akamba,

5 “Kwa mbwai ayo mavuta yenye mzingo mtana yasekutagwa kwaviya nee tikadaha kupata hea za kuiha mtu maiho yakwe ya mwaka mgima na hea iyo tikawekha wakiwa?”

6 Kagombeka ivyo, khio kwa kuwaonea mbazi wakiwa, iya kwaajii yee nekawa na mkwiji wa hea na nee mbavi. Maa kwa maa nee akadoa hea na kuzida ikedu.

7 Naho Yesu akagombeka, “Mwesekumpisha mvyee uyu! Kwaviya kanetiiya mavuta aya kwaajii ya msi wangu wa kugewa mwe mbiya.

8 Wakiwa mnawo misi yose, akini miye khamna muwe nami misi yose.”

*Nteganyi ya kumkoma Lazalo*

9 Wayahudi wangi wasikia Yesu kawa Besania, ivyo wakaita uko khio kwaajii ya Yesu iya kumuona Lazalo yuda ekuyuyuswae na Yesu.

10 Viyaviya waviki wakuu wakagosoa nteganyi ya kumkoma Lazalo,

11 kwaajii ya kuyuyuswa kwa Lazalo, Wayahudi wangi wakawahituka waongoezi wao, wakamzumiia Yesu.

*Yesu engia Yelusalemu kwa nyemi khuu*

*Matayo 21:1-11; Maliko 11:1-11; Luka 19:28-40*

12 Kioi dakwe zumwezumwe khuu da wantu wakeza kwe sikukhuu, wasikia Yesu kawa siai eza Yelusalemu.

13 Nee wadoa matambi ya mitende madodo dodo, wakalawa kwa kumhachiiza, wakatoa mgutio wakamba, “Ntunyo! Ajaiwe uyo mweza kwa udaho wa zina da Zumbe, ajaiwe Seuta wa Isilaeli!”

14 Yesu nekapata mwanaphunda akamkwea uwanga inga viya yekuandikwavyo mwe Maandiko ya Muungu,

15 “Mwesekuogoha ee wantu wa mzi wa Sayuni!
Kauwa Seuta wenu eza,
Kakwea mwana phunda.”

16 Kisingi icho wahina wakwe khawekuzimanya mbui izo, akini Yesu ekutogolwaho, nee wakumbuka Maandiko yekuandikwayo uwanga yakwe na wantu wamgosweeya ivyo.

17 Zumwezumwe da wantu wekuwao hamwe na Yesu kisingi ekumwetangaho Lazalo kulawa mwe mbiya, na kamyuyusa kulawa kwa wekufao nee wa mvuhuzia.

18 Kwa ivyo zumwezumwe ido da wantu, wakamhachiiza kwaviya wose wasikia ntangio iyo, kuwa Yesu kamyuyusa Lazalo.

19 Mafalisayo wakaambizana “Mwaona khatidaha kugosoa chochose vituhu! Kauwani inusi ngima wantu wose wamtongea yee!”

*Wamwe wa Wagiiki wakunda kumwona Yesu*

20 Nekuwa na Wagiiki wekuawo wabua Yelusalemu kuvika kisingi cha sikukhuu ya pasaka.

21 Awo wakamtimia Fiipo mwenyezi wa Betisaida wa mzi wa Galilaya, wakamba, “Mkuu taombeza kumwona Yesu.”

22 Fiipo akaita akamwamba Andulea, aho wose waidi wakaita kumwamba Yesu.

23 Yesu akawamba, “Saa ya kutogolwa muno miye Mwana wa Mntu ibua.

24 Nawamba ukwei, mbeyu ya ngano yasigaa mbeyu ikesekugwa, akini ikagwa ahosi na kufa, ati ikafa, aho yavyaa matunda mangi.

25 Mntu yoyose akundisae ugima wakwe endaawaze, akimae ugima wakwe mwe inusi, endaauike kwaajii ya ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi.

26 Mntu akundae kunigosweeya ndima akundigwa anitongee, ili awe na miye kia hantu niitako, viyaviya mntu akanigosoeya ndima, Tate yangu endaamwekhe ntunyo.

*Yesu agombeka mbui ya ufe wakwe*

27 “Isasa moyo wangu wasuumia muno, nigombeke mbwai? Ivi nigombeke, ‘Tate, nakuombeza unihonye kisingi iki cha masuumizo?’ Khivyo khidaha kugombeka akini ni kwaajii ya ayo nee kiekacho nibwiiye mda unu.

28 Tate, uditogoe zina dako!”

Aho ukalawa mgutio kulawa uwanga kwa Muungu ukamba, “Khiditogoa zina dako na nendaniditogoe vituhu.”

29 Akini zumwezumwe da wantu wekuwao hantu hada wasikia mgutio uwo, nawo wakagombeka, uwo ni mgutio wa tuntumo, na wantu watuhu wakamba, “Mndima wa uwanga kwa Muungu katamwiiya na Yesu!”

30 Yesu akawamba, “Mgutio uwo utegeezeka khio kwaajii yangu, iya ni kwaajii nywie mumzumiiye Muungu.

31 Isasa ni kisingi cha inusi kuamuiiwa, mkuu wa mwe inusi endaasigwe chongoi.

32 Nendaho nenulwe uwanga kulawa mwe inusi, nendaniwetange kia yumwe eze kwangu.”

33 Kwa kugombeka ivyo, Yesu kamanya endaauye na nyuma viivihi.

34 Naho zumwezumwe ido dikamtambaisa, “Swie tisoma mwe Miagiiyo kuwa uyo Klistu endaekae kisingi chose kwesiho kisiikizi, wadaha viivihi kugombeka Mwana wa Mntu akundigwa enulwe? Uyo Mwana wa Mntu ni ndai?”

35 Yesu akawamba, “Un'gazi wendauwe na nywie kwa mda mjihi, endani mke na

uwo un'gazi ili kiza kisekuwavota, kwaviya endae na kiza khamanya aitako.

36 Kisingi mke na uwo ung'azi, uzumiiye ili mdahe kuwa wantu wa ung'azi."

*Wantu khawazumiiya*

Yesu ekugombekaho mbui izo akenda kwefisa hae nawo.

37 Etiho Yesu kagosoa ntangio vyose hemeso yawo, wowo khawekumzumiiya,

38 Inu neiwa ili kuiganiza ida mbui yekugombekwayo na Muoni wa Muungu Isaya,

"Zumbe ni ndai mwekuzumiia mbui zetu?
Naho Zumbe kumgubuiya ndai udaho wakwe?"

39 Ivyo khawekudaha kumzumiia Yesu, kwaviya Muungu kagombeka hantu hatuhu kwembokea muoni yakwe Isaya,

40 "Muungu kawatenda wasekuona,
Kawatenda wasekuva kwa mioyo yao,
Wasekukauwa kwa meso yawo,
Wasekumanya kwa akii zawo,
Naho wasekunihitukia,
Ili nidahe kuwahonya, agombeka Zumbe."

41 Isaya kagombeka mbui izi kwaajii ya ukuu uwo wa Yesu, akamba mbui zakwe.

42 Na ivyo waongoezi wangi wa kiyahudi wamzumiiya Yesu, akini khawekugombeka pwii kuwa wamzumiiya kwa kuogoha kuguuswa mwe Nyumba ya kukintania Wayahudi.

43 Waongoezi awo wa Wayahudi nee wakakundisa muno kutunywa ni wantu kusima kutunywa na Muungu.

*Yesu keza kuohowa wantu wa inusi*

44 Naho Yesu akagombeka kwa mgutio mkuu, "Mntu mnizumiiya miye, khanizumiiya miye du, iya amzumiiya viyaviya yuda mwekunigiiya.

45 Mwekuniona miye kamuona yuda mwekuniagiiya.

46 Miye ni ung'azi, nami ncheza mwe inusi, ili wose wamzumiiao wasekusigaa mwe kiza.

47 Mntu yoyose ategeezae mbui zangu akini khazitozeeza, miye khinanimuamwiiye, mana ncheekweza kwaajii ya kuamuiiya inusi iya kuiohoa.

48 Akini wose wekuniemeao miye na kuemea mbui yangu, wendawaamuiwe mwe msi uda wa kisiikizi, kwa mbui ya kwei nekugombekayo.

49 Miye ncheekugombeka kwa mwiko wangu mwenye iya khigombeka yada ekunekhayo Tate.

50 Miye namanya miko yakwe yaeta ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi. Miye nagombeka du yada Tate ekuniagiiyao niyagombeke."

# 13

*Yesu asunta wahina wakwe miundi*

1 Neiwa msi nee khaizati kubua sikukhuu ya Pasaka. Yesu akamanya mda wakwe wa kuhauka mwe inusi kuita kwa Tate nee ubua kae. Nee kawakundisa misi yose wantu wakwe wekaao mwe inusi, naho nee kawakundisa muno kwesiho mihaka.

2 Nee Yesu na wahina wakwe wawa wekaa kuda khande ya guoni, Ibiisi kamgeya kae Yuda mwana wa Simoni Isikaliote moyo wa kumhituka Yesu.

3 Yesu akamanya kuwa Tate kaika vintu vyose asi ya udaho wakwe, na kuwa nee kalawa kwa Muungu na endaagotoke kwa Muungu.

4 Aho Yesu akagooka, akaika khandai gwanda dakwe da chongoi, akadoa ntii kitambaa na kwefunga mwe kigudi.

5 Naho, akagea mazi mwe wiga, akavoka kuwasunta wahina wakwe miundi na kuihangusa kwa kitambaa ekwefungacho mwe kigudi.

6 Aho, akamtimia Simoni Petulo, nae Petulo akamba, "Zumbe wee wendaunisunte miundi miye?"

7 Yesu akamtambaisa, "Khumanya nigosoacho isasa, akini wendaumanye kisingi chezaho."

8 Petulo akamwamba Yesu, "Wee khunaunisunte miundi katu."

Yesu akamtambaisa, "Nikesekukusunta khaunauwe yumwe wa wantu wangu kisingi chose."

9 Simoni Petulo akamtambaisa, "Zumbe nisunta, khio miundi du, ata na mikono yangu na viyaviya mtwi."

10 Yesu akamwamba, "Mwekwehaka kae mazi khakundigwa kwehaka vituhu, iya akundigwa kusunta miundi du kwaviya kang'aa mwii wose, nywie mng'aa akini khio nyose."

11 Yesu akamanya yuda endaeamhituke nee mana kagombeka, "Nywie msuntika, akini khio nyose."

12 Ekubindaho kuwasunta miundi na kwehasika vituhu gwanda dakwe, akekaa he meza hantu hakwe, akawauza, "Ivi mniva ivyo nekuwagosoeacho?"

13 "Nywie mwanetanga Mhinyi na Zumbe, nanywi mwagombeka vyedi, kwaajii ni miye.

14 Naho, ikawa miye Zumbe na mhinyi khimisunta miundi, nywie nanywi mwakundigwa mgosoeane ivyo.

15 Khiwekha msimo unu, ili nanywi mgosoe inga nekuwagosweeavyo.

16 Nawagombeka ukwei, mndima khio mkuu kusima mkuu yakwe, wala mwagiiwa khio mkuu kusima yuda mwekumuagiiya.

17 Naho, ikawa mwayamanya ayo, mwendamjaiwe.

18 “Aya nigombekayo ni kwa nywie nyose, miye nawamanya wada nekuwasaguwao. Akini yakundigwa yaiganie Maandiko ya Muungu yagombekavyo, ‘Yuda mwekuda khande hamwe na miye kanihituka.’

19 Miye nawamba mbui izi isasa umo khayazati kulawiiya, ili yalawiaho mdahe kuzumiia kuwa, ‘Miye Nee Uyo.’

20 Nawamba ukwei, amuhokeae yuda nimuagiiye anihokea miye, na anihokeae miye amhokea yuda mwekuniagiiya.”

### *Yesu agombeka mbui ya kuhitukwa kwakwe*

*Matayo 26:20-25; Maliko 14:17-21; Luka 22:21-23*

21 Yesu ekugombekaho ayo, moyo ukamuuma, akagombeka pwii, “Nawamba kwei, yumwe yenu endaanihituke.”

22 Wahina wakwe wakakauwana, kwaviya khawekumanya amgombeka ndai.

23 Mhina yumwe yuda Yesu ekuae amkundisa muno, nee kekaa hehi na Yesu.

24 Simoni Petulo akamhungia mkono na kumwonyesha utangio, na kugombeka, “Muuze amgombeka ni ndai.”

25 Mhina uyo akesogeza hehi na Yesu akamuuza, “Zumbe ni ndai?”

26 Yesu akamtambaisa, “Yuda nendaenimwekhe kibendu cha bumunda, nekukigintacho mwe wiga, nee uyo.” Akadoa kibendu cha bumunda, akakiginta mwe wiga, akamwekha Yuda mwana wa Simoni wa Isikaliote.

27 Yuda wa Isikaliote ekubindaho kuhokea kia kibendu cha bumunda Ibilisi akamwengiya. Aho Yesu akamwamba, “Ukundacho kukigosoa kigosoe kinyio.”

28 Akini khakuna katu yumwe wa wada wekwekaao he meza mwekumanya kwa mbwai kagombeka ivyo.

29 Kwaviya Yuda kawa mwiika hea, watuhu wakamamakhanya, Yesu kamwamba ague vyekukundigwavyo mwe sikukhuu, hambu kamwamba alavye chochose kwa wakiwa.

30 Yuda wa Isikaliote ekuhokeaho kia kibendu cha bumunda, akalawa chongoi kinyio, neiwa kiza.

### *Mwiko mhya*

31 Naho Yuda kisingi kalawa chongoi, Yesu akawamba wahina wakwe akagombeka, “Isasa ukuu wangu miye Mwana wa Mntu uhehi kuoneka pwii. Naho wendauoneke pwii ukuu wa Muungu kwembokea mwe ntendwa zangu.

32 Mwana endaawaonyeshe wantu, Muungu ekuwavyo mkuu, naho Muungu endaawaonyeshe wantu viya Mwana ekuwavyo mkuu.

33 Wanangu nikeaho na nywie kwa mda mjihi du. Mwendamniondeze akini isasa nawamba yada nekuwagombekayo waongoezi wa Kiyahudi, ‘Niitako nywie khamdaha kuita.’

34 Nawekha mwiko mhya, kundisaneni inga viya niwakundisavyo nywie, na nywie kundisaneni.

35 Mkakundisana, wantu wose wendawamanye nywie ni wahina wangu.”

### *Yesu atamwiiya kuwa Petulo endaamuemee*

*Matayo 26:31-35; Maliko 14:27-31; Luka 22:31-34*

36 Simoni Petulo akamuuza, “Waita kuhi?”

Yesu akatambaisa, “Niitako khudaha kunitongea isasa, akini wendaunitongee kisingi chezacho.”

37 Petulo akamwamba, “Kwambwai isasa khidaha kukutongea? Ntayali kuuya na nyuma kwaajii yako.”

38 Yesu akamtambaisa, “Ivi kwei wadaha kuuya na nyuma kwaajii yangu? Nakwamba zogoo khadizati kukema, wendauniemee maa ntatu.”

## 14

### *Yesu nee sia ya kuita kwa Tate*

1 Yesu akawamba, “Mwesekugwidukwa mwe mioyo yenu, mwamzumiiya Muungu, mnizumiie na miye viyaviya.

2 Kaya mwa Tate yangu mna vyekao vingi, ati nee khayekuwa ivyo nee khiwamba kae, isasa naita kuwaikia hakwekaa.

3 Na nikaita kuwaikia hantu ha kwekaa, nendaniuye niwadoe na nywie muwe hada neiho.

4 Sia ya kuita uko, nywie mwaimanya.”

5 Tomaso akamuuza, “Zumbe uitako khatikumanya, tadaha vivihi kuimanya iyo sia?”

6 Yesu akatambaisa, “Miye ni sia na kwei na ugima, khahana mntu adahae kuita kwa Tate kwesiho kwembokea kwa miye.

7 Ati nee mwanimanya miye nee mkammanya na Tate yangu, kuvokea isasa mwammanya naho mmuona kae.”

8 Filipo akamwamba, “Zumbe Tionyeshe Tate du, na swie nee tikundacho!”

9 Yesu akamtambaisa, “Nchekaa na nywie kisingi chose iki, nawe Filipo khauzati kunimanya? Mwekuniona miye

kamuona Tate, wadaha viivihi kugombeka, ‘Tionyeshe Tate?’ ”

10 Ivi, khaunizumiiya ati miye niumo mwa Tate, nae Tate yuumu mwangu? Mbui niwagombekeazo khizigombeka inga nikundavyo miye, iya Tate mweumo mwangu agosoa ndima yakwe.

11 Mwakundigwa mnizumiie nigombekayo miye niumo ndani ya Tate na Tate yuumu mwangu, inga khivyo, zumiiyani kwa ndima nizigosoazo.

12 Nawamba ukwei, anizumiiae endaagosoe mbui nizigosoazo miye, naho endaagosoe makuu muno kwaviya naita kwa Tate.

13 Chochose muombezacho kwa zina dangu ido nendanigosoe, ili Tate atogolwe ekuwavyo mkuu kwembokea Mwanawe.

14 Chochose mniombezacho kwa udaho wa zina dangu nendanimigoswee.

*Yesu agombeka endaawaetee Muye wa Muungu*

15 “Inga nee mkanikundisa mwenda mtoze miko yangu.

16 Nendanimuombeze Tate, nae endaawekhe mwaambiza mtuhu endaeekae na nywie kisingi chose.

17 Muye unu endaawagubuie wantu ukwei. Wantu wa inusi ambao wamuemea Muungu khawadaha kumhokea Muye uyo, kwaajii khawamuona naho khawammanya, akini nywie mwammanya Muye wa Muungu, kwaajii ekaa hamwe na nywie naho endaawe ndani yenu.”

18 “Khinanimibade nywie ikedu, nendaneze vituhu kwenu.

19 Hasigaa hadodo wantu wa mwe inusi khawana wanione vituhu, akini nywie mwendamnione kwaviya miye ni mgima, na nywie nanywi mwendamuwe wagima.”

20 Msi uda wendaho ubue, mwendammanye miye niumo mwa Tate, na nywie muumo mwangu na miye viyaviya niumo mwenu.

21 “Yuda ahokeao miko yangu na kuitongea, yee nee mnikundisa. Anikundisae miye endaakundwe ni Tate yangu, na miye nendanimkundise na nendanimtende animanye.”

22 Yuda, akini khio Yuda Isikaliote akamwamba, “Zumbe yendaidahike viivihi kutitenda swie tikumanye na khio wantu wa inusi wesaokukuzumiiya wee, wakumanye?”

23 Yesu akatambaisa, “Mntu yoyose anikundisae endaatoze mbui yangu na Tate yangu endaamkundise, miye na Tate tendateze kwakwe na kwekaa nae.

24 Mwesaekunikunda khatoza mbui zangu. Na mbui mwekutegeezayo khio yangu, iya ni yakwe Tate mwekuniagiiya.”

25 “Nawamba mbui izi, nike hamwe na nywie.

26 Akini uyo Mwaambizi, nee Muye wa Muungu ambae Tate endaamuagiiye kwenu kwa udaho wa zina dangu, endaawahinye kia kintu na kuwakumbusa yose nekugombekayo.”

27 “Nawabadia uivanisi, ni uivanisi ulawao kwangu, khio uivanisi inga uda ulawao kwa wantu wa inusi, ivyo mwesekwepisha mwe mioyo yenu, naho mwesekuogoha kintu chochose.

28 Mtegeeza kae, nikawamba, ‘Naita nikaukaaho nagotoka vituhu.’ ” Inga nee mkanikundisa, nee mkatamiwa kwaviya naita kwa Tate kwaviya yee ni mkuu kusima miye.

29 Nawamba aya isasa khayazati kulawiiya, aho yendaho yalawiiye, mdahe kuzumiia.

30 Khinanigombeke na nywie vituhu, mbui nyingi mana mkuu wa inusi atimia kwangu, iya khana udaho kwangu.

31 Akini wantu wa inusi wakundigwa kumanya inga namkundisa Tate, nee vyeekavyo nagosoa kia kintu inga Tate ekuniagiiyavyo.

“Gookani tihauke aha.”

# 15

*Yesu nee Mzabibu wa kwei*

1 Yesu akagombeka “Miye ni mzabibu wa kwei, na Tate yangu nee muimi.

2 Kia tambi desado kuvyaa matunda yee adiusa, na kia tambi divyaado adisengeasengea didahe kuvyaa vitana.

3 Nywie msuntwa kae na msuntwa kwaajii ya mzumiiya mbui zangu.

4 Ekaani ndani yangu, nami nekae ndani yenu inga viya tambi desavyo kudaha ikedu kuvyaa matunda dikesekusigaa he mzabibu, ivyoivyo khamdaha kugosoa yada akundayo Muungu kwesiho kusigaa umu mwangu.”

5 “Miye ni mzabibu, na nywie ni matambi, ekaaye umu mwangu, na miye nekaa umo mwake, uyo avyaa matunda mangi, kwaviya kwesiho miye khamdaha kugosoa chochose.

6 Mntu yoyose mwesaekwekaa ndani yangu, atambikwa chongoi inga tambi ditambikwavyo chongoi, adi dinyae. Wantu wadidodoa tambi inga ido na kuditambika mwe moto dihye.

7 Mkekaa umu mwangu na mbui zangu zikekaa mwenu, ombezani chochose mkundacho nanywi mwendamwekhigwe.

8 Wantu wendawammanye Tate yangu endaatogolwe ekuwavyo mkuu inga mkagosoa mbui nyingi akundazo Muungu na mwendamuwe wahina wangu.

9 Inga viya Tate ekunikundisavyo miye, ivyo ndiho miye nekuwakundavyo nywie, ekaeni kwa kuongoewa na ukundiso wangu.
10 Mkatoza miko yangu nendaniendee kuwakundisa, inga viya miye nekutozeezavyo miko ya Tate yangu ambae aendeea kunikundisa.
11 "Nawamba mbui izi, nakunda nywie muwe na nyemi na miye, inga viya miye niwavyo na nyemi na nywie.
12 Inu nee miko yangu, kundisaneni inga nekumikundisavyo miye.
13 Sia khuu muno ya kuonyesha wawakundisa wambuya zako, ni kuuya na nyuma ili wowo wekae.
14 Nywie ni wambuya wangu mkagosoa niwaagiiavyo.
15 Nywie khinaniwetange wandima wangu vituhu, kwaviya mndima khamanya agosoado Zumbe yakwe, akini miye nawetanga nywie wambuya, kwaajii nawamba yose nekutegeezayo kulawa kwa Tate yangu.
16 Nywie khamwekunisagua miye, iya miye khiwasagua na kuwaagiiya muite mkavyae matunda yekaayo, naye Tate adahe kuwekha chochose mkiombezacho kwa zina dangu.
17 Naho nawagiiya kia mntu na amkundise mwezie.

*Wantu wa inusi khawawakundisa nywie*

18 "Inga wantu wa mwe inusi wakawakima nywie, akini msekujaa idi, wowo wavoka kunikima miye.
19 Inga nemuwa wantu wa inusi, inusi nee ikamikunda nywie inga wantu wakwe, Akini kwaviya nywie khio wa mwe inusi, iya miye khiwasagua kulawa mwe inusi inu, kwaajii inu wantu wa inusi wawakima.
20 Kumbukani nekuwambiavyo, 'Mtumwa khio mkuu kusima mkuu yakwe.' Ikawa wanisuumiza miye wenda wamisuumize nywie naywi ati watoza mbui zangu, wendawatoze na da kwenu.
21 Akini ayo yose wenda wamigoswee nywie kwaajii ya kunizumiiya miye, kwaviya khawammanya mwekuniagiiya.
22 Inga nchekweza na kugombeka nawo nee khawekuwa na mavigaviga, akini isasa khawadaha kwevunia inga khawana mavigaviga.
23 Mnikima miye, viyaviya amkima Tate yangu.
24 Wesekuwa na mavigaviga inga nchekugosoa vihii gatigati yao, yada ambayo khahana mntu yoyose adahae kuyagosoa akini wowo waona yada nekuyagosoayo na wakanikima miye hamwe na Tate yangu.
25 Nee mana yada yekuandikwayo mwe miagiiyo yao ni kwei, 'Wanikima buebue.'
26 "Nendanimwagiiye Muye wa Muungu alawaye kwa Tate, endaeawaonyeshe ukwei. Muye uyo wa Muungu endaawambize na kuwagombeka miye neivyo.
27 Na nywie nanywi mwenda mnigombekee, kwaviya muwa na miye kuvokea aho bosi.

## 16

1 "Kiwamba ayo kwaviya msekueka kunizumiiya.
2 Wantu wendawamiguuse nywie he nyumba zawo za kukintania Wayahudi. Naho kisingi cheza kia endaeawakome nywie endaamamakhanye kuwa amgosoea ndima Muungu.
3 Wenda wamigoswee mbui izo kwaviya khawekummanya Tate naho khawekunimanya miye."
4 Akini khiwamba mbui izo ili mda wendahoubue kwa wowo kuwagosoea ayo, mwendamkumbuke kuwa khiwamba.

*Ndima za Muye wa Muungu*

Nchekuwamba mbui izo, kuvokea aho bosi, kwaviya khiwa hamwe na nywie.
5 Akini isasa naita kwa yuda mwekuniagiiya na khahana katu mntu yumwe aniuzae, waita hahi?
6 Kwaviya khiwamba mbui izo mmema usungu mwe mioyo yenu.
7 Akini nawamba ukwei, ni vyedi kwenu miye nihauke, kwaviya nikesekuita mwambizi khanaeze kwenu, akini nikaita uko nendanimwaagiiye kwenu.
8 Nae endahoeze endaawaonyeshe wantu wa mwe inusi mbui ya mavigaviga, na kwa mbui ziya zimtamiazo Muungu na kwa mbui ya uwamuiiyo wa Muungu.
9 Waga kwa mbui za mavigaviga kwaajii khawanizumiiya miye,
10 Mwe mbui ya kumtamiza Muungu, miye khigosoa yamtamizayo Muungu nee mana naita kwa Tate, nanywi khamna mnione vituhu.
11 Aonyesha pwii kuwa Muungu endaawaamuiye kwaajii kamuamuiya kae Shetani ambae ni muongoezi wa inusi.
12 "Nina mangi ya kuwamba iya kwa isasa khamdaha kuyamanya yose.
13 Akini endaho auye uyo Muye wa kwei endaawatende muimanye kwei yose ya Muungu, naho khana agombeke mbui zakwe mwenye, iya enda agombeke ekuyategeezayo na kugombeka yendayoyeze.
14 Yee endaawatende mnitunye, kwaajii endaawambe yada yose endayo apate kulawa kwangu.

15 Vyose enavyo Tate ni vyangu, nee vyekweekacho khigombeka kuwa Muye endaawambe yada yose yalawayo kwangu.

*Usungu na nyemi*

16 “Kisingi kidodo khamnamnione, na bada ya kisingi kidodo vituhu mwendamnione.”

17 Aho wamwe wa wahina wakwe wakauzana, “Ambaze? Atambiaho, kusigaa kisingi kidodo khamna mnione na ikemboka kisingi kidodo vituhu mwendamnione? Naho amba, ‘kwaviya naita kwa Tate.’

18 Aho wakaendeea kuuzana, ana mana yani, agombekaho, ‘Kusigaa kisingi kidodo?’ Khatimanya amba mbwai!”

19 Yesu kamanya ati nee wakoondeza kumuuza, aho akawamba, “Ivi mwauzana kwa yada nekugombekayo, ‘Kusigaa kisingi kidodo nywie khamna mnione.’ Na ikemboka kisingi kidodo vituhu mwendamnione?

20 Nawamba ukwei, nywinywi mwendamwiiye na kuwa na bwaimbo, akini wantu wa inusi wendawawe na nyemi, mwendamuone usungu, akini usungu wenu wendauhituke uwe nyemi.

21 Inga mvyee aita kuvyaa mwana, ana usungu kwaajii amanya kisingi chakwe cha maumevu makai kibuwa, akini akabinda kuvyaa mwana, khakumbuka vituhu maumevu ayo, kwaajii ya nyemi ya kuvyaigwa mwana mteke mwe inusi ibua.

22 Nanywi, isasa mna usungu, akini nendaniwezee vituhu, naho mwendammeme nyemi he miyoyo yenu na nyemi iyo khahana mntu mwendae aiyuse kwenu.

23 “Msi uwo khamna mniombeze chochose. Nawamba ukwei, chochose mwendacho mumuombeze Tate, kwa udaho wangu mwendamwekhigwe.

24 Adi isasa khamzati kuombeza chochose kwa udaho wangu. Akini isasa ombezani nanywi mwenda mwekhigwe, ili muwe na nyemi muno.

*Yesu kaivota inusi*

25 “Khiwamba mbui izo kwa misimo, akini kisingi cheza ambaho khina nigombeke na nywie vituhu kwa misimo iya nendaniwambe pwii mbui za Tate.

26 Msi uwo, mwendamuombeze kwa udaho wangu na khinaniwambe ati nendanimuombeze Tate kwaajii yenu,

27 yee mwenye Tate awakundisa nywie, kwaviya nywie mwanikundisa miye, na kunizumiiya kuwa nalawa kwa Tate.

28 Miye nalawa kwa Tate ncheza mwe inusi, isasa nahauka mwe inusi inu na kuuya kwa Tate.”

29 Aho wahina wakwe wakamwamba, “Isasa wagombeka pwii kwesiho kugea misimo.

30 Isasa tamanya kuwa wee wamanya kiya kintu, khahana haja ya kuuzigwa mbui na mntu yoyose, ivyo tazumiiya ati kulawa kwa Muungu.”

31 Yesu akawatambaisa, “Ivi isasa twazumiia?

32 Kisingi cheza, naho kibua kae, ambaho nywie nyose mwendahomumwaganike kiya mntu kwakwe, namiye nabadwa ikedu, aaha akini miye khiko ikedu, mana Tate yu hamwe na mie.

33 Nawamba mbui izi mdahe kuwa na uivanisi he kuwa hamwe na miye, mwe inusi mwenda mkubwaniswe, akini togwani ni moyo miye khivota inusi.”

# 17

*Yesu awavikia wahina wakwe*

1 Yesu ekubindaho kugombeka ayo, akenua meso uwanga kwa Muungu, akamba, “Tate ida saa ibuwa! Mtogoe Mwanao na Mwana nae adahe kukutogoa.

2 Kwaviya kumwekha udaho Mwanao mwa wantu wose, ili awekhe ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi, wose wekumwekhao.

3 Na ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi nee unu, kukumanya wee ikedu Muungu wa kwei na kummanya Yesu Klistu wekumwaagiiaye.

4 Miye kikutogoa mwe inusi nakuwaonyesha wantu ukuu wako, kwembokea ndima wekuniagiiazo nizigosoe.

5 Isasa Tate unitogoe uwaonyeshe wantu nekuwavyo mkuu kwa uda Ukuu nekuwao nao, kabla ya kuumbigwa inusi.

6 “Khikutenda umanyike kwa wantu wekunekhao kulawa mwe inusi, nee wawa wantu wako, nawe ukanekha wawe wangu naho wagosoa yose wekuwaagiiayo,

7 isasa wamanya kuwa kia wekunekhacho kilawa kwako.

8 Kwaajii khiwamba yose wekunigombekayo, nawo wakahokea, wamanya kwei kilawa kwako na wazumiiya wee nee mwekuniagiiya.

9 “Nawaombezea awo, nawala khiwaombezea wantu wa inusi, iya nawaombezea wada wekunekhao kwaviya ni wako.

10 Wantu wose nekuwao nao ni wako naho wantu wose ambao ni wako ni wangu na miye kitogolwa na waoneka mwe wada wekunekhao.

11 Na isasa neza kwako, khimo vituhu mwe inusi, akini wowo wendawaendee kuwa mwe inusi, Tate Muungu! Kwa udaho wa zina dako wekunekhado uwaike

pheho wawe kintu kimwe inga swie teivyo hamwe.

12 Nekuaho nawo, miye kiwaika pheho kwa udaho wa zina dako wekunekhado Miye khiwainda naho khahana katu yumwe yawo mwekwaga iya ni yuda mwana mwekwaga, ili Maandiko ya Muungu yaiganie inga yekuandikwavyo.

13 Isasa neza kwako na kigombeka mbui izo mwe inusi, ili wawe na nyemi muno mioyo yao inga ambavyo miye nekuwavyo na nyemi.

14 Miye kiwekha mbui yako, naho wantu wa inusi wakawakima, akini wowo wekukuzumiiao khio wantu wa inusi inu, inga viya mie nesivyo wa mwe inusi inu.

15 Khiombeza uwalavye mwe inusi iya naombeza uwainde na yuda mbanasi.

16 Wowo khiwo wa mwe inusi, inga viya nesivyo wa mwe inusi.

17 Eee Tate nakuombeza uwazingue kuwa wantu wako wa kwei, kwa sia ya ukwei wako, kwaajii mbui yako nee ukwei.

18 Inga viya wekuniagiiavyo mwe inusi na miye kiwaagiiya wowo mwe inusi.

19 Miye mwenye nchezingua kukugosoea ndima kwaajii yawo ili wowo nawo wezingue kukugosoea ndima mwe ukwei.

20 “Khiwavikia wowo du, iya nawavikia wose wendao wakuzumiiye kwaawiana na mbui zao.

21 Naombeza ili wose wawe kintu kimwe, Tate naombeza wawe ndani yetu inga viya wee weivyo ndani yangu miye ndani yako, naombeza wawe kintu kimwe ili wantu wa inusi wakuzumiiye inga wee nee mwekuniagiiya.

22 Miye khiwekha ukuu udauda wekunekhao miye, wawe kintu kimwe inga viya swie teivyo hamwe.

23 Miye niwe ndani yawo nawe uwe ndani yangu, naombeza watendwe wawe kintu kimwe, kwaivyo wantu wa inusi wamanye wee nee mwekuniagiiya naho wawakundisa wowo inga unikundisavyo mie.

24 “Tate naondeza awo wekunekhao wawe hamwe na miye hada neiho, waone Ukuu wangu wekunekhao, kwaviya nee kunikunda, kabla inusi khaizati kuumbigwa.

25 Tate Yedi! Wantu wa mwe inusi khawakumanya, akini miye nakumanya, awa nawo wamanya wee kuniagiiya.

26 Khikutenda zina dimanyike kwao, na nendanitendese kugosoa ivyo, ili ukundiso wenao kwangu uwe umo mwao na miye umo mwao.”

# 18

*Yesu agwiwa*

*Matayo 26:47-56; Maliko 14:43-50; Luka 22:47-53*

1 Yesu ekubindaho kugombeka ayo, akaita phande ya kaidi ya ngodi ya mazi ya Kedloni, hamwe na wahina wakwe, hantu hada hawa na kamnda. Nae Yesu akengiya umo hamwe na wahina wakwe.

2 Yuda, mwekumhituka Yesu, kahamanya hantu hada, kwa viya kia maa Yesu nee wakakintana hamwe na wahina wakwe.

3 Yuda akadoa wakhondo wa Kilumi na wagoji kulawa kwa waviki wakuu na mafalisayo, akeza nawo he kamnda, uku watoza mienge, na chemli na vitoanavyo.

4 Yesu, kwaviya kavimanya vyose vyendavyo vimbwiiye, akalawa akawauza, “Mwamwondeza ndai?”

5 Nawo wakamtambaisa, “Yesu wa mzi wa Nazaleti.”

Yesu akawamba, “Nee Miye.”

Yuda mwe kumhituka kagooka aho hamwe nawo.

6 Yesu ekuwambaho, “Nee Miye,” wowo wakauya mgeeka, na wakagwa asi.

7 Yesu akawauza vituhu, “Mwamwondeza ndai?”

Wowo wakamtambaisa, “Yesu wa Nazaleti.”

8 Yesu akawamba, “Khiwamba kae kuwa nee miye, naho inga mwaniondeza miye, waekeni awa waite.”

9 Yesu kagombeka ayo, ili yalawiiye yada ekugombekayo aho bosi, “Wada wekunekhao nchekumwaza ata yumwe.”

10 Simoni Petulo kawa na paange, nee adisoomoa, akamsenga gutwi da kuume mndima wa Mviki Mkuu. Mndima uyo nee aketangwa Maliko.

11 Aho Yesu akamwamba Petulo, “Vuza paange dako mwe safuo dako, ivi nisekudomeya kikombe cha usuumizi ekunekhacho Tate?”

*Yesu egalwa kwa Mviki Mkuu*

12 Wada wakhondo wa Kilumi na mgookezi yawo na wagoji wa Wayahudi nee wamgwiiya Yesu wakamzengeteza sigi,

13 na wakamwegaa kwa Anasi, Anasi ni mkwewe da Kayafa yuda mwekuwa Mviki Mkuu wa kisingi icho.

14 Uyo Kayafa nee mwekuwamba Wayahudi kuwa, yendaiwe vitana mntu yumwe auye na nyuma, kwaajii ya wantu wose.

*Petulo amhituka Yesu*

*Matayo 26:69-70; Maliko 14:66-68; Luka 22:55-57*

15 Simoni Petulo hamwe na mhina mtuhu wakamtongea Yesu. Uyo mhina mtuhu nee akamanyika kwa Mviki Mkuu,

ivyo akengia na Yesu heukumbi wa Mviki Mkuu.
16 Akini Petulo, nee kagooka chongoi hehi na uvi. Naho uyo mhina mtuhu mwekumanyika kwa Mviki Mkuu akalawa chongoi, na akagombeka na mndima wa kivyee mgoji wauvi akamwengiza Petulo ndani.
17 Mtumwa uyo ya kivyee mgoji wauvi akamuuza Petulo, nawe wee ni yumwe wa wahina wa mntu uyu?
Petulo akamtambaisa, “Khio miye.”
18 Msi uwo nekuwa na pheho na wandima na wagoji nee wagimba moto, naye Petulo akagooka hamwe nawo wakaotea moto.

*Mviki Mkuu amuuza Yesu*

*Matayo 26:59-66; Maliko 14:55-64; Luka 22:66-71*

19 Naho Mviki Mkuu akamuuza Yesu mbui ya wahina wakwe na mahinyo yakwe.
20 Yesu akamtambaisa, “Miye khigombeka na inusi pwii, kia maa nahinya he Nyumba ya kukintania Wayahudi, na kwe Nyumba ya Muungu na hantu wakintanaho Wayahudi wose, naho ncheekugombeka dodose kwa sii.
21 Kwa mbwai waniuza miye? Wauze wada wekunitegeezao khiwambaze, wowo wamanya nekuwambiavyo.”
22 Ekubindaho kugombeka ayo, mgoji yumwe mwekua kagooka hada akamtoa Yesu kofi akamba, ivi wee nee umtambaisavyo Mviki Mkuu?
23 Yesu akamtambaisa, ati khigombeka yesayo kutama vuhuzia ivyo vyesavyo kutama, akini ati kigombeka vyedi wanitoeyani?
24 Nee Anasi amwegaa Yesu uku kazengetezwa sigi, kwa Mviki Mkuu Kayafa.

*Petulo agombeka khammanya Yesu*

*Matayo 26:71-75; Maliko 14:69-72; Luka 22:58-62*

25 Na Simoni Petulo kawa aho aotea moto, umo wakamuuza, “Ivi, wee ni yumwe wa wahina wakwe?”
Petulo akaemea na kwamba, “Khiyo miye.”
26 Yumwe da wandima wa Mviki Mkuu akamba, ni nduguye da yuda mntu mwe kusengwa gutwi ni Petulo, akamuuza, “Ivi miye nchekukuona he kamnda hamwe naye?”
27 Petulo akaemea vituhu, akagombeka khio miye, vuupu zogoo dikakema.

*Yesu egalwa kwa Pilato*

*Matayo 27:1-2,11-14; Maliko 15:1-5; Luka 23:1-5*

28 Keokeo da mtungaihu wakamdoa Yesu kulawa kwa Kayafa, na kumwegaa kwe nyumba khuu ya mkuu wa Walumi, nawo wadahe kuida sikukhuu ya Pasaka, khawe kwengia mwe nyumba ya mkuu wa Walumi, nee waogoha kwaviya wakengia kwendakuwatende wesekuzumiwa kwe kumvikia Muungu, ivyo newavotwa kugosoa sikukhuu ya Pasaka.
29 Ivyo Pilato akawabasa chongoi akawauza, “Ivi mntu uyu kagosoa masa yani adi mumwete kwangu?”
30 Wakamtambaisa, “Inga uyu kheekuwa mkoa masa khatekuwa timwete kwako.”
31 Pilato akawamba, “Hayani, mdoeni nywinywi wenye mkamuamwiiye kutongeana na miagiiyo yenu.”
Wayahudi wakamtambaisa, “Miagiiyo yetu yatiemeza kumkoma mntu yoyose.”
32 Wagombeka ivyo, ili vidahe kuigania mbui ekugombekayo Yesu kumanya enda afe vivihi.
33 Pilato akengia vituhu mwe nyumba ya mkuu wa Walumi akamwetanga Yesu na kumuuza, “Ivi wee nee Seuta wa Wayahudi?”
34 Yesu akamtambaisa, izo ni mbui zako mwenye, hambu wantu watuhu wakwamba mbui zangu?
35 Pilato akamtambaisa, “Ivi miye ni Myahudi? Wantu wa si yako na waviki nee wekukuetao kwangu. Kugosoa masa yani?”
36 Yesu akamtambaisa, “Useuta wangu khio wa mwe inusi, ati useuta wangu nee ni wa mwe inusi, wandima wangu nee wakanivunia nisekweza kugwiwa na Wayahudi, akini isasa useuta wangu khio wa aha.”
37 Aho Pilato akamwamba, “Ivi wee u Seuta?”
Yesu akamtambaisa, “Weye wamba miye ni Seuta, miye khivyaigwa kwaajii iyo, na kwaajii iyo ncheza mwe inusi kuwamba wantu ukwei na kia mntu azumiiyae ukwei, uyo anitegeeza.”
38 Pilato akamuuza Yesu, “Ukwei ni mbwai?”

*Yesu aamuiiwa kuuya na nyuma*

*Matayo 27:15-31; Maliko 15:6-20; Luka 23:13-25*

Pilato ekubindaho kugombeka ayo, akawabasa Wayahudi vituhu chongoi akawamba, “Miye khiona masa yoyose kwakwe.”
39 Akini mna mazweeya ya kuniombeza miye kuwavuguiya mfungwa yumwe kisingi cha sikukhuu ya pasaka, Ivi mwakunda niwavugwiiye Seuta wa Wayahudi?

40 Aho wakatoa vuzo, “Aah! Khio mntu uyu iya Balaba!” Na yuda Balaba nee kawa mhokaji.

# 19

1 Naho Pilato akaagiiya Yesu adoigwe, atoigwe makoto.

2 Na awo maasikali wakagosoa kintu inga khofia ya useuta yekugosolwayo na miwa, wakambadika mwe mtwi, wakamvikia gwanda da langi ya zambalau.

3 Wakeza hemeso yakwe na kugombeka “Togoa, Seuta wa Wayahudi!” Wakamtoa vibao.

4 Pilato akalawa vituhu chongoi, akawamba wada wekukintanao, “Kauwani, namwekhiiza Yesu henu na kuwamanyisha miye khiona masa yoyose ya mntu huyu.”

5 Umo Yesu akalavigwa chongoi kevaiya kiya kintu inga khofia ya useuta yekugosolwayo na miwa, na gwanda da langi ya zambalau, Pilato akawamba, “kauwani mntu mwenye nee uyo.”

6 Waviki wakuu na wagoji wekumuonaho wakakweza mgutio, “Agong'ondewe he mhamba! Agong'ondewe he mhamba.”

Pilato, akawamba, “Mdoeni nywinywi wenye mkamsuumiize, mana miye khiona masa yoyose kwakwe.”

7 Wayahudi wakatambaisa, “Swiye tina Miko, na kutongeana na miko iyo akundigwa auye na nyuma kwaviya ketanga Mwana Muungu.”

8 Pilato ekusikiaho mbui iyo akaogoha.

9 Akengiya mwe nyumba khuu ya kiseuta vituhu akamuuza Yesu, “kulawiiya kuhi?”

Akini Yesu khee kumwaandua mbui yoyose.

10 Pilato akamwamba, “Wee khukunda kutamwiiya na miye? Khumanya kuwa miye ninaudaho wakukuekea naho ninaudaho wa kukugong'ondea he mhamba.”

11 Yesu akatambaisa, “Wee una udaho uwanga yangu, kwaajii du kwekhigwa ni Muungu, ivyo yuda mwekunekhiiza kwako kagosoa kintu kifyaimi muno.”

12 Kuvokeya aho, Pilato akaondeza sia ya kumweekeya, akini wayahudi wakatoa vuzo, “Ukamwekeya mntu uyu, wee khiwe mmbuya wa zumbe mkuu wa Walumi, kiya mntu atendaye kuwa seuta ahigana na seuta wa Wakilumi.”

13 Naho Pilato ekutegeezaho mbui izo akamlavya Yesu chongoi akekaa he kigoda cha uamwiiyo hantu hetangwaho “Hantu hekupangwaho maiwe.” Kwa kieblania “Gabasa”

14 Yekubuwaho saa mtandatu wa musi, msi wa kweika tayali kwaajii ya Pasaka. Pilato akawamba Wayahudi, “Mkauweni Seuta yenu.”

15 Wowo wakakweza mgutio, “Mkome! Mkome! Agong'ondwe he mhamba.”

Pilato akawauza, “uwo nimgong'onde he mhamba seuta yenu?”

Waviki wakuu wakatambaisa, “Swie khatina seuta iya seuta mkuu wa kilumi!”

16 Aho pilato akamgeya Yesu mwe mikono yao agong'ondewe he mhamba.

### *Yesu agong'o ndewa he mhamba*

*Matayo 27:32-44; Maliko 15:21-32; Luka 23:26-43*

Ivyo wakamdoa Yesu.

17 Yesu ekwenuwaho mhamba wakwe, akalawa kuita hantu he kwetangwaho, “Fufu da mtwi” kwa Kieblania ni Goligota.

18 Aho nee agong'ondewa he mhamba, hamwe nae wawagong'ondea he mhamba wantu watuhu waidi, kia yumwe he mhamba wakwe, yumwe phande ya kuume na mtuhu phande yakwe ya kumoso, na Yesu gatigati.

19 Pilato akaandika kibao akakiika uwanga ya mti wa mhamba nee kiandikwa ivi, “Yesu Mnazaleti Seuta wa Wayahudi”

20 Wayahudi wangi wasoma kibao icho, mana hada ekugong'ondewaho Yesu hawa hehi na mzi. Naho kibao icho kiwa kiandikwa kwa Kieblania na Kilatini na Kigiiki.

21 Waviki Wakuu wa Wayahudi wakaemea wakamwamba Pilato, “Usekuandika, ‘Seuta wa Wayahudi,’ iya andika, mntu huyu nee kamba, ‘Miye ni Seuta wa Wayahudi.’ ”

22 Pilato akawatambaisa, “Nekuandikayo khiyaandika.”

23 Maasikai wekubindaho kumgong'ondea Yesu he mhamba, wakadoa magwanda yakwe wakayapanga mafungu mane, fungu dimwe kwa kia asikai, wakadoa viyaviya na gwanda dakwe, gwanda ido diwa difumwa na kuwa kintu kimwe kulawa uwanga adi asi.

24 Awo masikai wakamamakhanya, “Tisekuitatua iya tiitwee kula yendaiwe ya ndai.” Mbui iyo igosoka ili Maandiko ya Muungu yaiganie, yagombekayo,

“Wapangana magwanda yangu

Na gwanda dangu wakaditwee kula.”

Ivyo nee wekugosoavyo wada maasikai.

25 Hehi ya mti wa mhamba wa Yesu nee wagooka mami yakwe da Yesu, na mami yakwe mdodo da Yesu na Maliamu mkaza Kileopa na Maliamu wa mzi wa Magidala.

26 Yesu ekumuonaho mami yakwe, na hehi naye kagooka yuda mhina ekumkundisae, akamwamba mami yakwe, “Mmaa uyo nee mwanao.”

27 Akabinda akamwamba yuda mhina, "Kauwa uyo nee mami yako." Na kuvokeya mda uda mhina akahauka nae kaya kwakwe.

*Ufe wa Yesu*

*Matayo 27:45-56; Maliko 15:33-41; Luka 23:44-49*

28 Yesu akamanya kabindiiza ndima yakwe ya uohozi, naho akagombeka ili Maandiko ya Muungu yadahe kuigania, "Naona khiu."

29 Aho nee hana wiga wekumemao divai yekusasayo, akadoa dodoki akadiginta mwe divai yekusasayo, wakaigea uwanga ya lasi, wakamwiikiya mwe muomo.

30 Yesu ekusonaho iyo divai yekusasayo akamba, "Yaigania!"

Naho akenamiza mtwi wakwe, akauya na nyuma.

*Yesu atungwa guha mwe ubavu*

31 Iwa Ijumaa msi wa mwaandao, kwaivyo mii isekwekaa mwe mti wa mhamba, kwaajii Msi uwo wa Kuhumwiiza iwa msi mkuu kwa Wayahudi, wakamwoombeza Pilato miundi ya awo wekugong'ondewao he mhamba ibondwe na mii yawo iusigwe.

32 Ivyo maasikai wakaita, wakaibonda miundi ya yuda mntu wa bosi na yuda wakaidi wekugong'ondewa he mhamba hamwe na Yesu.

33 Akini wekumbwiiaho Yesu waona kauya kae na nyuma, ivyo khawekumbonda miundi yakwe.

34 Akini asikai yumwe akamtunga ubavu kwa guha na vuupuu ikalawa phome na mazi.

35 Yuda mwekuona mbui iyo, akawamba wantu ili nywie mdahe kuzumiia, na yada ekugombekayo ni kwei naho amanya kuwa agombeka ukwei.

36 Mbui iyo igosoka ili Maandiko ya Muungu yaiganie "Khahana katu vuha dakwe dimwe dendado dibondwe."

37 Naho Maandiko ya Muungu matuhu yamba, "Wendawamkauwe yuda wekumtungae."

*Yesu agewa mwe mbia*

*Matayo 27:57-61; Maliko 15:42-47; Luka 23:50-56*

38 Yekusiaho ayo, Yusufu mwenyezi wa mzi wa Alimataya, mwekuwaye mndima wa Yesu etiho kwa sii kwaajii ya kuwaogoha Wayahudi, akaita kwa Pilato na kumuombeza uhusa wa kuudoa mwii wa Yesu, Pilato akamzumiiya, ivyo Yusufu akaita akaudoa mwii wa Yesu.

39 Naho Nikodemo, ambae aho bosi kawa kambasa Yesu na kio, akaita hamwe na Yusufu wakadoa mhanganyo wa manemane na ubani yabua kilo makumi matatu.

40 Wantu waidi awo, wakaudoa uda mwii wa Yesu wakauzengeteza sanda hamwe na yada malashi inga yeivyo mazweeya ya Wayahudi he uzisi.

41 Hada hakugong'ondewa Yesu hawa na kamnda, na mwe kamnda ako hawa na mbia dihya dekusongwado he iwe kuu, ambado khadizati kugewa mntu yoyose.

42 Kwa ngijangija za Wayahudi za mwaandao wa Msi wa Kuhumwiiza, kwaviya mbia ido diwa hehi, wakaika mwii wa Yesu umo.

# 20

*Mbia ibue*

*Matayo 28:1-8; Maliko 16:1-8; Luka 24:1-12*

1 Keokeo da mtungaihu, msi wa bosi wa juma kukekuwa na kakiza, Maliamu wa kulawa Magidala akaita kwe mbia, akadiona dia iwe diusigwa he uvi wa mbia.

2 Aho akaguuka kuita kwa Simoni Petulo na yuda mhina mtuhu Yesu ekuaye kamkundisa muno akawamba, "Wamuusa Zumbe he mbia na aho khatimanya wamwiikia kuhi."

3 Ahoaho, Petulo hamwe na yuda mhina mtuhu wakahauka na kuita kwe mbia.

4 Wose waidi wakaguuka akini yuda mhina mtuhu kaguuka kinyio kusima Petulo, akaongoa kubua he mbia.

5 Ekwenamaho na kusungiia ndani ya mbia akoona sanda, akini kheekwengia ndani.

6 Simoni Petulo akeza akamtimia, akengia he mbia, umo akaona sanda,

7 na kia kitambaa ekuzengetewazo Yesu kwe mtwi. Kitambaa icho khachekuikwa hamwe na sanda, kikunjwa na kuikwa hantu ha ikedu.

8 Naho yuda mhina mtuhu mwekuongoa kubua he mbia, akengia viyaviya ndani akoona na akazumiiya.

9 Nee khawazati kuva Maandiko ya Muungu yekwambayo kuwa, nee yakundigwa ayuyuke kulawa he ufe.

10 Naho awo wahina wakauya kaya.

*Yesu amuawiiya Maliamu kulawa Magidala*

*Matayo 28:9-10; Maliko 16:9-11*

11 Maliamu kawa kagooka chongoi ya mbia aiya, uku akekwiiya nee enama na kusungiia he mbia,

12 akaona wandima wa uwanga wa Muungu waidi, wekuvaawo magwanda yekung'aayo muno, wekaa hada wekuwaho mwii wa Yesu ugonezwa yumwe he mtwi, wa kaidi he miundi.

[13] Awo wandima wa uwanga wa Muungu
wakamuuza, “Mmaa kwa mbwai waiya?”
Nae akawatambaisa, “Wamuusa Zumbe yangu na khimanya wekumwiikako!”
[14] Ekugombekaho ayo, akahituka mgeeka akamuona Yesu kagooka aho, akini kheekumtanga inga ni Yesu.
[15] Yesu akamuuza, “Mmaa waiya mbwai?
Wamwoondeza ndai?”
Maliamu akamamakhanya uyo nee mgookezi wa kamnda akamwamba, “Mkuu inga ni weye mwekumuusa, nambia wekumwiikako, nami ninda nimdoe.”
[16] Yesu akamwetanga, “Maliamu!” Nae
Maliamu akamhitukia Yesu na kumwamba kwa Kiebulania, “Laboni” mana yakwe, “Mhinyi.”
[17] Yesu akamwamba, “Usekunitoza
khizati kuita uwanga kwa Tate, akini uite kwa wandugu zangu ukawambe, naita uwanga kwa Tate yangu na Tate yenu, Muungu yangu na Muungu yenu.”
[18] Ivyo Maliamu wa mzi wa Magidala
akaita kuwamba wada wahina kuwa kamuona Zumbe na kuwa nee kamwamba ivyo.

*Yesu awalawiiya wahina wakwe*

*Matayo 28:16-20; Maliko 16:14-18; Luka 24:36-49*

[19] Nee iwa guoni wa msi uwo wa bosi
wa juma, wahina wa Yesu, wakakintana hamwe mwe nyumba, na nyuvi nee zivugalwa kwaajii ya kuwaogoha waongoezi wa Kiyahudi. Aho Yesu akeza akagooka gati yawo akawamba, “Uivanisi uwe kwenu.”
[20] Ekugombekaho ivyo, akawaonyesha
mikono yakwe na mbavu zakwe, aho wahina wakwe wakawa na nyemi muno kwaviya wamuona Zumbe.
[21] Yesu akawamba vituhu, “Uivanisi uwe
hamwe nanywi, inga viya Tate ekuniagiiavyo miye, na miye nawaagiiya nywinywi.”
[22] Ekugombekaho ayo, akawavuziya
muye na kuwamba, “Hokeani Muye wa Muungu.”
[23] Inga mwawaekea wantu mavigaviga
yao Muungu endaawaekee na inga mkese kuwaekea wantu mavigaviga yao, Muungu khana awaekee mavigaviga yao.

*Yesu na Tomaso*

[24] Tomaso, yumwe wa wada kumi dimwe
na waidi etangwae zina tuhu mpasa kheekuwa hamwe nae kisingi Yesu ekwezaho.
[25] Aho wada wahina watuhu
wakamwamba, “Timwoona Zumbe.”
Akini Tomaso akawamba, “Nikesekuona alama za misumai mwe mikono yakwe na kugeya chaa changu he khovu izo na kugeya mkono wangu he ubavu wakwe, khinanizumiiye.”
[26] Yekwembokaho misi nane, wahina
wakwe wawa hamwe umo ndani, na Tomaso kawa hamwe nawo, akeza Yesu akagooka gatigati yawo, uku nyuvi ziwa zivugalwa akamba, “Uivanisi uwe nanywi.”
[27] Naho akamwamba Tomaso, “Ete chaa
chako aha uikauwe mikono yangu, ete mkono wako wembose he ubavu wangu usekuwa na maatu iya zumiiya.”
[28] Tomaso akamtambaisa, “Weye ni
Zumbe yangu naho weye ni Muungu yangu!”
[29] Yesu akamwamba, “Ivi kuzumiia
kwaajii kuniona? Ebae wada wesaokuona akini wazumiiya.”

*Mbui zikundigwazo na kitabu iki*

[30] Yesu kagosoa hemeso ya
wahina wakwe ntangio ntuhu nyingi khazekuandikwa mwe kitabu iki.
[31] Akini izi ziandikwa mdahe kuzumiia
inga Yesu ni Klistu Mwana wa Muungu na kwa kuzumiiya mdahe kuwa na ugima wa misi yose kwesiho kisiikizi.

# 21

*Yesu awalawiiya wahina mfungate*

[1] Yekwembokaho ayo, Yesu akawalawi-
iya vituhu wahina wakwe, khandakhanda ya tondoo da mazi da Tibelia na idoido nado nee tondondoo da mazi da Galilaya na nee yekuwavyo,
[2] Simoni Petulo na Tomaso etangwae
phasa na Nasanaeli mwenyezi wa mzi wa Kana ya Galilaya, na wana waidi wa Zebedayo, na wahina watuhu waidi wawa hamwe wose.
[3] Simoni Petulo akawamba weziwe,
“Naita kwekuloa samaki.”
Nawo wakamwamba, “Tenda tiite hamwe nawe.” Naho wakalawa, wakengia mwe ngaawa, akini kio icho khawekwaambua chochose.
[4] Wekuvokaho kucha, Yesu nee agooka
khandakhanda ya tondoo da mazi, akini wahina khawekummanya ati ni yee nee Yesu.
[5] Aho Yesu akawauza, “Wambuya wangu,
khamzati kupata samaki wowose?”
Wowo wakamtambaisa, “Bue! Khatizati kwaambua kintu.”
[6] Yesu akawamba, “Tambikani nyavu
zenu phande ya kuume ya ngaawa nanywi mwenda mpate samaki.” Nee wazitambika nyavu akini isasa khawekudaha kubuuta vituhu kwa wingi wa samaki.
[7] Aho yuda mhina mwekuwa
akakundiswa ni Yesu akamwamba Petulo, “Uyu ni Zumbe!” Simoni Petulo ekusikiaho ni Zumbe, akevika gwanda da uwanga,

mana kheekuwa kadivaa akasooka mwe mazi.
8 Akini wada wahina watuhu watimiya phwani kwa ngaawa uku wabuuta wavu wekumemao samaki, khawekuwa hae na si khavu, iya neeiwa yapata mita mia mwenga kubua khandakhanda ya mazi.
9 Wekubuaho si khavu waona moto wa makaa ugimbwa, uwanga yakwe kuikwa samaki na bumunda.
10 Yesu akawamba, "Eteni aha izo samaki wacheche mwekuloazo."
11 Simoni Petulo akakwea ngaawa na kuubuuta uda wavu adi si khavu. Nee umema samaki wakuu mia mwenga hamsini na ntatu na etiho wawa wangi, akini wavu khawekudumuka.
12 Yesu akawamba, "Sooni mde." Khahana katu yumwe wa wahina mwekugeeza kumuuza wee undai? Kwaviya wammanya ni Zumbe.
13 Yesu akeza, akadoa bumunda akawekha, akagosoa ivyoivyo na wada samaki.
14 Inu nee iwa maa ya ntatu Yesu kuwaawiiya wahina wakwe bada ya kuyuyuka.

*Yesu atamwiiya na Petulo*

15 Wekubindaho kuda, Yesu akamuuza Simoni Petulo, "Simoni mwana wa Yohana, Ivi wanikundisa kusima awa?"

Naye akatambaisa, "Eehe, Zumbe wamanya ati mie nakukundisa."

Yesu akamwamba, "Wakauwe wanangoto wangu."
16 Naho akamwamba kakaidi, Simoni mwana wa Yohana, "Ivi wanikundisa?"

Petulo akamtambaisa, "Eehe Zumbe wamanya kuwa nakukundisa."

Yesu akamwamba, "Wakauwe ngoto zangu."
17 Akamuuza maa ya ntatu, "Simoni mwana wa Yohana! Ivi wanikundisa?"

Aho Petulo akasuumia mwe moyo wakwe, kwaajii ekumuuzavyo maa ntatu, "Wanikundisa?" Akamwamba, "Zumbe, wee wamanya yose ati miye nakukundisa."

Yesu akamwamba, "Wakauwe ngoto zangu.
18 Nakwamba ukwei, wekuaho mbwanga, kwezoweya kweika mwenye tayali na kuita kokose wekukundako. Akini wendaho uwe mdaa wenda wenue mikono yako na mntu mtuhu endaakufunge na kukwegaa wesakokukunda uite."
19 Kwa kugombeka ivyo, koonyesha Petulo ufe wakwe wendavyouete ukuu kwa Muungu. Naho akamwamba, "Nitongea."

*Yesu na mhina mtuhu*

20 Aho Petulo akahituka, akamuona mhina mtuhu yuda ekukundiswae muno na Yesu ambasa, uyu mhina ni yuda kisingi cha khande ya guoni kekaa hehi na Yesu na kumuuza "Zumbe ni yuhi endae akuhituke?"
21 Petulo ekumuonaho yuda mhina akamuuza Yesu, "Zumbe, na uyu vihi?"
22 Yesu akamtambaisa, "Ati nakunda asigae adi nendaho niuye, yakuusu mbwai? Weye yakundigwa unitongee."
23 Nee mbui iyo ikazagaa gatigati mwa wantu wekumzumiiya Yesu kuwa mhina uyo khana auye na nyuma, akini Yesu kheekumwamba inga mhina uyo khana auye na nyuma, akini kagombeka, "Inga nikakunda asigae adi msi nendaho neze, wakunda mbwai?"
24 Uyo ni yuda mhina mwekuvuhuzia mbui izi na kuziandika, naswi tamanya uvuhuzi wakwe ni kwei.

*Kisiikizi*

25 Naho kuna mbui nyingi ekugosoazo Yesu, ayo inga nee yaandikwa yose dimwe kutongea ntuhu, namamakhanya mwe inusi yenye khavyekuwa vikaiganiya kuviika vitabu ambavyo nee viandikwa.